

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**MSAMBWENI CONSTITUENCY, HELD**

**AT JOMO KENYATTA PRIMARY SCHOOL**

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

**ON**

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

[REDACTED]

**MONDAY, 6<sup>TH</sup> MAY 2002**

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, MSAMBWENI CONSTITUENCY, HELD AT JOMO KENYATTA  
PRIMARY SCHOOL, ON MONDAY, 6<sup>TH</sup> MAY, 2002

**Present:**

Com. Prof. A.I. Salim  
Com. Domiziano Ratanya  
Com. Kavetsa Adagala

**Secretariat in Attendance:**

Collins Mukewa - Programme Officer  
Fidelis Wangatta - Asst. Programme Officer  
Grace Gitu - Verbatim Reporting  
Lucy Atieno - Sign Language Interpreter

**Meeting was called to order at 9.00 a.m. with Com. A.I. Salim in the chair.**

**Com. Salim:** Samahani hatukuweza kuanza hapo mapema kabla ya sasa, kwa sababu ya shida za mitambo na ni lazima mitambo ifanye kazi ili tuweze kunasa maneno yote ambayo itasemwa, na maoni yote yatakayosemewa hivi leo. Lakini tunaambiwa kwamba sasa tunaweza kuanza na ningependa/au tukaanza kwa “dua” au maombi ma mtu atufungulie mkutano wetu, tafadhali. Tuna nani? Karibu.

**Sheikh Maombi:** Ewe Mwenyezi Mungu sifa njema ni zako na wewe ndio mlezi wa vyumbe vyote, tunakuomba utupe rehema zako leo. Ewe Mwenyezi Mungu wewe ndio mwingi wa rehema tunakuomba uhimize rehema zako katika sehemu hii ya leo. Wewe Mwenyezi Mungu wewe ndio Falme wa malipo, tunaomba malipo yako yaweze kutimia hapa leo tuweze kupata malipo, sisi na jamii ya watu wote wa Kenya. Ewe Mwenyezi Mungu tuongoze njia iliyo nyooka *yahrab kulalamina* isipokuwa njia ile ya wale waliopotea wala wale ulio wakasirikia. Ewe Mwenyezi Mungu ujalie mkutano wetu huu uwe mkutano wa heri na mkutano wetu huu uwe wa masikizano na maafikiano na yale tutakayo yazungumza, yaweze kuwa na kipawa cha kuweza kutumika katika Kenya hii. Mwenyezi Mungu tupe katika dunia hii mem na kesho *alhera* utupe mema na utujalie sisi zote na jamii ya weingineo wote, utwe na afya nzuri na matekelezo mazuri. Kwa hayo Mwenyezi Mungu tunakuomba utuchukulie yale ambayo tumekusudia na tunakuomba umpatie rehema bwana wetu akiwa Mohamed wa salaam na jamii ya waislamu, na jamii ya watu wa Kenya. Kwa hayo Salaam Aleikum..

**Com. Salim:** Aleikum Salaam. Asante sana kwa maombi na “dua” na inshallah mungu atatupa kufaulu katika kazi yetu hii. Nianze kwa kuwajulisha wenzangu hapa na kujijulisha mwenyewe. Mimi naitwa Ahmed Idha Salim, mimi ni Commissioner, na ni naibu wa mwenyekiti wa Tume ya kurekebisha Katiba. Na kwa upande wangu wa kushoto, ninaye mwenzangu Kavetsa Adagala Commissioner, ambaye kwa miaka mingi amekuwa akisomesha katika mpaka leo anasomesha katika Chuo kikuu cha Nairobi, mbali na kazi zake hizi za Tume. Upande wangu kuna mwanafunzi wake yuko hapa, Districti Co-ordinator bwana Mkalla, kati ya wanafunzi wengi ambao tunakutana nao hapa na pale. Na kwa upande wangu wa kulia, ninaye Commissioner

Domiziano Ratanya, ambaye pia ni mtu mwenye hekima na maarifa na ujuzi na experience ya miaka mingi katika serikali yetu ya Kenya, akishughulika katika Provincial Administration kwa miaka mingi. Pia, ni mzee mashuhuri katika eneo lake la Meru. Basi upande wangu pia tunaye District Co-ordinator wetu bwana Mkalla ambaye bila shaka mwamjua, na pia tunawana kamati ambao washughulika katika kazi hii muhimu ya kuhamazisha jamaa waliopo eneo hili katika mambo hayo ya kurekebisha Katiba. Na ningemuomba labda yuko mwenyekiti wa kamati hapa? Lakini labda bwana Co-ordinator ungewajulisha wale walioko na wananchi.

**Mweru Mkalla – D.C.:** Wananchi wa Msambweni Salaam Aleikum! Asante sana Prof. Idha Salim, Kaimu mwenyekiti wa Tume ya kurekebisha mambo ya Katiba katika Jamhuri yetu ya Kenya, na wanatume ambao mumeandamana nao. Kabla sijaendelea mbele ningeuomba pia kuwajulisheni District Officer wa Msambweni Division ambaye yuko hapa bwana Tergon, wasalimie wageni wetu tafadhali. Halafu na mwenyeji watu mwalimu mkuu wa shule hii bwana Bashir ambaye ameturuhusu tukaweza kukaa hapa pamoja siku ya leo. Halafu kuna wanakamati ambao wako hapa, Councillor Mohamed Buso, wanakamati wa Msambweni Constituency Committee, halafu kuna ndugu Ramadhan Tarai ambaye anasajili wale ambao wanafika hapa kutoa maoni yao siku ya leo. Halafu kuna baadhi ya wanakamati ambao wako Diani Youth Polytechnic, kuandaa na kuangalia kwamba sherehe hii inaendelea vilivyo siku ya leo. Na kuna mwingine ambaye atakuja kuwa nasi siku ya leo, pia na mzee Suleiman Bakari pia yuko hapa, yeye pia ni mwanakamati wetu, na kuna mwingine ambaye tunamtarajia aweze kukuja. Mimi ni Mweru Mkalla, Co-ordinator na nashukuru wote ambao wamefika hapa na tutaanza shughuli yetu siku ya leo na tuko hapa mpaka mtakapomaliza kuchukua maoni yetu. Karibuni. Na ninakumbushwa kwamba nimjulisha Councillor Chibunda wa Lunga Lunga, salamia wananchi. Na wale wageni wote ambao wamefika kutoka Nairobi na wale walimu wetu ambao wanafundisha Civic Education pia wako hapa, karibuni pia na wananchi wote wa Msambweni.

**Com. Salim:** Pia tunao kati ya staff au wafanyakazi wa Tume, kwa upande wangu wa kushoto kwa ile meza, yuko Fidelis, ambaye ni Assistant Programme Officer na pamoja naye pale yuko Lucy, pia tunaye Collins, Programme Officer mwenyewe, ambaye ameshughulika na mambo mengine kuhusu kikao hiki, na wote hawa kazi yao ni muhimu sana. Vijana kazi yao ni kusajili kwa mkono kila jambo ambalo linasemwa hapa, mbali na mitambo kuwa yatanasa kila neno ambalo litasemwa hapa. Hii ni muhimu ili kwamba tukirudi tujue kikao hiki cha Msambweni ilisemwa mambo gani. Lucy pale anakazi pia muhimu ingawa hatujaona mtu ambaye twahitajia kazi yake, yeye ni mtafsiri kwa ishara ya mkono, mambo yanayosemwa kwa wenzetu, ndugu zetu, dada zetu ambo hawawezi kusikia vizuri. Sifikiri yuko mtu hapa ambaye ana taabu hii au tatizo hilo, lakini ikiwa yuko, Lucy yu tayari kusaidia katika kazi hiyo. Kwa ufupi tuko tayari kabisa kusikiza maoni yenu.

Hii ni kazi muhimu sana sina haja kupoteza wakati, tumekwisha poteza wakati wa kutosha. Kazi muhimu sana ya kukusanya maoni ya wananchi, juu ya kazi hii kubwa ya kurekebisha Katiba. Ni mara ya kwanza wakenya wana nafasi ya kurekebisha Katiba yao. Katiba kama mjuavyo, ndio sheria kuu kabisa nchini, hakuna sheria yeyote nyingine ambayo yaweza kupinga Katiba. Ikiwa kuna sheria yeyote ambayo yapinga Katiba, basi sheria hiyo ni “baapen” tusemavyo sisi waislamu, haina msingi na haiwezi kutumiwa. Kwa hivyo mko na kazi kubwa sana, maana maoni yenu ndiyo ambayo yataumba hiyo Katiba.

Nikutegemea maoni ya wananchi, ndipo tutakapoweza kuandika hii Katiba, si maoni yetu lakini maoni ya wananchi. Kwa hivyo “*inshallah*” wale jamaa walioshughulika na Civic Education kati yenu, kwa miezi hivi sasa, pia wanakamati wanaohusika na kazi hii ya kurekebisha Katiba, wamekuwa wakifanya kazi yao ya kuhamasisha, kueleleisha, kuwaambiwa ni mambo gani yaliyomo katika Katiba ya leo. Kwa hivyo ni mambo gani ambayo nyinyi mwafikiri kwamba yapasa yabadilishwe, au mambo gani mapya ambayo hayako kabisa katika hii Katiba ya leo, ambayo yapasa yaweko katika hii Katiba. Na bila shaka mko tayari hivi leo kutoa maoni yenu.

Na njia ambayo tutaifuata ni kwamba moja wenu atapewa nafasi ya kutoa maoni yake, kufuatia hii ratiba iliyoko katika registration form. Aliyekuja kwanza ataanza yeye na huyo atapewa dakika tano ikiwa ataka kutoa maoni yake kwa mdomo tu. Samahani wakati ni muhimu, hatujui watu wangapi wengine watakuja baadaye. Na tungependa kuondoka hapa baada ya kila moja wenu amekwisha kupata nafasi ya kutoa maoni yake. Kwa hivi sasa, kwa hivyo dakika tano kwa kila moja wenu anataka kutoa maoni yake kwa mdomo. Na ikiwa una Memorandum – mswaada, ushaandika maoni yako hapo, basi utapata dakika tatu, maana baadaye tutasoma Memorandum yako kwa makini tukirudi Nairobi. Kwa hivyo hatuna haja ya kukusikia sana hivi sasa, lakini wenzako hapa na sisi pia tungependa utudokezee tu kuna nini katika mswaada wako. Points gani zilizoko, mapendekezo gani ambayo unayo ya kutupa. Na hivyo pia ni jambo muhimu, maanake baadala ya kutupa ile background ya malalamiko na mashtaka, sisi ni wakenya kama alivyokuwa akisema mwenzangu, Commissioner Adagala. Twajua matatizo yaliyoko. Tupeni mapendekezo, matatizo hayo tunaweza kuyarekebisha vipi? Tutayatatia vipi? Tuseme kwa mfano, mushkil wa mashamba, mushkil wa ardhi – una mapendekezo gani juu ya mushkil au tatizo la ardhi au mashamba na kadhalika? Au aina ya serikali ambayo tungependa iwekwe hapa. Ni aina gani, bila kutuambia serikali ya hivi sasa ni hivi, ina tatizo hili na lile na kadhalika. Hao tunajua, tunajua aina gani ya serikali tunayo. Sema tu, tungependa mabadiliko gani yafanyike, au mimi sioni jambo lolote mbaya katika serikali tunayo. Tuibakishe hii serikali kama ilivyo sasa na hiyo itatosha, tushapata oni lako. Serikali ambayo wewe wapenda ni hii, ambayo tunayo hivi sasa. Mbunge awe na miaka mingapi katika bunge, tatu, nne? Bila kueleza historia au vile bunge ilivyo na mbunge anakazi zake vile ilivyo. Nafikiria tumefahamiana.

Basi bila kupoteza wakati mwingi zaidi, moja kwa moja ningependa kumuita mwenzetu wa kwanza hapa aliyejiandikisha, bwana Rashid M. Barua ambaye naona kwamba ana Memorandum kutupa. Kwa hivyo nitampa dakika tatu maximum, juu kabisa. Pia mwenzangu ameniambia jambo muhimu, tungependa kuona chumba hiki kimejaa watu wa aina tofauti, tofauti vijana, wazee, kina mama. Nimwonae dada hapa ni mmoja tu, ningependa kuona wengi zaidi, labda wengi kuliko kina baba na ndugu. Kwa hivyo tunatumai kwamba baadaye watakuja kina mama wengine hapa kumpa support huyu mmoja aliyefika. Pia tungependa kupata maoni ya wale ambao wahisi kwamba wamewekwa kando katika jamii. Kama walemavu, yuko mlemavu hapa hivi leo? Hayuko. Twatumaini au twataraji kwamba atakuweko baadaye, kutueleza taabu zao hao jamaa ambao wamewekwa kando na kadhalika. Asanteni. Sasa moja kwa moja kwake bwana Rashid M. Barua. Bwana Rashid tafadhali utakaa pale, utueleze dakika tatu tu.

**Rashid Mohamed Barua:** Mimi ni Rashid Mohamed Barua, nikitoa maoni yangu kwa Tume la marekebisho ya Katiba na

maoni yangu yameambatana na Memorandum niliyoiandika. Lakini kwanza ningependa niseme katika Memorandum yangu, kitu cha kwanza katika area hii yetu tumekubaliana kwamba tunataka serikali iwe ya majimbo. Pia tumekubaliana pia au tumefikiri mpaka tukaona uwezo wa Rais au President upunguzwe, kwa maana ni ya hali ya juu sana ambayo hatuwezi kustahimilia. Kitu kingine tumesema mamlaka kama vile ya County Council, pawe mamlaka kamili ya kusimamia yenyewe mambo yao. Na province iwe hivyo hivyo ipewe mamlaka ya kusimamia yenyewe mambo yao. Na ikiwa basi ni lazima 75% ya hizo pesa au ya kodi ibaki kwa lile jimbo lenyewe, 25% ipewe kwa serikali kuu.

Na katika uchaguzi tumesema kwamba tumesikia etu mtu awe wa University, awe nini, twasema representation sio lazima iwe ya elimu. Yeyote anaweza kuwakilisha watu, kwa hivyo tunataka, si lazima ya elimu fulani. Lakini tunataka representation iwe fair kwa watu wote, sio kuchagua elimu, hapana. Elimu kama iko, basi kwanzia form four kwenda mpaka juu. Pia tumesema muda wa President uwe vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Hiyo tumesema tumeona vigumu kwa upande fulani.

Upande wa chief au wamakazi tuwe na vipengele kama vifuatavyo. Mtu, yaani tukishakuwa na District Educational Court ya kiislamu, ikienda kwa District ya kiislamu, ikienda kwa province ya kiislamu kuwe na other positions za huo mlolongo wa dini ya Islamu. Sio tu kumalizia kwa Chief Kadhi halafu imalizike. Location kisha iende kwa District, kama hawajapatana waende kwa Kadhi, kama hawajapatana waende kwa High Court ya kiislamu. Sio kwa High Court ile ya maoni ya watu wa kawaida, High Court ya kiislamu. Na hiyo ikiwezekana hapo tukiwa na Chief Justice wa mambo mengine, kuwe na Chief Justice wa mambo ya kiislamu katika Islamic Court.

Sasa upande wa elections: Upande wa elections tunataka pale patakapo pigiwa kura zihesabiwe pale pale, sio kuchukuliwa kutoka Ganjoni, Msambweni zikipelekwa mahali fulani. Hiyo hatutaki, maana tunajua kwamba kutakuwa na corruption during transit.

Haya habari ya maji: Tumesema maji yana gharama nyingi kwa watu. Sasa watu wanalipa gharama nyingi, tumesema ziwe chini kabisa, iwe free kwa maana ni kitu kimoja essential kwa raia, kwa hivyo iwe free.

Mambo ya communication kama vile simu na vitu vingine kama vile umeme zipunguzwe bei, ili kila mwananchi zimfikie.

Elimu: Tumesema kuna Universities nyingi huko nje, na sisi tunataka usawa. Kwa hivyo lazima watu wa Pwani wawe nao wanaonekana na wanapewa University yao au zao Universities. Elimu ya bure kwa watoto wote, wakiwa wa aina yote, wakiwa disabled, wakiwa nini, wote elimu wapate bure, na iwe bure.

**Com. Salim:** Bure kuanzia wapi mpaka wapi?

**Rashid Mohamed Barua:** Kuanzia nursery school to form four.

**Com. Salim:** Endelea.

**Rashid Mohamed Barua:** Hospitali: Tumeona kwamba kuwe na total freedom of hospital services “red” bure, ile inaitwa bure ambayo haina madoadoa, kuliko hii ya sasa kwa maana ina madoadoa kuna sijui cost-sharing. Sasa pia imegeuka imekuwa ni cost-tearing, sasa tunataka iwe free. Education, I mean medical.

**Com. Salim:** Wakati wako umekwisha.

**Rashid Mohamed Barua:** Wangu? I am sorry you did not give me a signal.

**Com. Salim:** Right now I have given you a signal.

**Rashid Mohamed Barua:** Laughter, okay nishamaliza kulingana na rules ulizoniambia na mimi huogopa sana wakati. Kwa hayo machache, nasema asante sana kwa kupata wakati huu. Hata hivyo ningepomba niwakabidhi hii Memorandum.

**Com. Salim:** Asante. Mwenzangu ana swala moja kufafanua hayo uliyoyasema.

**Com. Ratanya:** Bwana Rashid, umesema kwamba kuwe na Chief Justice wa Islamic. Na sasa tuna Chief Kadhi, sasa unataka waendeleo pamoja ama mmoja awe mkubwa zaidi au mdogo ama wawe namna gani? Wafanye kazi aje?

**Rashid Mohamed Barua:** Kuwe na Chief Justice lakini tunataka awe Chief Kadhi halafu pale juu kuwe na Chief Justice dealing with Islamic problems.

**Com. Ratanya:** Achaguliwe na nani?

**Rashid Mohamed Barua:** Atachaguliwa kama vile vyama kama Supkem kama vile baraza la maimamu. Lakini lazima wahakikishe kwamba anayo elimu ya kufaa.

**Com. Ratanya:** Achaguliwe na President ama ni waislamu?

**Rashid Mohamed Barua:** Hapana President, waislamu wenyewe. Sisi tumesema twataka kuondoa mamlaka mengine huko.

**Com. Salim:** Sasa namuita bwana Bakari M. Koja.

**Bakari M. Koja:** Asante bwana Commissioner. Mimi jina langu naitwa Bakari Koja Mwasime na nimeshiriki hapa kutoa maoni yangu, juu ya marekebisho ya Katiba ya nchi. Na ninaamua kuzungumzia juu ya mahakama. Katika mahakama, mimi naona kuwe na mahakama huru ambazo zitaidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo. Kuwe na Supreme Court headed by the Chief Justice, halafu kuwe na High Court which should include Kadhi's court. Halafu kuwe na Court of Appeal pamoja na Islamic Court of Appeal, halafu kuwe na Magistrate's Court, kuwe na Kadhi's Court na kuwe na Marshall Court.

Baada ya hapo, nitazungumzia kuhusu hisima kama za kiislamu. Kuwe na Islamic Court of Appeal, yaani ikuwe na Chief Kadhi, kuwe na Principal Chief Kadhi, kuwe na Senior District Kadhi, kuwe na District Kadhi class one, class two na class three. Halafu kuwe na Islamic Tribunals at the grassroot level. Yaani kwa mfano, zianzie kwenye location huku halafu Division, halafu District kwenda huko mbele. Kwa hivyo hii ni mambo ya mahakama kwa sababu ni kitu ambacho ni cha muhimu sana kwa wananchi, basi ianzie from the grassroots. Halafu Chief Kadhi awe na cheo na heshima sawa na ile wanaopatiwa majaji wa mahakama kuu hivi sasa. Na umri wake uwe kuanzia miaka arobaini na tano na kuendelea. Wale Kadhi wengine wanzie miaka thelathini na tano na kuendelea.

**Com. Ratanya:** Chief Kadhi miaka ngapi?

**Bakari M. Koja:** Aanzie arobaini na tano and above. Forty-five and above.

**Bakari M. Koja:** Halafu mahakama lazima ziwe karibu na watu, kama nilivyosema kuanzia hapo kwenye location, division, district, provincial, halafu national na court of appeal.

Halafu, kitu kingine ni utawala: Mamlaka ya utawala wa nchi yaanzie kwa watu wenyewe ambao wako huru, pale waishipo kwenye maeneo yao ya upigaji kura.

Serikali ya mitaa na local authorities: Wakenya lazima watawaliwe kupitia makubaliano yao na maoni ya utashi wao, yaani iwe na their will and consent. Serikali lazima iongozwe au iongoze kufuatana na Katiba ya nchi, na sheria za nchi ambazo zimekubaliwa na wananchi wenyewe, na kuhidhinishwa na Bunge hii. Raia lazima wawe na uhaki wa kufanya maandamano ya amani, kwa lengo la kuirekebisha serikali endapo maongozi ya serikali hiyo, yanakiuka Katiba au sheria za nchi, maslahi ya wale wachache walio kwenye mamlaka. Vyombo vya kulinda usalama kwa raia, lazima tujue na kutambua kwamba majukumu yao ni kuwalinda raia na mali yao. Hivyo wao ni watumishi wa umma na wala sio ..... ndio bwana.

**Com. Salim:** Samahani unasoma Memorandum?

**Bakari M. Koja:** Haraka, haraka. Ni maoni yangu lakini nimeyaandika kama Memorandum. Kama unataka naweza nikakupea.



**Com. Salim:** Tunaweza kuchukua, lakini kwa kuwa hatuna wakati na ni ndefu hautaweza kuisoma yote.

**Bakari M. Koja:** Bado mbili nimalize.

**Com. Salim:** Haya.

**Bakari M. Koja:** Kwa hivyo nimesema vyombo vya kulinda usalama wa raia, lazima vijue na kutambua kwamba majukumu yao ni kulinda raia na haki zao, au na mali yao. Kwa hivyo wao wajue kwamba ni watumishi wa umma, wala sio watawala kama inavyodhihirika sasa. Raia au wananchi peke yao ndio wenye mamlaka au uwezo wa kuyatoa mamlaka waliyoyapa serikali yao, pingi tu serikali itakapozitukana sheria za Katiba ya nchi hii. Mwisho, tunasema kila mkenya lazima awe na haki ya kudumisha, kuridhisha na kuendeleza mila na desturi na tamaduni za kiasili, ambazo zinaambatana na haki za kibinadamu na demokrasia. Kwa maana hiyo, serikali lazima iendeleze, ihifadhi, na itukuze lugha ya wakenya. Serikali lazima itoe na kuendeleza tamaduni zinazoambatana na sayansi na maendeleo ya ufundi katika jamii za wakenya, kufuatana na mazingira ya makao yao na itakadi za imani za dini zao. Asante sana.

**Com. Salim:** Asante sana bwana Bakari M. Koja. Tafadhali utaenda pale ujisajilishe kuwa umetoa maoni. Bwana Ali H. Njama.

**Ali Hassan Njama:** Kwa jina naitwa Ali Hassan Njama na maoni nitatoa kuhusu mfumo mpya wa Katiba, na maoni yangu ni ya mdomo na Memorandum kwa jumla, kulingana na makala yangu ambayo nimeandika.

**Com. Salim:** Kwa hivyo ni dakika tatu.

**Ali Hassan Njama:** Sawa. Ninasema mfumo wa Unitary Government ambao uliopo unatawala sasa umeshindwa na kuchangia maovu mengi katika nchi hii ya Kenya. Kwa hivyo napendekeza tuwe na serikali ya Majimbo. Kwanza katika mada yangu, ya kwanza nimezungumza katika nyanja ya elimu. Elimu katika mitihani ya kitaifa inayofanyika huwa kuna maonevu sana. Maneno haya nilifanya utafiti katika shule mbali mbali, katika mikoa mitatu, Coast, Nairobi na Rift Valley. Katika wanafunzi ambao wamesajiliwa katika vyuo vikuu wa Coast Province ni wachache sana, kulinganisha na idadi ya province zingine.

**Com. Salim:** Pendekezo?

**Ali Hassan Njama:** Pendekezo langu ni kuwe na usawa, kwa sababu wananchi wa mashambani shule zao si nzuri. Mtoto kama amepata B- huyo already in mtu ambaye ana uwezo wa kuwa aende University, sio lazima amekosa one mark anaachwa

nje wasiende University. Halafu katika baraza la kusahihisha mitihani iwe kunafuatwa usawa, kwa sababu nikinukuu gazeti la mtihani uliofanyika 1994, 1995 wakati wa shule ya Musa Gitau Primary School ilipoanguka, wazazi wakasema hawakuridhika na matokeo hayo, wakalipa pesa zingine za mtihani, mtihani ukawa remarked, wakawa maeshinda. Wanafunzi wao wakawa wameshinda mtihani, je wa kama sisi wanyonge ambao hatuna uwezo wa kutoa pesa mtihani uwe remarked, matokeo yake ni nini?

Nimependekeza mapendekezo yangu mengine katika mali ya asili, kwa mfano mimi hili ni eneo langu la ardhi ambalo lina ni help halafu papatikane madini, madini yakipatikana katika serikali za mfumo wa majimbo ama mfumo mwingine, mimi siwezi kuondolewa hapa kwanza, mpaka niwe nitajengewa nyumba, niwe nitapata share katika mali ile ambayo imepatikana pale. Kama sasa mafuta mumeambiwa yamepatikana Kwale District, lakini wananchi wa Kwale hawajahusishwa wakaambiwa mafuta yako sehemu gani, itawaadhiri vipi, watapata nini? Madini mengine kama ya Titanium ambayo ilipatikana Maumba, tunadhulumiwa sana ambapo mwananchi leo anaambiwa atalipwa elfu tisa na ambapo sioni watachukua pesa nyingi ambayo madini hayo ya Titanium ni metric tonnes 200,000,000 (two hundred million).

**Com. Salim:** Yote hayo tuyajua. Pendekezo.

**Ali Hassan Njama:** Pendekezo. Tunataka mali ile kama imepatikana pale, mwananchi awe na share na mpaka kufa kwake na wajukuu zake. Nina dakika ngapi? Napendekeza kama serikali za wilaya, mikoa kama vile wenzetu wa Maasai Mara wanavyopatiwa collection tax ile ambayo wanachukua, na sisi Hotel Industry ambayo 75% inapatikana Coast Province, levy ambayo itachukuliwa ipelekwe kwa County Council ili tuweze kujiendelesha katika mambo yetu. Mambo ya utawala .... (intejection).

**Com. Salim:** Mnataka percentage maalum au?

**Ali Hassan Njama:** Tunataka percentage maalum.

**Com. Salim:** Percentage ngapi?

**Ali Hassan Njama:** Tunataka 75%.

**Ali Hassan Njama:** Halafu lingine hospitali ziwe za bure, kwa sababu wananchi sasa katika taquim ambazo zilifanywa na UNICEF ni kwamba, watoto wengi katika Kwale District hufa kabla, akizaliwa hamalizi muda wa miezi mitatu au miezi sita anakufa. Na hili ni swala nyeti ambalo serikali haijashughulikia ki sawa sawa.

**Com. Salim:** Pendekezo?

**Ali Hassan Njama:** Pendekezo, nataka utafiti ufanywe na kama kuna shida yeyote, serikali ichukulie kama janga la kitaifa na tuhakikishe tunaishi kama vile wenzetu wa Europe ambao mtu anaamua kuzaa mtoto mmoja, na ana guarantee kwamba ataishi. Kwa hayo machache nitawapa Memorandum. Asanteni.

**Com. Kavetsa:** Kwa upande wa - microphones ziko wapi? Upande wa elimu umesema mtoto wa mashambani akipata B-apelekwe shule, University. Lakini unajua University hubadilika badilika depending on performance. La kwanza hilo, sasa wewe unasema kuwe na quota system ya rural areas?

**Ali Hassan Njama:** Ndio.

**Com. Kavetsa:** Okay. Kwa sababu inafaa useme ndio tujue unasema vipi.

**Ali Hassan Njama:** (inaudible).

**Com. Salim:** Asante bwana Ali Hassan Njama kwa maoni yako. Tafadhali enda pale ujisajilishe. Bwana Halfani Wasumu.

*Interjection (conversation inaudible)*

**Com. Kavetsa:** Tumefanya mahali kwingine na inatokea sawa. Ni hili lakutoa pendekezo, pendekezo.

**Halfani Mwasuma:** Inaudible.

**Com. Salim:** Si kuwa tunahaja ya kumharakisha mtu au kumnyima nafasi ya kutoa maoni yake, la hasha. Kwa hakika kwa ajili ya wakati ni mfupi na kwa experience yetu hapo kwingine, tuliona kwamba mtu atakasirika zaidi ikiwa atajiandikisha, kisha tukimaliza kazi zetu awe hajapata nafasi, kutoa maoni yake. Hafadhali kumpa kila mmoja nafasi ya dakika chache kuliko kuwapa wachache, nafasi ya kusema kwa wakati mrefu zaidi. Hii ndio sababu.

**Halfani Mwatsuma:** Umesema ni dakika tano.

**Com. Salim:** Kwa ajili ni dakika tano ikiwa mtu anataka kusema tu. Lakini akiwa ashaandika, na kama ndugu yetu Sheikh Ali hivi sasa, alikuwa na Memorandum, alitoa mapendekezo yake, kisha Memorandum tutaisoma kwa makini baadaye. Kwa hivyo tujaribu kuendelea hivi, ikiwa tutaona kwamba idadi ya watu haitazidi, tutazidisha wakati “inshallah”. Sawa bwana Gaso. Ikiwa watu hawatazidi, idadi yao haitazidi, tutawapa watu wakati mrefu zaidi. Lakini tunaogopa kwamba baada ya kila nusu saa, jamaa kumi watafika. Na siku yetu ni hii moja tu. Tutajaribu tuseme, we will leave it open bwana Kadhi. Sawa, ikiwa

tutaona idadi ya watu haikuzidi, mtaongezewa wakati. Haya shukrani. Naam, bwana Halfani, ni Omar. Halfani Omar.

**Halfani Omar:** Naitwa Halfani Omari Mwatsuma, mzaliwa wa Msambweni location. Ninataka kupeana mchango katika Tume ya marekebisho ya Katiba, na mchango huu unahusiana na swali ambalo liliulizwa kwenye pamphlets ambazo swali lenyewe linahusiana na Commission ambazo zingeongezewa, ama ziwekwe ndani ya Katiba inayokuja. Na kujibu swali hilo, nilikuwa nimeandika karatasi kwamba, I wish to make the following presentations in answer to the above questions or to the questions I am saying. I would urge for the inclusion of a body to be called the “The Joint Admission Commission:”. It’s composition will be two people from each of the provinces of the Republic of Kenya. This Commission, when established, should be given the task of enrolling candidates in all colleges or professional studies in the Republic. Like the college of Health Profession, Teacher Training College, Kenya Armed Forces, Kenya Police, Prisons, Administration Police and Kenya Universities, this is to mention just but a few, although they wish to make ...(inaudible). This implies that, should vacancies arise from those national institutions or colleges, the Commission should be informed and colleges should only wait for students admitted by the Commission.

If this is done will instil fairness and proper tribal balance in the institutions or colleges, than a case where about 30% or more of the candidates, can communicate in one language. If this is done also, confidence of students in secondary schools will increase, since qualifications will be a criteria for intake. Since the chances will now be open to all in the Republic. Justice will be the shield and defender and not power. Faith will be restored to the Government machinery. I mean the public will restore their faith to the Government machinery thing, they will account for it as their property. Look at a case where, as we are all aware that learning at the Coast started as far back as 1910 and back.

**Com. Kavetsa:** What you are saying, we are all aware. Give us your proposals. It is a very important thing if you would give us your proposals than you give us the history, because we are all aware of the rest.

**Halfani Omar:** Okay. Learning started as far back – I have removed that word.

**Com. Kavetsa:** No. We don’t want you to remove the word, we don’t want you to make us aware again. We want a proposal.

**Halfani Omar:** Yes, I have hear you.

**Com. Salim:** You are recommending kwamba kuwe na Joint Admission Commission. The reason why you want that is to create fairness to secondary schools to all equally; and you also told us that in the past this has not been happening and we have some areas where we have people (inaudible). You have already made the point and you have already justified why you want it. Ikiwa una pendekezo lingine sasa labda ungeendelea na hilo. Does the whole Memorandum talk of the joint commission?

**Halfani Omar:** I was signing out. Hiyo, hiyo. Ndio nimesema I am signing out. Nimesema kama educationers group yaani ilikuja 1910 hapa, lakini kutoka sasa 2002 tunakama advocate mmoja wa High Court of Kenya katika hii tribe ya kidigo kama bwana sikosei ambaye ni bwana Kitemo. Kwa hivyo, kama kugusia ni kwamba, kama ile Joint Admissioin Board kwa mfano ya Kenyan Universities ingekuwa fair na kuaangalia mambo kama haya, tusingekuwa na mmoja mbali tungekuwa na zaidi ya wale. Kwa sababu unajua such people are disadvantaged in certain areas, lakini angalia .. (inaudible).

**Com. Salim:** (Interjection).

**Halfani Omar:** Okay. Nafikiri presentation yangu ilikuwa hiyo.

**Com. Salim:** Lakini wajua labda kwamba kuna mambo mengine utakayoyataja.

**Halfani Omar:** Hapana sina. Langu ni hili tu kwa sasa.

**Com. Salim:** Kwa mfano ya Treasury na mambo ya election, mambo ya bunge, mambo ya serikali. Kwa hivyo ungetaka pengine uende ndio uweke ziwe one point.

**Halfani Omar:** Nishamaliza.

**Com. Salim:** Una Memorandum?

**Halfani Omar:** Nina karatasi.

**Com. Salim:** Unaweza ukapeana hiyo karatasi kwa Tume?

**Halfani Omar:** No problem.

**Com. Kavetsa:** Nataka kuuliza mwingine amesema hapa B- is a mark, which shoul dbe given to rural areas for University, what is your recommendation?

**Halfani Omar:** (inaudible).

**Com. Kavetsa:** No. Tunajaribu kutengeneza Kenya mpya, huyu jamaa amesema, badala ya mambo kubaki hivyo angependa iwe reviewed.

**Halfani Omar:** Wange. You are right.

**Com. Kavetsa:** Don't say how we feel. That's how it is now. Should it remain like that.

**Halfani Omar:** Itakuwa ni (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Kwa maoni yako.

**Com. Salim:** Kwa maoni yako.

**Halfani Omar:** Kwa maoni yangu, nataka iangalie quota system ya zile areas ambazo bado hazija catch up, waangaliwe kusudi wasukumwe. Ndio hiyo inaitwa quota system.

**Com. Salim:** Iwe aje au wasukumwe aje?

**Halfani Omar:** Kwa hivyo utaangalia kama hawa bila kuweka C+ hawaendi University, for such people ku-drop si vibaya.

**Com. Kavetsa:** You know, you must be aware there are other Kenyans who don't want the quota system. Na wana sababu, na wanaisema na nguvu. Huwezi kuja hapa na kusema quota system na hujaangalia, wewe utambie.

**Halfani Omar:** Kwa sababu ..... (interjection)

**Com. Kavetsa:** Sisi hatuwezi kusema. Hatutaenda na kusema Msambweni walisema quota system iwekwe. Lazima utuambie kamili ni nini. Kwa sababu wengine wanasema ni merit, meritorious na hiyo, iwe hivi, hakuna mambo ya quota system. Waalimu wako kila mahali Kenya, kwa nini waweke quota system. Wewe utuambie kwa nini mnataka quota system?

**Com. Ratanya:** Particularly, sisi tunataka maoni ya Msambweni kuwa maoni ya Central na mahali kwingine, lakini sisi tumetumwa tuje kuchukua maoni hapa Msambweni.

**Halfani Omar:** Mimi ninataka quota system kwa sababu moja. Muangalie kwamba ata kama waalimu wamekuwa spread throughout the Republic ..... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Its not the operations of the sytem, what do you want in the quota system?

**Halfani Omar:** Nataka quota system kwa sababu wengine kama sisi tuko very ... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Tell us what you want in that quota system. I am telling you it's not a debate. Ni maoni, toa maoni yako. The other person said B-.

**Halfani Omar:** I also say that it should be B-

**Com. Ratanya:** B- ya University ama?

**Halfani Omar:** Ya University. B-

**Com. Ratanya:** Wewe hauna maoni tofauti ama kuonyesha maoni yako?

**Halfani Omar:** Ndio hiyo quota system ninazungumzia.

**Com. Kavetsa:** Na ukisema tu mambo juu juu, it is upon the teacher kwa sababu wengine wamesema kwa nguvu, wanataka merit only. So if you have heard even the other person who was here said very well B-, na wewe usirudie ukisema quota system, sema what kind of quota system you want. Okay. But you have understood me now.

**Com. Ratanya:** Nasema Kenya tunaposema B- ujue kuna international assessment here, kuna hii mpaka pengine inapita watu, inapita kama D+. Sasa ukienda chini ya D+, pia ukienda D- ni kama hivyo you are still ..... (inaudible). Na wewe umesoma, mwaambie hapo ukifika hapo kiwango cha kuweza kusoma, kuendelea na masomo ... (inaudible).

**Halfani Omar:** Mimi nimesema kwa sababu allocation za hii elimu hazikuwa allocated tayari, wengine ukiweka D- utawa-knock out. Kwa hivyo katika zile areas ambazo ziko inferior .....(inaudible).

**Interjections:** (Inaudible).

**Com. Salim:** As long as there is the quota system na wale jamaa ambao katika maeneo ambapo standards na facilities kama alivyosema bwana Ali, ziko chini wasamehewe kwa lower grade, but he does not want to specify the grade. Sio, fikiria jambo la specification. Naam.

**Com. Ratanya:** Ama useme wakati wako. Si wewe utakuja kusema.

**Com. Salim:** Utapata nafasi. Lakini tushafahamiana bwana Halfani.

**Halfani Omar:** Tumefahamiana.

**Com. Ratanya:** Ufafanue wakati wako ukifika.

**Com. Salim:** Na sasa utajiandikisha, na ikiwa unataka kutuwachia hiyo Memorandum, tutachukua pia. Mheshimiwa bwana Kassim, retired MP.

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Mimi ni mmoja katika ile Memorandum iliyotolewa. Jina langu naitwa Kassim Bakhari Mwamzani. Nilikuwa mbunge wa sehemu hii kutoka 1963, sasa niko cold storage kidogo, kwa hivyo ninafuraha kuja mbele yenu na kwa sababu time ni chache nitaenda direct.

Jambo la kwanza siungani na nyinyi ma-Commissioners ya kwamba mnataka time nyingine zaidi ili mumalize hii Katiba. Hiyo mnataka tu kwa sababu, wajua mna mshahara kubwa, ma-allowance mazuri, kwa hivyo mnetaka mketi tu, lakini maoni yangu ningependa mumalize kwa sababu mkimaliza mapema ndio mtatoa wananchi wasi wasi. Lakini mkienda goigoi ili m-buy time, it will be very unfortunate. Na hii nasema kwa sababu hii habari ya Katiba haiwezi kufika kwenye villages. Hata hapa representation utaona ni hapa hapa karibu tu. Ukiangalia Vanga haiko, Kondeni haiko, Lunga Lunga haiko, wapi haiko. Kwa hivyo haya matatizo ya Katiba yalikuja na political parties. Walipoanza 1992, wanalazima ile Katiba ya multi-party, ile ya single party iondolewe mpaka ikakubalika. Wakaja na kwamba hii taratibu ya Katiba ifanyiwe Commission iende kwa watu. Hawa watu ni kina nani? Kabla ya 1963 ni political parties, ndizo zilizo represent wananchi wote hawa, wakaenda London. Na hizo political parties zilizoko katika Kenya zina represent kila mahali. Kuna wabunge humo na kila kitu. Kwa hivyo mungewaita wale political parties pamoja na wabunge mtauliza what section do you want amended? Badala ya kusema mmefika hapa, tumechukua maoni ya Msambweni, lakini mwanamke wa kawaida, wewe mwenyewe bwana Chairman, Prof. Idha amesema mwanamke ni mmoja. Why is it only one? Why? Unasikia. Kwa hivyo there is no need of adding any time.

Nikienda kwa jambo lingine ningepeda President yeyote wa Republic ya Kenya asiwe na constituency. Hii nikupunguza *joy riders* katika Presidential Elections na tumeona hata wenzetu wa Tanzania wanayo hiyo. Ni upuzi mtu hawezi kushinda akasema anataka u-president kwa sababu akikosa kuwa President aende nyumbani akalale, not constituency member, not at all.

Ningependa katika voting system, Katiba hapa voting system ya Parliament tulikuwa nayo ile ya nyuma tulipokuwa tukichagua special elected member, it was by secret vote. Siku hizi imeondolewa ni decision, go this way and the other. Those that made that opinion say I go that way and they know I went this way, unasikia. Ssa my conviction pengine nataka ni-oppose hii, lakini boss wangu yuko huku wa chama, kwa hivyo I must follow. Hii iondolewe iwe secret ballot. Katiba utu gani, kama kuna divisions katika house, iwe secret ballot.



*Interjections: (Inaudible)*

**Kassim Bakhari Mwamzani:** No, there is time for such a board.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim Bakhari Mwamzani:** When we have a decision then there should be secret ballots, not wanaopenda waende huku, wasiopenda waende huku. That's very bad. Kesho unaona magazetini watu wamekuwa publicized, hii mbaya. Kwa hivyo sheria nyingi ambazo pengine zingepita, zipite kwa sababu authority inaweza kumfanya yule mtu aki vote against, apate taabu. So there should be secret ballot.

Another thing I would like to give an idea to you, is healthcare, tulipopigania Uhuru tulisema matibabu yangukuwa bure kabisa, na sasa ni cost-sharing. Imekuwa difficult watu wanakufa kama mbuzi sasa. Kwa sababu ordinary man cannot afford a hospital, afadhali kuenda kwa mganga wa kawaida, utaulizwa kuku na shilingi nne. Lakini hospitali haiwezekani, kwa hivyo na-propose kwamba, iwe entrenched in the Constitution ya kwamba medical treatment shall be free for all. Zitatokaje pesa za kusaidia hii medical treatment? Tunahii National Hospital Insurance Fund. Hawa wote, in wengi wanalipa National Hospital Insurance Fund, lakini hakuna aliye benefit hata mara moja, kwa sababu kwanza if you go to Pandya, Aga Khan, Mombasa Hospital in Coast Province, ile allowance utakayoruhusiwa kulipiwa na fund ni one-eighth of the total cost. Na ni pesa nyingi, kwa hivyo pesa hizi, watu wa contribute for medical care through National Hospital Insurance Fund na pesa hizi zisaidie wananchi kupata matibabu ya bure. Hii naona ingesaidia wananchi wasife bure kama wanyama, kama ilivyotokea sasa.

Jambo ambalo ningetaka kuongezea kwa sababu time ni fupi kidogo, kuna section 91 ya Katiba, unapooa non-Kenyan, si umemuoa umemuleta hapa, kuna wengine wanaweza kulipa uraia wake. Kama wazungu, wahindi, they are capable of paying for their expenses. Lakini kuna hawa watu hata sisi tulio mipakani hapa, umeoa Tanzanian ama Ugandan unaambiwa uende na procedure ile ya kuchukua forms kwa Immigration na nini, ingekubalika katika Katiba wakati mtu wa Kenya atakapooa mwananchi ambaye si wa Kenya na anataka awe citizen, procedure iwe kama ya kawaida, iwe marriage certificate na udhibitisho wa kwamba ameolewa na mume, apate uraia. Lakini sasa sijaona, watu wengi hapa wakaa na mabibi ambao yeye ni Kenyan, bibi si Kenyan. Kwa hivyo, hii section ya Katiba ibadilishwe ili wapate free citizenship. Sio ile kuambiwa wakaleta passport, wa-apply passport, wa-renounce, hapana ni wa hapa tu karibu hawa. Kwa hivyo hii ni moja... (inaudible).

**Com. Salim:** What procedure should be followed?

**Kassim Bakhari Mwamzani:** The procedure should be the same, kama Professor umeenda ukaoa mzungu, si umekubali aje aongeze taifa, sasa hizo taabu apate kwa sababu gani? Iko, inasema they are entitled.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Hizo gharama ndizo nazo tuziepuke kwa sababu ordinary man cannot afford that cost.

**Com. Ratanya:** Sasa unasema iwe aje?

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Iwe simplified ili akija akionyesha documents apate.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Ukae na mtu nyumbani hajijui ma-askari wakija yuakimbia kitandani. Taabu gani bwana? Haya, ya mwisho kwa sababu time ni short, I know five minutes should have gone. Katika hii Tume recommend ya kwamba appointment nyingine ziende through Parliament. Most of the appointments ziende through parliament na zingine ziende through Public Service Commission na Public Investments Commission. Na hii twasema kwa sababu, let me go direct to a Permanent Secretary. Permanent Secretary anachaguliwa na President, disregarding any qualifications, amemchukua tu kutoka mahali popote kuwa Permanent Secretary. I say that should not be the case. That Permanent Secretary should go through Public Service Commission whether he is capable or not capable. Kuna ma-director wa institutions kama hizi Government corporations anachukuliwa mtu kutoka mahali fulani anafanywa Managing Director, hatujui ana qualifications gani. Imefika wakati hata akifanya kosa kwa sababu ni relative wa President, no action will be taken. There will be no action. Huyu amekula pesa, no action. Kwa hivyo iende through Public Investment Committee, anafaa ama hafai? Na ndio watu wengine wangepata nafasi ya kuingia huko. Sasa mambo kama haya tumeweka lakini nimeona hatukueleza sawa sawa.

Lakini appointment of political appointments should therefore be abolished. The President should be assisted by the Commission. Nafikiri nimeeleza hii ya kutosha, na ukitaka mfano naweza kuwapa.

Another thing, ambayo naiona lazima iweko ni uoga wa watu wa civil service. Katiba ingekuwa imetengenezwa ili civil servants wasitishiwe na jambo lolote wakati wanafanya kazi yao. Nasema hivyo kwa mfano, kukiwa na General Elections, kuna general elections leo utamuona village chairman, assistant chief, mpaka kwa D.C. wana wasiwasi KANU ikianguka ama NDP, au ruling party ikianguka tutafukuzwa. So instead of them wajionee kwamba ni impartial wana take part, iondolewe hii, waondolewe tashwishi kwamba hata nani akiingia they should be entrenched, hata kama wana campaign-nia party nyingine. Lakini sasa ilivyo wote ni waoga, DC yuajua akigeuka serikali atafukuzwa maanake atakayekuja ni mbaluhya. They should be protected. Security of Kenya, when you are employed as a DC or DO you are there, you will be removed by the ills you have done, not because one is elected Ford People imeingia, but whether you can .... basi awafuta moja moja. This is very unfair, we shall never get free elections. Sawa. Basi nafikiri sitaki niambiwe saa yako imekwisha, ikiwa mna swali lolote mnaweza kuuliza.

**Com. Kavetsa:** Kwa sababu wewe umekaa kwa muda kwa siasa, ulisema aja kuhusu commission hii, no extension au extension au tuwache tu, au vile tunafanya tokenism tuwache. Kwa sababu pia mkisema hivyo tunaweza kuacha kesho kutwa you know, because it's something, budget ikizungumziwa na bunge inachukua miezi fulani, ina system fulani. Sasa kama haitoshi pengine tuseme isimamishwe.

**Kassim Bakhari Mwamzali:** Nimesema Commission inauliza for more time, na mungependa kuketi hata miaka mitatu kwa sababu ya benefits. It's not bad. The benefits you are earning in that Commission.

**Com. Kavetsa:** Of what? I would like to object.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim Bakhari Mwamzani:** No. Malizeni kazi as quickly as possible, Sio kuketi tu miaka na miaka mkiulizwa, mwasema time hazitoshi.

*Interjections (Inaudible).*

**Com. Ratanya:** Mheshimiwa Kassim niko na maswali mawili. Na moja ni hii ya kupiga kura kwa Parliament. Wewe umekaa Parliament na unajua njia za kupiga kura huko ndani. Hiyo ni ndani ya Parliament si kwa wananchi. Kuna hii nasikia wanasema hayee, kuna ingine ya divisions na ya secret ballots. Sasa hapo unataka kusema hiyo ibadilishwe, Katiba hii isaidie kutupa zingine na tuwache ipi? Hiyo ni swali moja. Nataka nikuulize yote halafu ujibu pamoja. Kuna swali lingine, jibu moja moja.

**Kassim Bakhari Mwamzani:** There are two types of voting. Kuna ile ya kuuliza wanaokubali ai speaker anasema ai ... (inaudible). Wakati such members wakisimama ku-oppose kwamba speaker amekosea kwa hivyo watu waende division, watu wanaenda division. Ile ya division, wengine wanaenda huku na wengine wanaenda huku. Ndio ninasema it should be defined a method of secret balloting during that time.

**Com. Ratanya:** Hiyo ingine iondolewe?

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Hapana, itakayo ondolewa ni hii ya division peke yake. Ifanywe badala ya wanaokubali waende huku, wasio kubali waende huku, wawe members wanaenda ku cast votes without knowing whether .... (interjections).

**Com. Ratanya:** Ingingine ambayo niko nayo hapa ni mambo ya appointment. Appointments zingine unasema ziende kwa

Parliament na ingine kwa PSC that is Public Service Commission, na ingine kwa Investment Committee. Unaweza kufafanua ni appointment zipi zingeenda kwa Parliament, PSC or kwa Investment Committee?

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Appointments zote sasa ilivyo, zote zinatoka kwa Public Service Commission. Sawa, isipokuwa hii tunaita political appointment. Political appointment in kama PS, Managing Director, ushaelewa? They should go to the Public Service Commission tujue kwamba wana-qualify ama wamepewa kwa sababu ni brother and sister, you now and if perhaps they have been appointed by the President in consultation with the Public Service Commission. Alright?

**Com. Ratanya:** Hapa unasema mambo ya kuendelea kumaliza kazi ya Commission ama kupunguza. Mheshimiwa hapo unajua wewe ulianza hapa kusema mungetaka kupewa masaa zaidi, na hapo tunaongea juu ya time management. Wewe mwenyewe umeuliza saa zaidi hapa, na tukikupatia masaa mawili, mawili kila mmoja jioni tutakuwa na watu kumi tu kutoka Msambweni. Na hapo mtaenda kwa Commission mtasema tunataka siku ingine na ingine na ingine. To add for instance, saa itaendelea namna hiyo, kwa hivyo ndio mambo ya kuongeza wakati wa kumaliza kazi yanatoka hapa hapa kwa nyinyi. Kwa hivyo, mkubali hata Commission mtupatie nafasi, kwa sababu kama hakuna wakati wakutosha hatutakupatia muda umalize maoni yako.

**Kassim Bakhari Mwamzani:** Ile Commission ikipeana nafasi sawa, lakini kule kwenda taratibu mpaka tu-add more days, more months, you know. Anyway, you should try your best. Shukrani.

**Com. Salim:** Tukiendelea mbele tunaye Hussein M. Kilalo.

**Hassan Mohamed Kilalo:** Mimi ni Hussein Mohammed Kilalo, mwenyekiti wa ma Imam, Mswambweni Division. Leo, natoa maoni yangu kwa Tume hii ya marekebisho ya Katiba nikianza hivi.

Hospital za kiserikali: Operation kubwa badala ya kuwa ni Shs.1,000/= (shilingi elfu moja) iwe ni Shs.500/= (shilingi mia tano) ama ikiwezekana iwe bure. Natoa maoni tu moja kwa moja. Operation ndogo, ambayo tunalipishwa mia tano iwe shilingi mia moja, ikiwezekana bure. Mushono ambao huwa tunatozwa vile vile, huu tunautaka bure, muda mtu amekatwa anaambiwa lazima mia tano ndio afanyiwe operation. Kwa vile mambo ambayo hukuyapanga, tunataka yawe bure. Mja mzito badala ya kutozwa shilingi mia mbili na hamsini, iwe ni mia moja, ikiwezekana bure.

Huduma za kudunga wagonjwa sindano: Hii ningelipendekeza madaktari wa kiume wadunge wenzi wao wa kiume. Madaktari wa kike wawe wakihudumia kudunga masindano ma-nasi wa kike.

Sekta ya jua kali: Napendekeza kwamba serikali iwe inatia muhimu sana kwa sekta ya jua kali, hasa mashambani. Sio kuwacha hiyo sekta bure mpaka watu wanafukuzia mijini kutafuta njia.

Kadhi wa kiislamu: Napendelea maoni yangu, kila division ya waislamu, iliyo na waislamu wengi hasa kama sehemu ya Pwani, kuwe kunapatikana Kadhi ya kiislamu, kila division ama ikiwezekana kuanzia location, ili kwamba waone matatizo watayatatua vipi. Kila wilaya tuwe na Kadhi wawili. Kwa mfano Kwale tuna mmoja, sasa kwa sababu Kwale ni kubwa tupate nafasi ya kuweka Kadhi mwingine katika wilaya hiyo, ili kazi iwe na urahisi. Chief Kadhi awe ndiye mwisho wa kuhukumu kesi, sio kesi imeshinda inaambiwa kwenda kataa siri inaenda kwa mtu ambaye sio muislamu kuhukumu kazi hiyo.

Mahakama: Oni langu napendelea mtu kama amepelikwa mahakamani wakati tu anaapishwa atoe ukweli wake, naomba kama ni muislamu awe anaapishwa na muislamu mwenzake. Sio aapishwe na mtu ambaye sio kitabu chake na wala hashiki kitabu hicho kwa udhu ama kwa usafi unaotakikana.

Maoni mengine ni kuhusu hii elimu ya kiislamu, oni langu ni kwamba kulingana na hii pia ni elimu ambayo inasaidia wananchi, ningelipenda waalimu wa dini ya kiislamu wawe nao wanatunzwa na serikali hii na kupata mshahara. Ombi langu la mwisho, katika wakati kwa vile ni mchache, mengine mtasoma wenyewe, nataka ile tarehe ya kuzaliwa Mtume Mohammed Swallahu Alehi wa Wasaalam ambaye ndiye kiongozi wa waislamu, siku ile iwe public day. Hayo yanataosha kulingana na wakati. Asanteni.

**Com. Kavetsa:** Nani hulipa waalimu wa kiislamu? Wanalipwa aje, wale wa madrasa?

**Hassan Mohammed Kilalo:** Hata kama hawa waalimu wanajitolea ... (inaudible) huwa ni waalimu wale wale wa serikali ambao wanalipwa na serikali kama ni kusaidia tu, lakini wote waalimu walilosoma hata kwa hakika. Sasa wale hatukuwahesabu, tunataka wale ambao wako mashule, wanasaidia mashule, ama wale ambao wako madrasa kwa vile kuna vyuo mbali mbali. Kuna wale wa shuleni na wale ambao wana madrasa, ambao sio shule lakini madrasa ya kiislamu.

**Interjections:** Yaani kwa sasa hujitolea?

**Hassan Mohammed Kilalo:** Kujitolea tu. Pesa zetu ni mifukoni sisi wanyonge, kumchangia mwalimu.

**Interjections:** (Inaudible).

**Hassan Mohammed Kilalo:** Sasa ndio nataka mambo kama hayo na wasiojitolea wajitolee kama wana maoni watoe kwa serikali.

**Com. Kavetsa:** (Inaudible).

**Com. Salim:** Shukrani bwana Hussein M. Kilalo kwa maoni yako. Sasa namuita bwana Challe Mrina.

**Challe Mrina:** Kwa jina naitwa Challe Mrina, natoka Mamba na ninao mmoja kati ya watatu ambao tunawakilisha Zombo location. Nitaongea tu kidogo kuhusu uwezo wa Rais na mamlaka yake mikononi, I mean uwezo wa Rais. Rais kwanza awe mbunge, awe amechaguliwa mwanzo kutoka kwa sehemu yake, ndio aweze kupata kibali cha kusimamai u-Rais. Makamu wa Rais, awe wasili katika uchaguzi wa Rais, kwa maana anapochaguliwa Rais, yule anayefuata kwa kura awe makamu wake.

**Com. Salim:** Ni lazima awe running mate wake? Ni lazima awe mushirika wake katika uchaguzi.

**Challe Mrina:** Hapana si lazima, awe kutoka kwa chama chochote kile, lakini awe ni wasili kwa kura.

Baraza la mawaziri: Lichaguliwe tunavyo fahamishwa ni kwamba hii huchaguliwa na Rais. Sasa badala yake baraza la mawaziri lichaguliwe na wabunge. Hapa Rais awe amri jeshi, yaani ina maana kuwa Rais bado awachiwe uwezo wa kuwa amri jeshi mkuu wa majeshi ya silaha. Rais awe na uwezo kamili wa kutangaza vita, ila tu kupitia kwa bunge. Maana yake ni kusema, awe na ule uwezo baada ya kuwa limetajiwa bungeni ndiyo yeye awe tu na ule uwezo wa kutangaza peke yake, kama ni vita na mambo kama hayo.

**Com. Salim:** Atakayetangaza vita tu ni Rais.

**Challe Mrina:** Nikupitia kwa bunge. Iwe bunge lishaamua ndio Rais atangaze. Yaani asiwe na ule uwezo wa moja kwa moja wa kutangaza vita.

**Com. Salim:** Asipopata kibali cha bunge afanye je?

**Challe Mrina:** Asitangaze. Si halali, hayo in maoni yetu. Nafikiri nitakomea hapo, yale mengine yako kwenye Memorandum. Asante.

**Com. Salim:** Asante bwana Challe Mrina. Sasa namuita, samahani ngoja kidogo kuna swala.

**Com. Kavetsa:** Kwa maoni yako serikali ambayo itatokea kama Rais, makamu wa Rais ni runner-up, okay. Runner-up means serikali ya mseto. Niya mseto, kwa sababu ukiwa na vyama viwili mmoja ni Rais yule ambaye anapata in votes. Then it becomes a coalition government. It's not? I am asking if you know what it means, that if you have two parties because you will have two parties then in cabinet because DP will be there from a different party, President from different parties. Yes.

**Com. Salim:** Lakini maoni yako ni yale yale.

**Com. Kavetsa:** Ni yale yale tumeyaandika. Yes.

**Challe Mrina:** Rais kuchaguliwe yule anayemfuata kwa kura bila kujali niwakutoka chama gani.

**Com. Kavetsa:** Yes. But the only thing is that it will be from a different party, because kila party ina one, one, one, one. Yes, I am just clarifying so that I know that the person with next number of votes is the Vice President. It makes sense, all I want to know is to understand.

**Com. Salim:** Asante bwana Challe. Tafadhali utasajili pale. Bi Jane Suma.

**Jane Suma:** Kwa jina ni Jane Suma, mimi nimuzaliwa wa Zombo location. Katika mswada huu wa kurekebisha Katiba yetu ya Kenya, katika location yetu nilihusika kama mwaandishi wa maoni ya wananchi wa Zombo.

*Interjections:* Ngoja kidogo ... (inaudible from audience).

**Jane Suma:** Kabisa, tuliwakilisha kila kitu. Kuna wawili tumekuja nao, tuko watatu katika watu waliokuja kuwakilisha watu wa Zombo location.

**Com. Kavetsa:** Mlikutana watu wote wa Zombo location?

**Jane Suma:** Tulikutana watu wote wa Zombo location.

**Com. Kavetsa:** Na wako wapi hao watu wa Zombo location ambao mlikutana wote? Mnakubali mlikutana location nzima?

*Interjections:* .... (inaudible) from audience. Mimi ni mmoja wa wale ambao walikutana nao kwa kujadiliana kutengeneza marekebisho haya.

**Com. Kavetsa:** Kitu kikubwa nikusema mnaakilisha, mlichaguliwa?

*Interjections:* (Inaudible) from audience. Nilichaguliwa ndio nikaja hapa.

**Com. Kavetsa:** Hatutakuwa na mwingine atakuja kusema hawakuniwakilisha?

*Interjections:* (Inaudible) from audience. Nina hakika yale maoni ambayo yako pale, tulikuwa na watu ambao walihusika

katika document hiyo. Kwa hivyo haitakuwa kwamba mtu fulani hakutuwakilisha kwa sababu tulichukua maoni kutoka kwake.

**Com. Kavetsa:** Mnaita group yenu basi.

**Interjections:** Zombo location ni katika Msambweni division ambayo ina marekebisho ya Katiba. Kwa hivyo hatukuwa na fitina fulani kuwa ni watu wa kutoka Zombo location, Msambweni division.

**Interjections:** Tulikuwa na bwana Bujo ambaye ndiye Councillor wa .... (inaudible) pamoja na mama Fatuma ambaye tulikuwa naye pia kwa mkutano. Kwa hivyo hawo wakiwa hapa wanaweza kuwaeleza zaidi kama tunawaambia sawa sawa.

**Com. Kavetsa:** Lakini sawa mmefanya vizuri baadaye msikuje kusema sisi hatukuwakilishwa kwa hiyo. Haya mambo ya Katiba sio una-represent watu inafaa uwe elected.

**Interjections:** Katika hilo nina ukweli tulikuwa na mkutano na bwana chief ambaye anahusika huko katika ile electoral division ya Zombo location, kwa sababu ya marekebisho ya Katiba.

**Com. Salim:** Sawa, tumepata dhibitisho kwa hayo. Asante. Endelea mama Jane.

**Jane Suma:** Kwa hivyo nitaongea tu kuhusu upande wa haki ya ardhi na mali, na hizo zingine tutapeleka katika ..(inaudible) kwa sababu ni maoni ambayo tuliweka pamoja. Minito ya mwisho wa ardhi ni jamii ya mahali pale. Haiwezekani serikali kuwa na uwezo wa kutoa ardhi ya mtu binafsi, kwa lengo lolote. Serikali kuu na serikali ya mitaa ziwe na uwezo wa kudhibiti namna wamilikaji na wakaazi wanavyotumia ardhi.

Maswali kuhusu ubadilishanaji wa urithi wa haki za ardhi, yanapaswa kushughulikiwa na Katiba kupitia kamati za wananchi wenyewe. Kusiwe na kiwango kikubwa cha ardhi kumilikiwa na mtu binafsi. Kwa mfano, kuwa na ranch. Kwa hivyo tukapendekeza kuwa ranchs zisimamiwe na wananchi wenyewe. Iwapo hazitumiki zivunjwe na wananchi wa mahali pale, wapate kurithi. Haiwezekani kwa raia wa nje kumiliki ardhi kwetu, labda akodishwe kwa muda maalum. Wanaume na wanawake wanahaki sawa za kurithi kulingana na mila zao. Kumalizia nitaongea kuna moja hapa inayosalia nitakuwa ninamalizia.

**Com. Kavetsa:** Umesema kiwango gani cha ardhi? Umesema ranch ni kubwa, kuna kiwango ambacho unafikiria kinafaa kiwe kwa kila mtu, au?

**Jane Suma:** Sasa hapo, isipokuwa ..... (inaudible) unataka usaidizi, watu walisema ni vigumu kuwa unaweza kumwachia mtu kiwango maalum. Mwanamke aliyeolewa anahaki ya kurithi mali ya bwana yake, hata baada ya ndoa kuvunjika. Mwanamke



anahaki ya kurithi hata kama alizaliwa nje ya ndoa. Wananchi wa Kenya wanahaki ya kuishi popote nchini, iwapo kuna makubaliano baina ya wakaaji wa mahali pale. Katiba ihakikishe kwamba mwananchi anahaki ya kumiliki ardhi na rasilmali yake. Kwa mfano, mtu anaweza kuwa anamiliki ardhi ambayo chini yake kuna mali ambazo ni muhimu, kama maji, madini. Sasa kwa wakati huu, katika majadiliano yale huwa unaweza kupewa notice ya kuwa unaondolewa pale mahali, unapelekwa mahali pengine ili pale watu waweze kutoa kile kiko ndani. Kwa hivyo tukakubaliana ya kwamba, ikiwa kuna mtu anataka ile mali iko chini ya ardhi yako, akubaliane na wewe na kama ni kununua kwa kiwango chochote. Kwa hivyo, mwananchi awe na haki ya kuuza chochote ndani bila kuingiliwa. Na kwa hayo nimemaliza.

**Com. Kavetsa:** Kwa upande wa kurithi unasema mwanamke anafaaa arithi mali ya bwana yake hata kabla ya kuwachana. Hiyo ina maana gani?

**Jane Suma:** Hata kama ndoa imevunjika.

**Com. Kavetsa:** Hata kama ndoa imevunjika. Okay, nilifikiri kwa waislamu hiyo iko.

**Interjections:** (Inaudible) – from audience.

**Com. Kavetsa:** Na kurithi kwa mtoto wa kike?

**Interjections:** Sawa.

**Jane Suma:** Kwa sababu nimesema kuwa wananchi wana uhuru wa kurithi kulingana na mila zao, na wengine huwa wanatimiza na wengine hawakubaliani nao. Hata tafadhali ... (inaudible) tujaribu kuwaleta wawe .... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Okay, umesema vizuri, umefafanua vizuri kulingana na mila zao.

**Com. Salim:** Asante bibi Jane Suma. Una Memorandum au utawapa hiyo? Japheth Mukomba.

**Japheth Mukomba:** Mimi kwa jina naitwa Japheth Rwande Mukomba mkaazi wa Zombo location katika Msambweni division. Hapa tuna marekebisho ya Katiba ya Kenya ambayo maoni tunayotaka kuyatoa hapa, ni kuhusu tiba za kiasili. Hili ni jambo ambalo halijazungumzwa na wala halijaandikwa katika Katiba yetu ambayo tunataka kurekebisha. Kwa hivyo ni maoni natoa mapendekezo yetu. Katiba Pwani hatujakuwa na clinic yeyote ambayo ndiyo inasimamia tiba za kiasili. Kwa hivyo wakati huu tunataka katika Pwani tuwe na clinic yetu ambayo tulipendekeza iwe inatiwa “Amani Herbal Clinic”. Na katika hiyo clinic wakati huu, imesagiliwa kupitia wizara ya National Heritage & Sports katika Ministry of Home Affairs, kitivo cha social services. Na hivi, tumependekeza kwamba, misaada yoyote kupitia kwa serikali na wadhamini, kulingana na wenzetu ambao

wanaopata misaada kama hiyo, wa tiba hasili kutoka bara na sisi Pwani tuwe tunaweza kupata misaada kama hiyo. Pia, tuwe na uwezo sawa wa kufanya tiba kupitia au kulingana na madaktari wa tiba za kisasa kusaidiana kwa marathi ambayo yanatatiza sana binadamu.

Pia, tuwe tunaweza kupata misaada ya mawasiliano na pia, wataalam ambao tunaweza kufanya kazi pamoja kwa kupima marathi na kuhakikisha kwamba tiba zinaendelea sawa. Hapo pia tumesimamia kwamba tunaweza kuwa na uajiri wa watu ambao wanaweza kuendesha hii clinic hii yetu, kwa midhamini ya tiba za kiasili. Ngoma zetu ambazo tunatumia ziwe zinaweza kudumishwa na Katiba, ili tuweze kufanya maendeleo tukitumia ngoma haizo za kiasili. Tiba zetu ziko aina tofauti ambazo tunatumia kwa kupima. Tiba ya kwanza, sisi wenyewe katika Pwani, huwa tunatumia vitabu vyetu ambavyo vina tiba zake za kipekee, kwa wagonjwa ambao wako na aina ya maradhi kama hayo. Kwa hivyo, tumependekeza kwamba tiba kama hiyo iendelee katika jimbo letu la Pwani. Kuna tiba lingine linatumia ngoma za kienyeji. Katika maradhi fulani yanahakikisha kwamba tiba kama hizo, lazima ziendelee kwa sababu ya maradhi kama hayo kwa kutumia vifaa kama hivyo. Kwa hivyo tumependekeza sisi wanatiba hasili tuweze kutumia vifaa kama hivyo. Kuna pia vifaa vingine ambazo tunaita “tungure”, tungure ni kama zile preservation bottles, ambazo zinatumika katika hospitali kuu, au hospitali yeyote. Vitu kama hivyo vinatumika kwa sababu ya aina ya maradhi yanayopitia vifaa kama hivyo vya tiba.

Pia, tunaomba kwa mapendekezo haya ya Katiba hii, kwamba, wananchi wote wa Pwani wahakikishiwe kwamba wana uhuru wa kufanya tiba kama hizo kupitia chama chetu cha Amani Herbal Clinic, kila mmoja wenu akiwa na cheti ama kitambulisho kama hicho asiwe anatizika, afanye kazi na uhuru wote. Isipokuwa yule anafanya kazi bila kujisajili wala kujitambulisha yeye ni daktari. Kwa sababu tumepata njia nyingi za kutatizwa na wenzetu ambao wanafanya tiba za kiasili kutofafanua vibaya kwa tiba zetu. Kwa hivyo huo ndio mswaada ambao tunao kwa wakati huu, katika tiba zetu za kiasili.

Jambo lingine, ni kuhusu urithi wa ardhi, tunatatizika sisi wananchi kwa sababu ya wakati wa sasa katika urithi wa ardhi. Tumependekeza kwamba mwananchi yeyote ambaye anakaa sehemu ambayo ni ya jadi yake, asiwe “kwack” kwa sababu pale ni kwao. Kuwe mtu asiruhusiwe mtu yeyote kutoka nje, kuja kuwa na urithi katika sehemu ambayo si yake. Mwananchi wa sehemu hiyo awe yeye anahaki ya kurithi sehemu kama hiyo. Na pia, tumependekeza kwamba Kenya isiwe na squatter hata mmoja, kila mmoja awe na haki ya ardhi ya kukaa mahali anapotaka, kulingana na Katiba ambayo tunaitengeneza sasa. Pasiwe na vipengele vya kutatiza, isipo waelewane ikiwa ni mtu wa kutoka nje, isipo waelewane na wale wanaohusika, kama vile mwenzangu wa kwanza alisema kwa kukodi ama kuelewana na watu ambao wanahusika na area hiyo.

**Com. Salim:** Time ndugu, tafadhali.

**Japheth Mukomba:** Tafadhali jambo moja. Ninazungumzia habari ya miradi ambayo imekufa. Tunataka Katiba hii ihakikishe kwamba miradi yote katika Pwani iliyokufa ifufuliwe kwa mijadala ya wananchi, maana tunatatizika sukari hatuna, hatuna korosho, hatuna mafuta ya nazi na kadhalika. Kwa hivyo Katiba ya sasa kupitia marekebisho tunataka hivyo vyote

vifanye kazi, ili wananchi wapate kufaidika. Kwa hayo ni asante sana.

**Com. Kavetsa:** Umesema sukari na?

**Japheth Mukomba:** Sukari, korosho na mafuta, pamba, kila kitu kuna hata pombe ya kikwetu ambayo ilikuwepo. Sasa vitu kama hizi zimekufa.

**Com. Ratanya:** Unapendekeza pombe ya mnazi ihalalishwe?

**Japheth Mukomba:** Ndio kama inaweza kuwa, kama wakati wa nyuma ilikuwa ikiwekwa madafu na maji ya nazi ambayo ilihalalishwa sasa inatengenezwa na vifaa vyaa kuchanganya.

**Com. Kavetsa:** Usiende ngoja kidogo. Hiyo ilikuwa moja ya kufafanua. Jambo lingine, umesema la kuvuta moyo, ni tusiwe na squatter Kenya. Okay, unajua hata sisi kwa maoni mengine kuna suluhisho. Watu wengi wametoa suluhisho lako ni nini watu wa hapa, kwa sababu kuna watu ambao ni squatters, watapata ardhi lini?

**Japheth Mukomba:** Katika wale ambao wana ardhi, wanamiliki ardhi kinyume cha wananchi wa sehemu ile, hiyo sio yao, wamewanyasya na kuwanyang'anya na kuwafanya wale wenye sehemu hiyo kuwa ma squatter. Hiyo si haki, kwa hivyo ardhi irudishwe kwa wenye nchi ambao ni wakaazi wa jadi hapa.

**Com. Kavetsa:** Ukisema mwenyeji au foreigner unamaanisha nini?

**Japheth Mukomba:** Foreigner ni kama mzungu au mtu mweupe yeyote ambaye sio mwanakenya, huyo ndiye mtu wa nje. Huyo aje akodi sio achukue Beach nzima iwe ni yake na mwananchi awe squatter, hapana iwe akodi na alipe ushuru kupitia kwa council ya area hii.

**Com. Kavetsa:** You know the wearer of the shoe is the one who feels the pain.

**Japheth Mukomba:** That's right.

**Com. Kavetsa:** Yes, sasa mimi vile natoka magharibi mambo ya huku nataka nisikie kutoka kwako, nisiende nikasema pengine alitaka kusema na pengine huenda hajasema, hapana. Iwe kutoka kwa watu wa hapa. Watu ndio wanaji ..... (inaudible).

**Japheth Mukomba:** Wanajisikia vile viatu vinawafinya.

**Com. Kavetsa:** Ndio hivo tunataka ukisema jambo uliseme kabisa. Kwa sababu hakuna mwingine atalisema.

**Japheth Mukomba:** Ni kweli.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo munasema ni mzungu peke yake, na akitoka Tanzania?

**Japheth Mukomba:** Akitoka nchi za nje kama Tanzania, yeye anahaki ya kukodi. Mwanakenya yeyote ambaye anakaa Kenya na ni mwananchi, anahaki ya kukaa pahali popote katika Kenya, kulingana na kwamba wameelewana na wenye kukaa pale ambao ni wakaazi wa jadi.

**Com. Salim:** Asante sana bwana Japheth kwa maoni yako. Sasa namuita bwana Hamisi Mkungu.

**Hamisi Mkungu:** Kwa jina ni Hamisi Mkungu. Mapendekezo ya mwanzo ni kuhusu ufisadi. Kenya imekuwa na ufisadi wa hali ya juu, ukianzia kila upande, kwa hivyo napendekeza njia moja ya kuondoa ufisadi ni kuweko kikatiba au Anti-corruption commission. Na tunapendekeza yeyote yule ambaye amekuwa katika ofisi, public office na akafanya ufisadi wa aina yeyote, mali ile ichukuliwe irudishwe kwa sababu ni mali ya nchi.

Pili, kuna watu wengi ambao wanapora hapa nchini na wanaweka pesa nchi za nje. Kwa hivyo tunasema pesa zile ambazo niza Kenya zirudishwe Kenya.

**Com. Kavetsa:** Foreign banks or foreign accounts.

**Hamisi Mkungu:** Yes, Yes. Kitu kingine, ili kupunguza ufisadi katika ofisi za serikali na mashirika ya kiserikali, tunapendekeza kwamba yeyote yule anayefanya kazi katika sehemu ambayo niya public asiruhusiwe kufanya biashara ya aina yeyote, but apewe mshahara mzuri, aangaliwe kikamilifu ili asiwe katika hali ya kufanya ukora. Tunasema kwamba, hongo ni njia moja ya ufisadi, kwa hivyo yeyote yule ambaye atachukua hongo, kwa sababu hata mapolisi ndio zaidi kwa miswala ya hongo tunapendekeza kwamba wananchi wawe wanapewa uwezo kikatiba sio kungoja mtu mwingine, mwananchi awe na uwezo wa kukamata huyo moja kwa moja na atachukuliwa hatua.

Ardhi: Swala la ardhi limekuwa swala nyeti katika mkoa wetu wa Pwani. Watu kutoka nje na wengine wanasema watu wa nje ni wazungu, watu kutoka nje, Mwenyezi Mungu amemleta mwanadamu kila mtu akapewa sehemu yake, Central – wakikuyu, North Eastern ni wasomali, Eastern huwa kama ni wameru, Coast ni wamijikenda, wataita, wabajunyi, wapokomo inajulikana hiyo kabisa kabisa. Kwa hivyo yeyote yule ambaye amenyakua ardhi kiholela, hakununua kwa mwenye nchi wa pale, hiyo ardhi irudishwe haraka sana kwa mbunge anayejulikana.

Mali ya asili: Mali ya asili ni chombo ambacho kinapatikana ili kuleta maendeleo. Tofauti tunayoipata nchini hapa, ni kwamba ardhi ikigundulika, kitu ambacho ni cha dhamani, kuna jambo ambalo nila kikoloni, wanasema kitu hicho kinarudi kwa serikali. Serikali ni nyingi sana ulimwenguni na jambo hilo hakuna. Kwa hivyo tunasema mali itayopatikana katika ardhi ya mwananchi ni mali yake na serikali ipewe kodi kama kawaida.

Ajira: Kumekuwa na unyanyasaji kabisa katika sehemu hii, tunapendekeza kwamba kukipatikana nafasi ya kazi, asili mia sabini ya watakaoajiriwa wawe ni wananchi wa eneo lile.

Mayor na chairman wa serikali za mitaa: Tunapendekeza kwamba kwa sababu hao wanahusiana na wananchi sharti wachaguliwe moja kwa moja na wananchi.

Provincial Administration: Kulingana na unyanyasaji ambao umetokana na swala hili, limeendeshwa kikoloni, tunapendekeza kwamba provincial administration hiyo system au hiyo structure iwe scrapped na badala ya watu wale wawe wanachaguliwa moja kwa moja na wananchi, kutoka kwa huko mpaka PC huko, ndio hiyo nafasi ipatikane. Kwa sababu kwa sasa kuna maonevu.

Tunaenda kwa upande wa ukulima na uvuvi: Swala la ukulima nafikiri ndicho chombo ambacho kinatufanya tupate chakula ima kwa wananchi au kwa kuuza soko la nje. Tatizo ni kwamba serikali imeshindwa kabisa kushughulikia ukulima huku kwetu. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba wakulima wapewe ma-tractor, ili wawe na uwezo wa kulipia kidogo kidogo. Wapatiwe mbolea na kuwe na research, ili tukuze mazao na kuondoa umasikini.

Uvuvi: Hili ni swala ambalo serikali sasa haijashughulikia watu wa Pwani. Tunasika tu kwamba Lake Victoria wameenda watu wanaondoa magugu, mabilioni na mabilioni huku, hatujashughulikiwa. Kidao kile cha zamani, ndiho hicho hicho. Tunapendekeza kwamba wavuvi washughulikiwe kikamilifu na wapatiwe mikopo na wapatiwe nyenzo zinazostahiki kwa uvuvi wa kisasa, ili waweze kuenda kule bahari kuu.

**Com. Salim:** Tayari hapo. Endelea.

**Hamisi Mkungu:** Simalizi leo. Eh.. Niendeleo. Swala ambalo linaumiza zaidi nikuhusu vyama vya kisiasa. Vyama vya kisiasa kwa sasa hakuna uwezo kwa vyama vingine wakati bunge likifungwa, vyama vingine huwa havipati maswala fulani, kuna maonevu fulani. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba, bunge linalovunjwa President ma-Ministers, Assistant Ministers nao wawe wame-resign, badala yake kuwe na Tume maalum, ambayo itakuwa kama caretaker, ichukue nyadhifa ya kuongoza serikali kwa wakati ule mpaka tutakapomaliza kura. Kwa sababu ile cabinet huwa inatumia vifaa na inatumia maswala yote! Kwa hivyo tunapendekeza hivyo kwamba bunge likivunjwa iwe nayo ikiwa ni Rais, Ministers wawe wawe wame-resign.

Kitu kingine tunapendekeza kwamba kuwe na ofisi ya mtu ambaye atatetea wananchi, kwa sababu serikali mara nyingine huonea wananchi. Kwa hivyo wananchi wanashindwa waende wapi, kwa hivyo tunapendekeza ofisi ya ombudsman iwekwe hapo. Pia, tunapendekeza kwamba kwa sababu nguvu zile za Rais zinakuwa nyingi, Katiba hii ya sasa tunapendekeza kwamba nguvu zipunguzwe na arms zile zingine ziwe huru kufanya kazi zake kisawa sawa bila kuingiliwa. Na ili kupunguza zaidi zile nguvu za Rais, tunapendekeza kuwe na serikali ya majimbo na kuwe na Prime Minister naye awe ni yule ambaye chama chake kimeshinda na Rais, awe atachaguliwa na wananchi wote na asiwe na constituency. Rais awe ceremonial.

**Com. Salim:** Unawakati kidogo. Wenzako walia.

**Hamisi Mkungu:** Hawana neno. Elimu, hapa kusema kweli ni swala ambalo tunaumia. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba, elimu iwe ni bure katika kiwango cha nursery mpaka form four na ionyeshe hali ya bure katika higher education. Tukisema ionyeshe hali ya bure tunasema kwamba, iwe imewekwa kiasi ambacho wananchi wataweza. Na zipelekwe katika kila maeneo, isiwe kama sasa Universities zote ziko huko, huku hakuna.

Vyuo vya elimu upungufu, kila kitu upungufu, tunataka nchi ambayo kila sehemu watu wanakula cake. Twaelewana, national cake.

**Com. Kavetsa:** Twaelewana, endelea.

**Hamisi Mkungu:** Okay. Tunasema kwamba tukizungumzia swala la ardhi ambalo ni swala nyeti, ardhi. Ardhi ni swala nyeti hapa kwetu kwa sababu zimechukuliwa na watu kutoka nje, lakini mwenzangu amesema watu kutoka nje ni hao wazungu. Mimi sisemi kwamba ni wazungu, narudia maneno yangu nikisema kwamba yeyote ambaye si mzaliwa aslia wa pale pahali, huyo ndiyo mtu kutoka nje. Na iwapo ardhi inatakikana itolewe iwe wapewe wale wanaostahili, wazaliwa wa pale, yule mtu mwingine awe kuja kwake atasikizana na wale. Sio kama hivi sasa, DC akija shamba zote nizake, PC akija shamba zote nizake, polisi akija shamba zote nizake, ofisa ameletwa wa land amekusanya zote, hatutaki namna hiyo. Zote zile ambazo zimekusanywa, tunasema zirudi na zipelekwe kwa wananchi.

Mwisho, nitasema kwamba Civic Education ni chombo imara kwa kuwazindua wananchi. Ukawa na shida ambayo imetusukuma kwa sasa, Constitution, Katiba. Imekuwa ya watu wachache kwa mifuko yao na wananchi wote hawajui Katiba ya nchi ya Kenya. Kwa hivyo tunapendekeza swala hilo la elimu ya Katiba liwe linafunzwa mashule kote. Na Katiba ya Kenya itafsiriwe kwa lugha ambayo wananchi wataipata.

**Com. Kavetsa:** Sema lugha gani?

**Hamisi Mkungu:** Kiswahili. Si, mlisema ndio lugha ya taifa.

**Com. Kavetsa:** Wewe ndio unajua lazima useme.

**Hamisi Mkungu:** Okay. Kiswahili.

**Com. Salim:** Kingereza?

**Hamisi Mkungu:** Watu wote hawajui Kingereza.

*Interjections: Anasema hawezi kuongea.*

**Hamisi Mkungu:** Kiswahili peke yake. Ikiwa ni Kingereza mtaweka balance kwa wale watu wa nje, wajue mambo yetu. Sawa sawa hiyo. Okay. Tunasema kwamba mali ya taifa igawe katika kila sehemu bila ubaguzi. Mali ya kitaifa.

**Com. Kavetsa:** Endelea.

**Hamisi Mkungu:** Okay, haya haya. Sasa kuna swala la viwanda. Viwanda vyetu vyote vimefunguliwa mbali. Viwanda vyetu, ambavyo tulikuwa tukijivunia katika swala la kuondoa umasikini na vinaleta ajira, zimefungwa kwa maksudi. Watu wakisema kwamba wengine mchanga sio mzuri, tunasema kwamba hizo ni propaganda. Kwa hivyo ili kuwe na umoja wa ukweli, mazao ambayo yanapatikana katika sehemu vipelekwe viwanda. Ikiwa kuna rasilimali katika sehemu, kupelekwe viwanda kulingana na rasilimali zile, bila ubaguzi.

Soko: Ni sharti serikali ihakikishe kwamba imeweka soko kwa mazao ambayo yanakuzwa na kupeleka kutambaza maswala ya barabara kwa sababu ukosefu wa barabara unafanya mali nyingi zinaoza njiani. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba swala likiwa ni barabara, maji, umeme, simu hayo ni maswala muhimu na yanastahili kusambaa vijijini. Sawa hiyo. Halafu swala ambalo linaumiza kabisa ni swala la afya. Tunapendekeza kwamba afya, iwe swala la mahospitali yawe ya bure, bila kujalisha ni ugonjwa wa aina gani.

**Com. Kavetsa:** Okay, ningependa kukuuliza lazima useme vitu kinaganaga, kwa sababu caretaker – government umesema. Caretaker government, nani atakuwa kwa hiyo caretaker government.

**Hamisi Mkungu:** Okay. Hapo tunapendekeza kwamba AG awe pale. Nasema Chief Justice awe pale, Controller & Auditor-General awe pale, halafu na Permanent Secretary wakiongozwa na AG. Swali lingine?

**Com. Kavetsa:** Unajua Constitution ni watawala na wale wanatawaliwa na pia kuna jambo ulilete la hongo, ukasema polisi

ndio wanahusika zaidi, polisi wanahonga polisi?

**Interjections:** Polisi hawahongi polisi, polisi wanahongwa.

**Com. Kavetsa:** Wanahongwa na?

**Hamisi Mkungu:** Okay, hata kama unajua lakini nitakuambia. Mimi nahonga polisi, hapo hizi gari ambazo zinapita, gari ambazo zinapita zimeweka mfumo maalum, haziangalii kwamba usalama wa magurudumu wala nini. Nikubwaga kitu na kuenda, hiyo ni hongo hiyo.

**Com. Kavetsa:** Watu wanahonga polisi kwa sababu ..... (inaudible) – sasa upande wa wananchi tufanye nini kwa sababu mkimpa hongo unasema yeye ashtakiwe na nyinyi?

**Hamisi Mkungu:** Pia wewe umekosea lakini tumesema nguvu wapewe wananchi ili washike mara moja hawa.

**Com. Ratanya:** Bwana Hamisi kuna swali lingine moja, na hili nikuhusu provincial administration. Ulisema kwamba hawa wote wa provincial administration wachaguliwe na mtu. Unamaanisha kutoka, unajua provincial administration iko juu kutoka PC mpaka assistant chief.

**Hamisi Mkungu:** Nimesema kutoka kwa PC mpaka kwa sub-chief.

**Com. Ratanya:** Wote wafanywe kura na wananchi. That is good clarification.

**Com. Salim:** Asante bwana Hamisi kwa maoni yako, ikiwa una Memorandum waeza kutuwekea pale. Sasa namuita bwana Abdul S. Kaole.

**Interjections:** Jina lako ni Kaole?

**Abdul Kaole:** Kwa majina naitwa Abdul Kaole, mimi ni mkaazi wa hapa hapa Msambweni, nataka kuongezea uzito juu ya Memorandum iliyotolewa na ujenzi, kwa hivyo nitaongezea, juu ya President. Kama vile mnenaji wa kwanza, pia mimi ningependa kusema kwamba President katika Katiba yetu ya Kenya ana uwezo mkubwa sana, hata saa ingine anaweza kutoa ahadi za mambo ambayo hayatimizi. Kwa hivyo, kwa sababu mbili zishatolewa kama vile Prime Minister, kupunguziwa miaka, hayo pia mimi nachangia kwamba asiwe akipigiwa tena kura mara ya pili kurudi, mbali akishika miaka mitano itoshe, apunguziwe awe anaweza kushtakiwa. Awe ikiwa kuna “vote of no confidence” kama vile American inavyofanya, mambo kama hayo President wetu awe mtu wa namna hiyo. Kuna mambo matatu ambayo katika mwananchi wa kawaida niya muhimu



sana.

Kama vile ambavyo employment inapungua sana Kenya, elimu, maji na hospitali au hudumu za afya, ni mambo ambayo ni muhimu sana kwa mwananchi wa kawaida. Hayo yashasemwa na mimi pia naongezea uzito kwamba mwananchi wa kawaida baada ya miaka mitano au kumi labda atakufa kijijini tu ikiwa hakutakuwa na huduma za bure au za chini kabisa. Kwa hivyo elimu yetu inasemekana ni ya bure, lakini iko ghali mpaka hata watu hawajui la kufanya.

Upande wa maji, pia maji labda serikali ingefanya mipango kama kuchimba dams, visima, unaweza kuona mji kama wa Mombasa ni kwamba maji yanauzwe mpaka sasa na mikokoteni, hakuna maji unakwenda kama Tudor ukakaa siku tatu huogi.

Na maji ya mvua yanamwagika mengi sana katika mkoa wa Pwani. Na sasa nasema kwamba water ikibidika badala ya hizi boreholes chache, tukafanya bidii maji mengi yanayomwagika kukawa na water catchments na watu wakawa na maji ya kutosha, kwa hivyo mambo matatu ya elimu, maji na hospitali ama afya katika Katiba inayotengenezwa tuzipate vitu hivyo bure.

Imeshatajwa tena juu ya mazao ya Pwani. Tunashangaa tulipokuwa tu watoto tuliona mazao ya Pwani mengi yana soko na yana viwanda na kukawa kuna ajiri za kutosha, lakini hivi sasa korosho, watu wameacha kupanda kwa sababu hakuna pa kuzipeleka, miwa hali kadhalika, machungwa ndio mengi, soko hakuna, machungwa yanaweza kuwachwa tu hapo yakaoza halafu mpaka watu wanauza tu moja sumni. Kwa hivyo tunashangaa, twatafuta mikopo ya kutoka nje, wakati watu hawa wa nje tungewauzia machungwa tukapata pesa, tungewauzia miwa tungepata pesa, tungewauzia korosho. Kwa hivyo kama huku Kwale District nataka nisema kwamba mazao yetu yote ni kama yamepuuzwa, na hakuna kitu cha kufanya. Minazi yetu twasikia sasa yapelekwa Tanzania, ambapo Kenya ingetumia nazi hizo, pengine tungepata pesa badala ya kutafuta pesa kutoka nchi zaidi. Kwa hivyo tuna mazao mengi ambayo hayatumwiwi katika District ya Kwale na hata mkoa wetu wote.

Upande wa parastatals: Nashangaa hizi parastatals hapa Pwani ziko nyingi. Kwanza Bandari, tuna KWS lakini sisi watu wa Pwani hatufaidiki sana. Lakini wacha niseme hivi, labda kungekuwa na District ama zingekuwa privatized angalau wananchi waweze kufaidika. Kwa mfano, KWS ina wanyama wengi ambao hao wanyama badala ya kutufaidi sisi wanatuharibia mimea, kama ndovu. Na sheria haituruhusu kuwaua ndovu, kwa hivyo sasa hata unapoharibiwa minazi yako, kule kupata afidia pia ni shida. Naomba kungekuwa na machinery fulani ambayo mwananchi wa kawaida kama hiyo District Committee inamuunganisha mwananchi wa kawaida na KWS ama na serikali, aweze kupeleka kilio chake kwamba ameharibikiwa. Twajua kwamba tuna nyani wengi, ni sehemu ya KWS, sasa hawa wote ndio sehemu ya utalii. Lakini sasa serikali ingefanya jambo badala ya hawa wanyama kulete umaskini, watu wamewacha mashamba kwa sababu ya wanyama hawa na ukulima. Sasa serikali ingeangalia wanyama hawa ambao ni mali ya serikali, watafanywa nini ili mwananchi wa kawaida aendelee na ukulima wake? Mimi mengi yamesemwa, kwa hivyo katika marketing tulikuwa tunasema cashewnuts, sugarcane, coconuts haya yote ni mimea ambayo Pwani haina soko la kutosha na ingeleta utajiri na ajira nzuri. Hayo ndio yangu.

**Com. Kavetsa:** Swali ni hapa, upande wa Rais unasema miaka tano – one term. Okay hapo umesema akifanya kosa awe prosecutable au impeached? Unajua akifanya kosa linaweza kuwa kosa, apelekwe kwa korti, halafu awe fined. Lakini ingine

ni impeachment, yaani ile kuwa na power ya kumtoa. Kwa sababu ulisema, ni aina mbili, nataka useme ni aina gani ulimaanisha?

**Abdul Kaole:** Mahali kama America, President akifanya kosa na wananchi kama hawakupendelea jambo fulani, kuna machinery fulani inafanyika na watu wanatoa kura yao, sio? Kwamba je, angefaa kuendelea kwa Rais kutokana na hiyo kashfar ama kutokana na hali fulani na halafu hiyo kura ita .... (*Interjection*).

**Com. Kavetsa:** Hii umesema ya mwisho ni referendum. Okay. Inginge ilikuwa akifanya kosa, apelekwe kortini.

**Abdul Kaole:** Aweze kushtakika, aweze kushtakiwa. Yes.

**Com. Kavetsa:** Unasema upande wa Rais, na upande wa MP na Councillor kwa hayo maneno? Kwa sababu, kama hauna maoni ya hiyo ni sawa, lakini kawaida ikiwa principle ina apply kwa Rais, na kwa mbunge na kwa Councillor. Na ikiwa five years hiyo pia, but if you have not thought about it, it is okay someone else will bring it up. Sasa ulisema water catchment, tuwe na water catchment areas.

**Abdul Kaole:** ... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Hapa Pwani?

**Abdul Kaole:** Hapa Pwani boreholes ni nyingi sana .... (inaudible) na maji yanamwagika bure ambapo .....(inaudible) .....kama boreholes kumaliza hapo. Water ni muhimu sana. Mimi nasema katika Katiba hayo yazingatiwe.

**Com. Salim:** Asante bwana Abdul Kaole kwa maoni yako. Sasa namuita bwana Kassim Kibunda, councillor.

**Kassim Nyawa Kibunda, Councillor:** Mimi kwa jina naitwa Kassim Nyawa Kibunda, ndio jina la kisawa sawa, lakini wanafupisha tu wanaandika Kassim N. Kibunda. Leo, mimi natoa maoni yangu kwa Katiba, maoni yangu yatakuwa mafupi. Na sababu ya maoni yangu yawe mafupi, ndani nina masikitiko kwamba, Katiba vile ninavyofahamu, ni jambo muhimu sana. Lakini vile ambavyo Katiba inasukumwa na Bunge, mpaka wale ma-Commissioner hawawezi kufanya ile kazi sawa sawa, mimi ninaona hata wale ambao tunatoa maoni, naona ni maoni ya bure. Lakini si maoni ambapo itaweza kusaidia wakenya. Kwa mfano, Lunga Lunga ni sehemu kubwa ambapo ina wananchi wengi. Na ma Commissioners hawatafika sehemu hiyo, nitakuwa ni mimi tu peke yangu kutoa maoni yangu binafsi. Watu wa Lunga Lunga hawatapata kutoa maoni. Hivi sasa bwana Commissioner uko hapa wasema umekuja Msambweni, lakini hukuja Msambweni Division. Hapa hutachukua maoni ya division nzima, wachukua maoni ya watu wachache tu. Kwa hivyo, maoni yangu mimi, yale maoni yangu ambapo nitayatoa naona litakuwa neno moja, ningesema ikiwa Kenya imekubali kuundwe Katiba, Bunge lititenge kando, liache Commissioners

waendeshe kutafuta hii Katiba kwa njia ya utaratibu.

Lakini ikiwa mnasema mnaunda Katiba, Katiba mimi naifahamu katika mwili wangu peke yangu. Huu mwili wangu wenyewe una mambo mengi ambayo yanahitaji yaangaliwe na Katiba, macho yangu yanataka yaangaliwe na Katiba, miguu yangu yanataka yaangaliwe na Katiba, mikoni yangu yatakikana yaangaliwe na Katiba. Je, tukiwa hivi tunavyoenda kweli tutatengeneza kitu gani? Hii, mimi ninasema ikiwa Kenya ilikubali itengeneze Katiba, waache ile Commission ifanye kazi kwenda kijiji baada ya kijiji. Ikiwa limetengenezwa Katiba hii kwa sababu ya bunge, basi ifanywe hivi hivi lakini watakuwa hawakutengeneza Katiba. Na ningesema, najua hamtakubaliana na mimi, lakini mwishoni mtakuja kukubali kwamba hamkutengeneza Katiba ya Kenya. Mtakuwa mmetengenezea watu fulani, kwa sababu wanahamu ya viti, au wanahamu ya uongozi fulani. Lakini anaona hawezi kupata ule uongozi mpaka kuondolewe kitu fulani, ndipo yeye aende kuingia pale kwa ule uongozi. Ma-Commissioners ningependa langu la mwisho kabisa. Ningependa Commission hii iende kijijini pole baada ya pole, mpaka imalize Kenya. Ndipo watakuwa wameunda Katiba. Hata hizi Memorandum ambazo mnazipokea hapa, bwana Commissioner, nakuhakikishia si za ukweli. Na ninasema hivyo nikisema sawa sawa. Mimi nikiwa ninatoka Lunga Lungu, kuna kamati liko Lungu Lungu linajiita Co-operative Society ya Lungu Lungu, na haina hata siku iliyoita mkutano wa viongozi, leaders meeting peke yake. Haina hata siku moja ilifanya hivyo. Haina hata siku moja iliyoita ile Co-operative yenyewe. Baada ya ile Co-operative Society ina wale members, na wale members wenyewe pia hawakuitwa wakakaa, wale members wenyewe hawakukaa, je ikiwa hata members wa Co-operative hawakukaa, je wale wananchi wa kawaida ambao sio member wa Co-operative, wanachochote wamechukua? Hakuna. Sasa basi, mimi yangu ya mwisho nafikiria sitakuwa na mengi ya kuendelea, uamuzi wangu wa mwisho ninasema uchaguzi usisimamishie mambo mengine ya kiserikali, iendelee serikali na kazi zake. Kwa sababu uchaguzi ni miaka mitano, lakini ikiwa itaharakisha Katiba hii ndipo wao waendeleo na uchaguzi, mimi naona hapo wametoka nje. Na serikali kuwa moja, mimi naunga mkono serikali yetu iwe moja, kwa sababu bado ni changa, na bado wenyewe hatujakaa na viwanda tofauti, tofauti au vyo viko tofauti, tofauti. Hatuna, bado tuko mbali sana.

**Com. Salim:** Maoni yake hayo. Ana haki ya kutoa maoni yake, kila mmoja wenu anahaki ya kutoa maoni yake. Tafadhali tumpe nafasi yake.

**Kassim Nyawa:** Swali?

**Com. Kavetsa:** Haya, sasa ningependa kukuuliza hivi, ningependa kukwambia kwanza sisi kweli ni Commission ya bunge, na wameandika sheria tunayofuata, okay? Hata wananchi walituambia mfike mpaka vijijini ndio tutoe maoni, lakini nashangaa kidogo kwa sababu wewe ni councillor, unaakilisha mahali, sivyo? Sasa hao watu unaowakilisha unawazungumzia?

**Kassim Nyawa Kibunda, Councillor:** Ndio tunawazungumzia.

**Com. Kavetsa:** Wewe, wewe sio nyinyi. La pili, wale watu wa society kwa nini hawakuita mkutano?

**Kassim Nyawa Kibunda, Councillor:** Mimi nilipowaona niliwaauliza kwamba nilisikia kuwa kuna Co-operative Society ambapo imechaguliwa kufanya kazi katika Lunga Lunga location, nilienda kwa chief nilipo ambiwa na co-ordinator, bwana Mkalla. Aliponiambia nilienda kuwauliza ni kitu gani kilichomfanya nyinyi mpewe uwezo, na kwa jina la co-operative. Kwa nini kinachomfanya bwana msiite kile kikundi chenu chenye mkaaka nacho chini na halafu mkaaita viongozi, mkaaka nao chini mkaweza kufanya kazi peke yenu. Sasa mnaniambia mkienda mnapata watu wawili, watu watatu. Sasa wale watu mlikuwa mtawapata namna gani? Lakini ni dakika za mwisho tumechelewa ambapo hata hakuna njia nyingine, ya wao kuweza kuita wale wakulima, au kuita wale viongozi wale ambao ni leaders wa ile sehemu. Tulipata hiyo information kama imechelewa kutoka kwa co-ordinator.

**Com. Kavetsa:** Kwa sababu, inafaa uwe umekuja na waakilishi wao kutoka kwa sehemu yako sio kuja peke yako. Na ya mwisho, unaelewa unitary government nguvu zake zote ziko Nairobi. Nusu ya mali yote iko Nairobi, hii si kitu mimi nasema, lakini kueleza tu. Sasa ukilalamika hakuna kama University huku, hivyo ndivyo unaunga unitary government, kwa sababu nguvu zake zote zinaenda kwa capital, sio Nairobi pekee. Nchi yeyote ambaye ina unitary government, nguvu zinaenda kwa capital, hiyo capital city. Sasa ni kama kuna witness mahali fulani, lakini itaendelea ikiwa hiyo unitary government itakuweko. Sasa mpakani huku Msambweni, na mpakani kule Teso, na mpakani kule Somalia hao hawatakuwa navyo, kwa sababu vitu vyote vinaenda kwa capital city.

**Kassim Nyawa Kibunda, Councillor:** Capital yetu ya Coast Province inatosha kuweza kuwa sisi katika hii Coast Province ingekuwa ina chuo moja au mbili. Hii capital yetu yatosha kabisa.

**Com. Kavetsa:** Councillor, councillor. Hiyo umesema hapo mwisho, tafadhali. Hiyo ume-describe sio unitary government, kwa sababu pesa za hapa Coast umesema zinafaa zi-develop Coast, hiyo sio unitary. Sasa inafaa wewe mwenyewe ufikirie unitary ni nini, na serikali ingine ni nini? Kwa sababu ukianza mambo, pesa zetu za Coast, kodi yetu ya Coast inafaa iwe University mbili, hiyo sio unitary. Unitary, vitu vyote vinaenda Nairobi. Nafikiri nimeandika maoni yako, Unitary.

**Com. Ratanya:** Bwana councillor umetueleza maoni yako na ningetaka kufuatia hapo hapo kwa hii unasema serikali moja. Umesema kuwa unapendekeza kuwe na serikali moja na unajua sasa tunakuja kuchukua maoni ya kila mahali, sasa tuko hapa Msambweni. Sasa hii serikali yako unasema moja, unaweza kufafanua difference ama tofauti ya hiyo yako moja na hii tuko nayo sasa?

**Kassim Nyawa Kibunda, Councillor:** Naweza kufafanua kidogo kwa sababu zangu. Sababu zangu za kusema kwamba sisi katika watu wa Coast Province, kuangalia, zile vifaa ambazo tungeweza kutegemea na zikatuendesha kwa njia ya kisawa sawa, naviona hakuna vifaa vyovyote ambavyo sisi watu wa Coast tunaweza tukafaulu, tukiwa tumechukua katika serikali ya majimbo yetu. Kwa sababu, kwa mfano.

*Interjections: (Noise from the crowd).*

**Com. Salim;** Hayo ni maoni yake.

**Kassim Nyawa Kibunda, Councillor:** Nimekuambia namba ya kwanza, nimekuambia katika Coast, hatuna University hata moja. Namba two, katika Coast mpaka hivi sasa hatujaendelea kibiashara, nikiangalia wafanyi biashara ni watu fulani ambapo ijapokuwa naweza kutaja nitaonekana niko na ukabila fulani. Lakini ni watu fulani wachache, watu wa nje, ndio ambao ni wafanyi biashara na ndio watu wale ambao wana mali. Sisi asili ya Coast wengi bado ni maskini. Na ninaonelea kwamba tutakuwa watumwa wa wale matajiri, kwa sababu sisi tukiwa hatuna chochote na hatuna la kutegemea, si lazima twende tukapigie magoti kwao? Na kwa sababu hiyo ya kujua sisi tu mwishoni tutakuwa watumwa wa watu fulani.

Afadhali kwanza tushikilie serikali hii ya pamoja tuende mbio, tujaribu kusomesha watoto na kuenda mbio za kubadilisha ule mtindo ambao tumekuwa nao hiyo miaka arobaini ambayo imetajwa. Kwa sababu katika hiyo miaka arobaini inayotajwa bado hatujainua mguu kwenda mahala popote, kwa sababu ukiangalia Coast Province nzima, hakuna mkulima mashuhuri hata mmoja, hakuna mfanyi biashara wa kisawa sawa hata mmoja. Sasa bado tuko chini sana.

**Com. Salim:** Asante sana bwana councillor umeshatoa maoni yako, umechukua wakati wa kutosha kutoa maoni yako na tumeyasajili na kuyanasa. Asante sana. Tukiendelea mbele basi yuko bwana Halid A. Maingo.

**Halid A. Maingo:** Mimi kwa jinani Halid Ali Maingo.

**Com. Kavetsa:** Ngoja kidogo, tutasimamisha kama hamtakuwa na kuvumiliana na heshima pia. Nitasimamisha, kwa sababu haya manung'uniko yanaingia kwenye rekodi zetu, watu watasikiza miaka hamsini ijao na watu watasikia tu ng'u, ng'u, ng'u. Tafadhali kila mtu ana maoni yake, ndio tunaenda round, lakini tungejua wakenya wana maoni moja, sisi tungeandika Katiba na kumaliza.

**Com. Salim:** Bwana Halid karibu.

**Halid A. Maingo:** Naam, Sheikh. Asante. Maoni yangu kulingana na Katiba ya Kenya, Katiba ya Kenya kama sisi majority sana sehemu yetu wengi sana ni waislamu, na Katiba ya muislamu iko katika Koran. Kwa hiyo sisi hasa lengo ama maoni yangu, ni kwamba sisi sheria zetu tuwe nazo sisi wenyewe. Nataka kama serikali itakayo kuja pengine, hasa serikali tunayoitaka ni ya majimbo, tujitawale sisi wenyewe maanake muda mrefu sana hatuna manufaa yoyote katika hii Kenya.

**Com. Salim:** Ukisema hatuna, hatuna watu wa Pwani ama hatuna waislamu au?

**Halid A. Maingo:** Tukiwa watu wa Pwani. Na tukiwa watu wa Pwani hatuna chochote tunachofaidika isipokuwa tunaona kama tuko hali ya utumwa. Na afadhali tuwe uhuru na utumwa, kuliko kuwa hivi tulivyo kama ng'ombe tunaofungwa, tunapewa nyasi tu basi lakini hatuna faida yote.

**Com. Salim:** Endelea.

*(Laughter)*

**Halid A. Maingo:** Kwa hviyo sisi hamu kubwa sana nikujitenga, tuwe peke yetu, tunataka serikali ya majimbo. Nadhani nikifika hapo nimekomaa, sitaki kuchukua muda mrefu zaidi.

**Com. Kavetsa:** Umetaja waislamu au umetaja watu wa Pwani. Halafu umetaja watu wa Pwani.

**Halid A. Maingo:** Nimetaja waislamu. Yote ni moja tu.

**Com. Kavetsa:** Hiyo Pwani inaenda mpaka Taita huko na wengi ..(inaudible).

**Halid A. Maingo:** Watu wote ikiwa tunamuita muislamu hata akiwa muislamu, mkikuyu ni muislamu, hata akiwa mbaluhya ni muislamu. Hiyo ni islam yote.

**Com. Kavetsa:** Nataka tu utofautishe mzee, kwa sababu umesema watu wa Pwani ni waislamu. Sasa tukiwa na sheria, sitaki kubadilisha maoni yako, lakini nataka unieleze tukiwa na sheria ya Kurani hapa Pwani, hao wataita na wataveta watakuwa aje?

**Halid A. Maingo:** Kurani niya waislamu wote katika ulimwengu.

**Com. Kavetsa:** Okay, okay.

**Com. Salim:** Asante sana bwana Halid Maingo. Umeshamaliza?

**Halid A. Maingo:** Nishamaliza.

**Com. Salim:** Shukrani. Sasa namuita bwana Hassan Bwata.

**Bwana Hassan Bwata:** Ka majina kamili naitwa Bwana Hassan Bwata na najitokeza hapa kuchangia juu ya marekebisho ya

Katiba. Kwanza kabisa ningetoea pendekezo langu kuwa, kuwe na sheria ya mwananchi kufunzwa Katiba kupitia shuleni, kwa sababu mpaka sasa wananchi wengi hawajafahamu Katiba hii ilivyo, watu wanachangia tu.

Ya pili; ni police force: Police amepewa nguvu kubwa sana katika Katiba ya sasa. Unakuta polisi saa hii akiingia hapa wananchi wote watakimbia, na weanweza kushika mtu wakaenda kumuwekea statement zingine na pia ataenda kortini. Kwa hivyo kuwe na sheria ya kupunguzwa nguvu za polisi kwa mwananchi.

Ya tatu ni elections: Uchaguzi unapofanywa mashinani, huko katika grassroots, kura zihesabiwe huko huko, ili wale ambao ni wawakilishi wa vyama tofauti tofauti wachukue hesabu zao huko huko, wakija huku wafahamu kuwa kura zimetokea ngapi.

Ya mwisho ni mara nyingi Tume za kuchuguzwa mambo yanayotokea, majanga hapa nchini, unakuta Rais ndiye ana uwezo wa kuchagua mtu asimamie jambo kama vile Kenya Ferry ilivyofanyika pale Mtongwe, na unakuta habari zinatokea ovyo. Uwezo huo usiwe wa Rais ni Bunge kwa sababu Bunge lina uwezo wa kuchagua yule mtu ambaye anaweza kutoa ripoti kamili na akaitoa kwa wananchi wakafahamu kisa hicho makosa yake yako wapi. Sina mengi ni hayo hayo.

**Com. Salim:** Asante sana Bwana Hassan Bwata kwa maoni yako. Hussein Rindano.

**Hussein Rindano:** Mimi rai yangu kama tulivyoambiwa tuchangie rai. Kutoka tuchukue Uhuru bila shaka tuna sehemu mbili, sehemu ya Pwani na tuna sehemu ya bara. Kweli sisi watu wa Pwani tumestaamili kuwa nyuma, tukawa na Rais wa kwanza bara na tukastaamili tukawa na Rais wa pili bara, maoni yangu napendelea hata kama si mwaka huu Raisi achaguliwe Pwani, bila kura, watu wapendekeze tu kwamba huku wamefaidika matunda ya uhuru na Pwani wafaidike na matunda ya uhuru.

**Com. Salim:** Sasa mwenzangu kabla hujaendelea mbele, unajua hapa ni kwa .... (inaudible). Kwa maana hii Katiba sio ya leo, sio ya kesho, sio ya mwaka ujao, mbali ni ya miaka na miaka ijayo, kwa hivyo tuandike vipi?

**Hussein Rindano:** Tupate Rais sehemu ya Pwani nayo, ili nayo ijikute kwamba kweli ina uhuru tangu tuchukue uhuru. Na vile vile ukitoka Pwani, ikiwa ni Ukambani uregeshwe urais nao kila mtu afaidike na urais.

**Com. Salim:** Ile inaitwa rotation.

**Com. Kavetsa:** La kwanza ulisema ni ... (inaudible) hii unasema ya pili hiyo ndiyo Katiba. Kwa sababu inataka kukiwa kama Pwani iwe na Rais miaka mia moja? Ya pili, ni kusema leo tubadilishane, hiyo ndio Katiba.

**Hussein Rindano:** Sawa nitahakikisha kuwa nasoma vile vitabu sana.

**Com. Ratanya:** Wewe hutaki uchaguzi?

**Hussein Rindano:** Nataka iwe democratic, wale wamepata na hawa wanaoipendekeza, isiwe kura atarudia yule yule tena. Nasi tunataka wao .... (inaudible).

**Com. Salim:** Na wataka Rais kutoka eneo lolote awe Rais kwa muda gani?

**Hussein Rindano:** Sisi tunataka tumpe miaka kumi afaidike kidogo. Akimaliza kumi, mwingine.

*Interjections: (Laughter) from the audience.*

**Com. Ratanya:** Unataka kwa tribal ama kwa province? Irudishwe kwa province, kama iko ukambani... (inaudible).

**Hussein Rindano:** Province.

**Com. Salim:** Endelea.

**Hussein Rindano:** Jambo la pili, ni mali ya asili kama bahari, imechangiwa sana lakini mimi nachangia nami kwamba bahari iwe iko mikononi mwa wananchi wa sehemu ile. Isiwe una part hapo kuambiwa bahari hii hakuna ruhusa kuingia mwananchi wa hapo ambapo huko ndipo anapoingia mwananchi kutafuta mbinu zake za ziriki. Tunataka bahari iwachwe huru kwa wananchi.

**Com. Salim:** Kwa uvuvi?

**Hussein Rindano:** Kwa uvuvi na shughuli zote za mali iliyo baharini kwa maana kuna madini, pia kuna lulu ziwe hizo niza wenyewe, ziwe zina wenyewe.

Sehemu ya pili napendekeza kwamba kama alivyosema msemaji wetu kwamba waislamu wote Kenya nzima wahukumiwe na kitabu cha Kurani kwamba hiyo ndiyo Katiba yao. Waislamu wote wa Kenya wahukumiwe na kitabu chao, Kurani, ikiwa ameiba atakatwa mkono, amezini apigwe mawe, amezini kiwango cha mwisho amepigwa na mawe afe, ama amezini tu hajaoa, apigwe bakora mia moja. Sisi tunataka sheria ya kiislamu tunapendekeza ipitishwe hivyo kwa maana ndiyo sheria yetu Kenya nzima ya kila muislamu.

Sehemu nyingine tunataka kwamba uajiri wa kazi, serikali ikitaka kuajiri kazi watu, ugawanya serikali sehemu mbali mbali za mikoa, sasa inapofika sehemu ya mkoa wetu tuwe ni sisi watu wa mkoa huu, tuajiriwe hapa kwanza. Halafu ndio wachukuliwe



wengine maana maonevu ambayo yanapita ni kwamba kazi hata ya kufagia inachukuliwa mtu kutoka juu kuletwa huku, ukiuliza unaambiwa hawa hawakusoma. Kwa hivyo tunataka Katiba hii kwamba, popote ilipo kazi sehemu ile inaajiri wakaazi iliyo kiwanda, wale wananchi wenyewe wa pale wafaidike. Ikiwa ni bara wafaidike, ikiwa ni Pwani wananchi wa Pwani wafaidike.

Sehemu nyingine ni upande wa kazi: kama tunavyojua kwamba waislamu wanazo sheria zao za urasi na hata mataifa mengine wanazo sheria zao za urasi. Lakini sisi tukifika kortini leo, tunachanganyiwa nyama, tunataka sheria zetu ziwe nje, tujue kwamba kama anavyotambua Mungu kwamba mtoto wa kiume anayo sehemu, na mtoto wa kike anayo sehemu katika ile mali iliyowachwa na wazazi wao. Isiwe kwamba mtoto wa kike hawezekani kurithi. Sheria yetu inasema mtoto wa kike arithi, lakini kurithi kwa mtoto wa kike si kama kwa mume. Mume anapata kamili na mke anapata nusu, kwa sababu yule mtoto wa kiume analo jukumu kubwa, yule dada yake akiwa kule amepata nusu na huyu amepata kamili, atakuwa na mke, watoto, family hata huyo dadake wakati anapokosana na mume, atarudi pale pale, ndio kwa sababu hapewi kamili. Nitamaliza na moja tu. Siendi mbali sana kwa sababu watu ni wengi.

Kitu kingine ni ardhi, ardhi ndiyo mali asili kabisa kabisa. Ikiwa leo hii huna ardhi utakuwa katika taabu kubwa sana. Mpaka imetokea kwamba leo utasiliwa na mtu wako imepatikana kwamba lazima ukazikwe kwa ardhi yako, lazima ukazikwe kwenye boma yako. Sasa ukiwa huna ardhi itakuwa ni tatizo kubwa, ardhi pia tunataka ziachiwe wananchi wenyewe, ardhi, wewe wanazo power. Wasiingililiwe kuhusu ardhi zao. Nafikiri hapo mimi nitakoma kupisha wenzangu kwa sababu wakati unaendelea na kuna maswali ya muhimu mengi yatakayoulizwa.

**Com. Kavetsa:** Ngoja kidogo. Upande wa elimu, watu wengine wanasema quota system, na wewe umesema tu kazi ipewe wale watu upande wa kuajiri. Unamaanisha nini?

**Hussein Rindano:** Ninamaanisha kwamba waajiri wate ambao wana ujuzi wa hiyo kazi, lakini wako katika sehemu hiyo. Sio kila mtu ambaye anao ujuzi wa kazi hiyo, lakini ukihakikisha hata kama atachukuliwa mwingine huku kutoka mbali aje, lakini tujue ile sehemu wamechangwiwa kidogo, na wenzetu nao wapate. Lakini wale wasiwe kidogo, wale wenye pale.

**Com. Kavetsa:** Hiyo kidogo ni watu wangapi?

**Hussein Rindano:** Kidogo ni watu wachache.

**Com. Kavetsa:** Unajua vile nakuuliza kwa sababu wengine wanasema, sikilizeni. Tume linataka maoni ya watu Kenya nzima, na kuna wengine wanasema watu waajiriwe Kenya bila ubaguzi, watu wanunue shamba Kenya bila ubaguzi, watu wanafanya hivi bila ubaguzi, na nyinyi vile naona, inafaa mleta ile na kusema ni kiwango fulani. Siwezi nikawaambia vile mtasema, lakini naona ukikosa kusema asili mia gani inafaa iajiriwe au asili mia gani ya shule, itakuwa haina nguvu sana ikifika kwa wale ambao wamesema kwa nguvu.

**Hussein Rindano:** Kwa mfano ikiwa wataajiriwa watu mia hapa, wale wenzetu wapatikane watu kama hamsini hivi, ni maoni tu.

*Interjections: Inaudible.*

**Com. Kavetsa:** Ni maoni yake. Asili mia gani? Haya.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo hapo unamaanisha kwamba kama kijana anaweza ku-qualify kuwa Chief Justice akae huko Nairobi kutoka Coast, unamaanisha kwamba asiajiriwe kazi huko Nairobi? Akae hapa kama Chief Justice wa Kenya.

**Hussein Rindano:** Aajiriwe kwao. Akiwa hapa na amekuja ama ni mwenyezi?

**Com. Ratanya:** Kama kuna nafasi ya P.S. kwa mfano ama Chief Justice.

**Com. Kavetsa:** Ama kiti anasimamia na ni mtu wa Pwani. Aondolewe huko aletwe hapa?

**Hussein Rindano:** Aletwe hapa badala ya kukaa nationally. Yaani, badala ya kuwa Nairobi kama ni national level.

*Interjections: Inaudible.*

**Com. Salim:** Hayo ni maoni yake, lakini bwana Hussein labda nikirudia swala la mwenzangu hapa, ungependa percentage gani, unajua percentage ni hesabu ya sawa. Maanake tuseme asili mia ngapi ya wafanyikazi kule Coast wawe ni wasio wa Pwani? Na zilizobakia asili mia hizo tutajua hizi niza watu wa bara. Mambo kama hayo.

**Hussein Rindano:** Mimi maoni yangu ni kwamba nasema watu wa bara wasipate.

*Interjections: Inaudible.*

**Com. Kavetsa:** Okay, sawa ni maoni yako.

**Hussein Rindano:** Ni maoni yangu hayo.

**Com. Salim:** Ni maoni yako. Ikiwa hakuna mwenyeji apewe mtu mwingine.

**Hussein Rindano:** Asante sana. Na kwa swala la pili nasema kwamba tunataka majimbo. Tunataka uhuru wa majimbo.

**Com. Salim:** Asante sana bwana Hussein Rindano kwa maoni yako.

**Com. Kavetsa:** It is one o'clock, may be we can have one more person.

*Interjections: Inaudible.*

**Com. Ratanya:** Unaweza kuwaambia sasa one person.

*Interjections: Inaudible.*

**Com. Salim:** Haya tuendele tafadhalini. Bwana Hassani Ali Ngenya. Karibu. Endelea.

**Hassan Ali Ngenya:** Jina langu naitwa Hassan Ali Ngenya, mkaaji wa hapa Mswambweni. Kwanza maoni yangu nazungumza habari ya Civic Education. Hii Civic Education kusema kweli tunashukuru sana kwa vile Katiba mwaka huu, imeletewa wananchi waizungumze na watoe maoni yao kwa mara ya kwanza. Kwa hivyo tunashukuru sana ma Commissioners kwa kuja kusikiza hapa, natumaini kwamba maoni yetu yale tutayazungumza yatachukuliwa na yatatiliwa maanani, maana watu wengine husema kweli kuwa wana taabu sana mioyoni mwao, kwa maana maoni yao yakitolewa hayatazingatiwa ama hayatachukuliwa. Lakini twashukuru sana mumekuja tutawapa yale ambayo tutawapea na pia tungependa hii Civic Education isiwe niya mwisho hapa, iwe ni jambo ambalo wananchi watafundishwa, si shuleni tu wafundishwe hata wazee wa ngumbaro pia wafundishwe. Iwe ni syllabus maalum, ambayo wananchi wataelezwa mambo yao kuhusu Katiba, kuhusu rights zao na kuhusu mambo yote ambayo wanataka kujua kwa maana mpaka sasa watu wengi wa Kenya tumezibwa macho, hatujui na tunaumizwa wakati kwamba sheria iko lakini kwa sababu huna ujalo utanyanyaswa tu. Kwa sababu umjinga utafanya aje, labda huu ujinga lazima tutaondoa, lazima tuondoe ujinga huu pia wa kujua haki zetu, katika Katiba zetu muhimu sana. Kwa hivyo naomba hii Katiba iwe katika elimu yetu.

**Com. Kavetsa:** Endelea.

**Hassan Ali Ngenya:** Jambo la pili, la kuzungumza ni kwamba elections, mimi naona mpaka sasa tumefanya elections miaka mingi, Kenya imekuwa huru miaka karibu sasa huyu wa thelathini na nane tunakwenda miaka arobaini. Mimi ningea kwanza hii elections iwekwe qualifications hasa kwa ma-councillor. Ma-councillors wawe wanachaguliwa wenye qualification ya form four, mtu hata akifika standard two pia anakuwa councillor. Haya mambo yanakuwa taabu sana, na hizi taabu zimekuwa tunachagua watu ambao representation yao haifai. Kwa hivyo ningea lazima kuwe na hiyo maneno ya kuwa councillors wawe watu ambao wamesoma at least to form four. MP's wawe wamefika form four, lakini hawa councillors wawe form four

leavers, hata kama hawakupita lakini wawe wamefika form four. Hiyo ni muhimu sana.

**Com. Kavetsa:** Umesema MP's wawe na?

**Hassani Ali Ngenya:** Wawe wamepita ile form four.

**Com. Kavetsa:** Umesema mpawe wa form four?

**Com. Ratanya:** Amepita form four na nini?

**Hassan Ali Ngenya:** Amepata D+ na kuendelea, ndio kupita.

**Com. Kavetsa:** Okay, councillors wawe na D+.

**Hassan Ali Ngenya:** Kama amepita vizuri, kama hakupita pia hana neno.

**Com. Kavetsa:** Unajua ile Constitution ya sasa inataka useme kitu kamili.

**Hassan Ali Ngenya:** Amefika form four, basi amepita hakupita, lakini awe amefika form four level.

Jambo jingine ni habari ya hii administration: Kusema kweli, administration ambayo tumekuwa nayo kutoka uhuru, ni administration ambayo iko geared ama imetengenezwa kwa kikoloni siku zile za ukoloni na haikubadilika. Iliwachwa na wazungu, vile wazungu walipoondoka hapa Kenya, waliacha hiyo administration na mpaka sasa haijabadilishwa iko vile vile. Kwanza tunaona hii administration, ile post iwe na Boss na karani, patakuwa na mkubwa pale katika Province wamechaguliwa na wananchi yeye ni karani pale ambaye ni Executive, lakini si yeye mkubwa.

**Com. Kavetsa:** Hapa sasa chief atakuwa karani wa location?

**Hassan Ali Ngenya:** Chief atakuwa karani katika ile board ya council, yule councillor atakayechaguliwa pale yule chief atakuwa ni karani katika ile locational board, atakuwa yeye ni karani, anapeleka mambo ya serikali, ana report, kila kitu anapeleka. DC na kule katika county council atakuwa hata yeye ni karani pale, pana yule councillor ama chairman, ama mayor atakuwa ndiye boss.

**Com. Salim:** ..... (Inaudible).

**Hassan Ali Ngenya:** Kama kazi gani ambayo yatakayofanywa hivi? Hebu tupe mfano maanake .... inaudible.

**Com. Salim:** Watakaofanya kazi zaidi kwa miaka ngapi kwenye nyanja la kuandika? ...(inaudible) mambo ya maji na kadhalika.

**Hassan Ali Ngenya:** Ndio nakuambia sasa hiyo mambo ndiyo yataka yabadilishwe kwa maana sasa anafaa afanye yule mayor ama anafanya yule chairman na vice chairman na wale ma-councillors na wale wachaguliwa wote wanafanya kazi ile, yeye anakuwa pale ana execute, ama anafanya yale mambo ambayo wale watu wamempa. Kwa maana mpaka sasa, kama iliyo ni kwamba yeye anachukua kama ni administrator, anakuwa wewe, nyinyi nyote, wewe sijui councillor, wewe sijui chairman huna lolote. Sasa iko vile na iwe kwamba sasa kuna police officer pale, kama ni katika polisi yuko police officer, kama ni mambo ya Agriculture yuko mkubwa wa Agriculture, kama ni habari ya land yuko mkubwa wa land. Kwa hivyo, everybody has got his own Ministry pale. Lazima afanye ile kazi yake, huyu atakuwa nimtu ambaye anachukua mawazo ya wale watu wote anapeleka serikalini ama ana report ama nini na nini kule kwa mazungumzo. Hiyo ndiyo itakuwa vizuri, lakini kama si hivyo tutakuwa tuna ule ruler moja ana-rule wenzake na wale wengine wanakuwa pale kama hawana lolote wafanyalo. Hakuna ile democracy kamili.

**Com. Salim:** Unasema majina tuyabadilishe kama kuwaitavyo provincial commissioner, District Commissioner tuyaondoe?

**Hassan Ali Ngenya:** Hayo majina yataka yaondolewe kwa maana majina yenyewe yanatisha.

**Com. Ratanya:** Waitwe aje?

**Hassan Ali Ngenya:** Waitwe pengine administrator ama pengine District Officer, something, lakini mengine tutoe kama hayo. Lakini hiyo District Commissioner, Provincial Commissioner yatisha hayo, maana niya hao hao wenyewe wakoloni.

**Com. Ratanya:** Endelea.

**Hassan Ali Ngenya:** Na kwa vile tunasema pia serikali tunayoitaka sisi ni serikali ya majimbo, kama hivi kwa hivyo itakuwa yuko Boss pale katika jimbo letu ambaye ataangalia mambo hayo ya jimbo, taabu zote zilizopo.

Jambo lingine ambalo tungependa kuwa nalo naongezea kidogo hapa ni ile ofisi ya ombudsman, yule mtu ambaye ataangalia haki za wananchi. Kwa maana mpaka sasa haki yako kama una shida na mkubwa fulani pale, pengine DC ama PC ukimshtaki wewe kupata haki si kweli hata kidogo. Maanake itakuwa hivyo hivyo huko huko na kadhalika.

Jambo lingine ambalo ni muhimu sana, nataka kusema kwamba tenure za wale majaji ama kuwe na separate powers, maanake

ni aibu mpaka sasa hivi tulivyo separate powers hakuna unaona. Kwa maana hakuna separate powers za majaji, za civil servants na wengine. Kwa hivyo kuwe na ule uwezo, lakini sasa uwezo hawana, watu wanachukuliwa leo ume-judge kesi yangu kesho wafutwa, kwa maana hakuna guarantee yoyote, it's temporary. In fact, mini husoma mara nyingi kwamba Kenyas are working under the pressure of the President, kwa hivyo hakuna mtu ambaye ana hakika atafanywa aje.

**Com. Salim:** Yaani, wataka security?

**Hassan Ali Ngenya:** Security of tenure lazima iwekwe ya wafanyi kazi wa serikali. Huwa twafanya kazi kwa pressure tu. Kwa hivyo kuwe na hiyo. Pia naona kuwe na Commissions ambazo zinafanya kazi, maana Commission naona pia zimekuwa, na zile commissions zichaguliwe, zichaguliwe vizuri kama commission zichague wana-commission ambao watachaguliwa na wa bunge, sio President achague commission. Kwa sababu hiyo commission ambayo itakuwa nzuri wawe wana-represent ama wanaangalia mambo ya ile commission. Si kuwa mimi nimechaguliwa commission, nimechaguliwa na President, what do you expect surely? I cannot do anything ambayo ni mbovu, lakini wabunge ni wabunge wote, sasa huwezi sema ndiye boss wangu huyu. Kwa hivyo kuwe na commission hizo.

Human Rights Commission, hii commission iwepo, Gender Commission pia iongezwe commission ya gender iwe at least wanawake nao wanaweza kusema mambo yao katika Katiba. Anti-corruption kama unajua mpaka leo inafujo, pia iwepo na Children and Elderly & Disabled Commissions. Kwa maana hawa wazee ambao wameacha kazi, na wengine wamekwisha ni wazee sana, hawaangaliwi Kenya hii. Kwa hivyo ni lazima kuwe na hiyo commission at least wale wazee nao waangaliwe, wasiwe tu ni watu wametupwa kabisa kabisa na Katiba.

**Interjections:** *Inaudible.*

**Hassan Ali Ngenya:** Sio children, elderly & disabled commission. Moja hii ina-deal na hao wote. Kwa maana hawa wote wako disadvantaged people hapo.

**Laughter:**

**Hassan Ali Ngenya:** Nimesema children and the aged and disabled commission.

**Com. Salim:** Uko karibu kumaliza?

**Hassan Ali Ngenya:** Sana. Niko karibu sana. Kwa hivyo jambo lingine ambalo nitasema kidogo ni habari ya land. Wajua land ina taabu sana.

**Com. Ratanya:** Umesema Gender Commission ama Women Commission?

**Hassan Ali Ngenya:** Mimi ningesema Gender, maanake nikisema Women tu nitawawacha peke yao, waume pia wana taabu zao. Kwa hivyo, yaweza kuangalia mambo hayo.

*Laughter/Interjections: (Inaudible).*

**Hassan Ali Ngenya:** Women: Sawa pia maana kuna shida pia. Kuna shida zao waume pia nao, lazima ziangaliwe angaliwe kuwa, unajua hii problem ya kusema gender, tunasema women. Haya mambo yameanza kule ulaya, mpaka sasa wazungu hawana kazi. Wazungu walianza gender ya huko ulaya zamani miaka mia moja iliyopita, sasa when you see a European man and his wife, the man will not say anything, it is only the woman who will talk. Do you know why? Because they have been brought up that way, the men have been shut down nowadays. It is only the women who are brought up. Now, so much talk is done by the women. Hii ni makosa, nasi tunasema gender, women, women mwisho mwisho huko wale watoto wajukuu watakuja kule watakuwa wakifanyaje?

**Com. Ratanya:** Commission ya Gender kama vile ..... (inaudible).

**Hassan Ali Ngenya:** Waume na wakike gender, waume na wake, kila mmoja aweko. Tusiige wazungu tukapata waume au wake peke yao.

Swala lingine ambalo nitazungumzia ni habari ya land: Hii land ni kitu ambacho ni muhimu sana katika nchi na haitumiki vizuri sana kwa wananchi wote. Lakini local communities lazima wapewe nafasi kubwa sana. Wajua kuna problems hizi za land sana. Unachukuliwa land kwa serikali hapa mahali pachukuliwa, paitwa aje, sijui scheme. Hiyo scheme ikija ni bahati mbaya, ni ajabu kubwa sana. Hiyo scheme itapewa watu ambao hata hauwajui, wachukua scheme waende zao. Hiyo scheme haina maana hiyo. Kama ni scheme, iwe ni scheme kwa sababu ya mambo kama hospital yajengwa kwa manufaa ya watu, ama pengine pajengwa shule, yajengwa sababu ya watu. Lakini sio scheme, watu waletwe kwa scheme yeyote yule na wale wananchi ambao wako pale hawapati chochote. Sasa hiyo inakuwa grading of land, ndio tunasema, isiwe mambo ya scheme, yasiwekwe unless scheme iwe ina manufaa ya watu wote, sio ya watu wale ambao wataletwa pale mahali.

Lingine ambalo serikali haifai kuchukua mali za watu kwa nguvu, kwa maana kwingine mali zingine huchukuliwa kwa nguvu, haifai mpaka watu wenyewe wakubaliane na pawe na negotiations vizuri, na watu wakubali kama ni sawa. Kama hayo madini, sijui ndiyo nani yafanywa hapa katika eneo. Wenyewe wanasema hawataki, lakini madini bado yafanya aje? Yachimbwa mpaka sasa, yachimbwa. Minister mwenyewe Kamotho alisema mpaka wananchi wakubali, lakini asema bado yachimbwa. Yeye asema tutaona watu, watakuja Jomo Kenyatta tutapigapiga kelele mpaka leo madini yachimbwa na hakuna lolote na wananchi wenyewe hawakubali. Sasa hiyo ndio mambo mabaya, kuchukua mali ya watu kwa nguvu. Sio sawa.

Sasa imekuwa ile serikali ya ukoloni.

*Interjections: Inaudible.*

**Hassan Ali Ngenya:** Okay, namaliza. Any land ambayo imepangiwa kwa public purpose, any land it should not be changed to another private use, na hii ndio problem inasemekana ni ya public. Unasikia kila siku shule za grade-iwa huku, imeambiwa hii land niya shule lakini siku tatu, nne land hiyo imepata mwenyewe imechukuliwa.

**Com. Salim:** Private developer?

**Hassan Ali Ngenya:** Ndio private developer. Mwisho nasema hii Katiba isiwe ni ya wabunge, maana wengine wanasema Katiba, wabunge sijui nini. Katiba isiwe ya wabunge, Katiba iwe ya wananchi, tuzungumze hapa. Vile tunavyotaka kufanya na Katiba pia wabunge na huo wizi wao wasiwe wataifanya peke yao, wabunge katika mwanzo pia waliharibu hayo yote ile ya Lacanster House kwa kugeza huku na huku ili wapate faida yao. Asanteni.

**Com. Kavetsa:** Ningependa tufanye mambo ili isiwe general sana, tukiketi hatutaweza kueleza ni nini watu wa Msambweni walisema kamili. Unasema Katiba isiwe ya wabunge, pendekezo lako ni nini? Tuketi tu, you know it's a lot more serious than you are taking it, a lot more serious, dead serious, yes. So, already kama Katiba ya sasa inasema niya wabunge, ni bunge kubadilisha. Sasa ukitaka iwe tofauti ungependa aje? Unasema tuketi, sema zaidi ya hapo. Sio vile iko sasa, sema zaidi.

**Hassan Ali Ngenya:** Tuko hapa sasa. Sasa tuko katika process ya kutengeneza Katiba. Kwa vile tutaweza kutengeneza Katiba, ni sisi wananchi tutoe mawazo yetu yote, muya-record mumalize nyinyi Commissioners. Mkimaliza ku ya-record yale mawazo yetu, kuwe na kikao, si cha wabunge peke yao, iwe ni wabunge na watu zaidi ya kama mia ngapi wale ambao wametoka kila area ambao wanaelewa habari ya Katiba vizuri, ambao wako learned na wanaelewa habari za Katiba, tuketi tuzungumze hiyo Katiba. Isipelekwe Bunge, wabunge waambiwe haya hii Katiba rekebisheni, fanyeni haya mabadiliko, hapana. Iwe inafanywa na watu wote. Ikipita pale bungeni, iwe ishatengenezwa. Kule nikusema tunapitisha.

**Com. Kavetsa:** Okay, hiyo ya public land should not be privatised. Tangu 1963 kumekuwa na hiyo kuwapa watu sehemu za mahali, privatisation. Sasa hiyo ifanye aje? Kwa sababu hapa ndio munaelewa vile mashamba yamebadilika or public land imekuwa mashamba?

**Hassan Ali Ngenya:** Kabla wale hufanya ile public land wale watu hufanya scheme unajua, kabla ya kufanya private igeuzwe ile land kuwa ya scheme. Wajue ile elimu iliyoko inafanya public, ile inaitwa trust land ya serikali. Ikishachukuliwa hiyo kutoka kwa watu huchukuliwa kuwa trust land, inafanywa kuwa scheme. Ikifanywa scheme hapo, sasa ndipo inapeanwa. Sasa



tunasema hii scheme isiwapo, maana hii ni njia moja ya kupeana mashamba. Watu wenyewe pale wanachukua mashamba hawawapi mashamba yao wafanya, sio kwamba watu waje wapewe mashamba tu bure na wale wengine pia wakose.

**Com. Kavetsa:** .... (inaudible) hujafika kabisa kwa sababu yes the scheme is there and the public land is there, but it has already been privatised. What will happen to privatised land, if it has already been privatized?

**Hassan Ali Ngenya:** Okay. Thank you very much. I have understood you. Kama iko privatised hiyo inachukuliwa na inarudishiwa wenyewe. Wenyewe warudishiwe land yao, kwa maana it's their rightful property.

**Com. Ratanya:** Jambo lingine, unaposema ya kwamba mambo yarudi kwa wananchi kuhusu shamba kama hilo, kuna pahali pengine tumesikia kwamba kama wataveta wanasema wana council ya wazee, wanasema hivyo huko Taveta, wana council yao ya wazee na ndiyo wanataka waambiwe haya maneno na waseme ama wakubali. Sasa wewe ukisema wananchi unamaanisha kama chama hicho cha wazee, mna chama kama hicho cha wazee hapa? Mna waita nini hapa? Kaya ya wazee – council or elders. Katika Kwale ama Coast yote?

**Hassan Ali Ngenya:** Coast yote kuna Kaya. Walikuwa wakichunga misitu hapa.

**Com. Ratanya:** Taveta ina "Njama" nyinyi muna "Kaya".

**Com. Salim:** Asante sana bwana Hassan Ali Ngenya, kwa maoni yako. Tafadhali kuna form hapa ya kujaza kama unaweza ukatujazia tungefurahi. Kutia jina tu, lakini organization, inaweza kuwa ni binafsi, maoni yako binafsi. Atakusaidia mwenzetu hapo.

**Com. Salim:** Naam, twafuata sequence, ile order tuliyonayo kwenye form. Naam, lakini ngonjea nitakuonyesha hatuwezi kumruka mtu kabisa. Hatuwezi kumruka mtu twafuatia, hebu Collins tupe hiyo register.

**Com. Salim :** It's only one page for registration and we recorded, that is the registration and why, that's wrong and where is that other registration? It's okay, where is the other one, out there? Which is which now, is this for registration or ther other one is for registration? This is for registration. Hebu tulettee ile ingine bwana. There is one for people with selected views, others for registration. We should deal with all. Samahani kuna tatizo moja, tumefurahi kwamba ndugu wetu hapa ametueleza jambo, kwa hivyo tunataka tulitatie sasa.

**Com. Ratanya:** Hawa ndio wamejiandikisha wote. Then we would like to deal with everybody.

**Com. Kavetsa:** And as people come they are noted.

**Com. Salim:** Ni wengi kuliko hawa.

**Com. Ratanya:** No, they are mixed up.

**Com. Salim:** Anyway what we do, we are breaking for lunch.

**Com. Ratanya:** They can sort out when we are on lunch.

**Com. Salim:** Now, tafadhali kuna tatizo moja tutakalotatua ikiwa tutapata muda wa kupumzika kidogo. Wale wanataka kwenda swali dhuhuri wapate nafasi, au kazi kama hizo. Kisha tutakuhakikishia kwamba tutabadilisha mambo, wale waliokuja kwanza watapata nafasi kwanza. Samahani, kuna list hapa ambayo kidogo yatofautiana na ile list ingine. Lakini tutayatatua yote haya, wale waliokuja kwanza watapata nafasi. Kwa sasa twawashukuru na “inshallah” mtarudi baada ya tuseme dakika arobaini na tano, saa nane. Shukrani, asanteni. Sasa ni saa saba na robo.

#### **AFTERNOON SESSION:**

**Com. Salim:** Tafadhali tuanze tena kupata maoni yenu, na tukiendelea mbele nataka kuuliza yuko bwana Suleiman Shauri, ulikuwa wazimia kutupa maoni yako sio? Unataka kusikiza tu, sio, sawa. Nafikiri pia ndugu yetu Ramadhani Mwamzadi yuko? Nafikiri kuwa ataka kusikiza tu, haya.

Na ya pili, katika hizi lists tumeona kwamba wengi kati yenu wasema kwamba wanataka toa Memorandum zao, tu, Memorandum au mswaada. Maoni yao yaliyoandikwa kwenye barua or whatever it is. Ikiwapo kati yenu wale ambao wana Memorandums na hawana haja kusema lolote, wataka toa Memorandum ili turudi tuisome, tu tayari kuzipokea na hamuna haja kungojea. Yuko yote ambaye atakatoa tu aondoke, Memorandum. Karibu, utatoa Memorandum yake pale, utupe jina lako, tutie tick kwamba tushamalizana na wewe. Na ikiwa yuko kati yenu mtu atakaye kuandika maoni yake aondoke, tutampa na karatasi aandike aondoke, bila kumfukuza.

Tu tayari kumpa karatasi aandike, tupokee Memorandum yake, kisha anaweza kuendelea kukaa kusikiza. Kwa hivyo yeyote ambaye ataka karatasi aandike aondoke au akae, tafadhali utaenda kwa Collins pale kijana wa mwisho upande huu, atakupa karatasi utaandika utatuwachia.

**Com. Kavetsa:** Na pia, yule ambaye anajisikia baadaye angependa kuandika Memorandum kwa Tume, au barua kwa Tume, anaweza kufanya hivyo baadaye. Sio hapa ndio mwisho, unaweza kuandika na kutuma, utampa District Co-ordinator au mwana kamati na itatufukia. Usijusikie kama ukipoteza wakati huu, hakuna nafasi ingine.

**Com. Salim:** Na kuna swala, sio? Naam uliza.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Salim:** Wewe ni Civic Education Provider? Uliambiwa na nani?

**Com. Kavetsa:** Lunga Lunga, uliambiwa na nani?

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Kavetsa:** Kuna kitu kinaitwa magazeti, haya mambo yalikuwa kwa magazeti na naamini ukiwa Civic Education Provider unasoma magazeti pia. Na pia, kuna District Co-ordinator, kuna kamati. Sasa ama ulitangaza mambo ya njiani .....(inaudible).

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Kavetsa:** Nani aliandika hiyo barua, leta hiyo barua. Let hiyo barua tafadhali.

**Com. Salim:** Huwezi kuchukua ripoti kwenye polisi au njiani kwa mtu, na wewe ni Civic Education Provider, kuna District Co-ordinator unge-check na yeye kama ni kweli au la?

**Com. Kavetsa:** Nani aliandika hii barua?

*Interjections: Chief?*

**Com. Salim:** Anyway, tuendelee mbele na sasa tumuite Yusuf Mwamzani, yuko? Haya, karibu.

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Jina langu ni Yusuf Bakari Mwamzani. Haya ni baadhi ya maoni yangu katika kuchangia hii Katiba.

Nitaanzia na President: President nachangia kwamba awe niwa nchi nzima. Nikisema awe wa nchi nzima ni kwamba asiwe mbunge. Kwa sababu hii, kuwa mbunge inamaanisha kwamba nguvu zake zote apeleke pale kwao, ili mwakani apendekezwe tena bungeni. Lakini, awe wa nchi nzima ili mwakani kukiwa na uchaguzi apate kurudishwa tena kwa kazi yake nzuri aliyofanya, au atupiliwe mbali na nchi nzima, Kenya nzima kwa kazi yake mbaya aliyofanya. Kwa hivyo, nitapendekeza

kwamba Rais asiwe mbunge. Pia, napendekeza kwamba mtu awe na uhuru wa kujiunga na chama chochote, kinyume cha sasa. Location au District ambayo itakuwa kinyume au haitajiunga na chama cha serikali hatupati maendeleo. Hatupati maendeleo yoyote kwa sababu wanaambiwa wale magaidi hawakujiunga na chama chetu cha serikali, tutawapa adhabu mpaka mwisho warudi huku kwetu. Kwa hivyo uhuru wa chama cha siasa kujiunga, huko huwa umetolewa kabisa, hakuna. Kuwe na uhuru kamili kabisa, kabisa.

*Interjections: (Inaudible).*

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Kadhalika, mahali ambapo maendeleo hakuna, tusitoe visababu eti mbunge wa wapi sio mzuri. Lakini tuseme kwamba serikali hapo imeshindwa, kwa sababu mbunge si aliye na hazina na watu wa pale ikiwa tutasema mbunge wa hapo si mzuri, mbunge wa hapo hajui kusema, hiyo ni kama kuziba ile haki kwamba serikali hapo imeshindwa. Kwa hivyo, lawama isiende kwa mbunge lakini iende kwa serikali nzima. Pia, isiwe ni dhambi, isiwe ni kosa, mwananchi kutaja uzuri wa serikali, au ubaya wa serikali, kuwa utaandikiwa ni makachero kesho utashikwa. Kwa hivyo mwananchi awe na uhuru wa kusifu serikali popote, hata kama ni barabara au kuikosoa serikali popote hata kama ni kwenye matatu, isiwe amefanya dhambi.

Elimu na changia kwamba iwe ya quota system. Tukisema quota system, haimaanishi kwamba hiyo quota ya Kwale ikiletwa, tutajiokotea tu watu wa University kiholela. Pia, patakuwa na merit hapo itafutwe lakini kuwa na quota system.

**Com. Salim:** Quota system kwa shule za msingi nao?

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Kwenye chuo kikuu na shule zozote. Kadhalika tumeona mashule, sekondari, primary yana inspectors. Kwa hivyo, utaona watu, waalimu wanaile nia ya kufanya kazi ili wapate sifa wakati inspector akifika hapo. Kwa hivyo, nataka hizo hospitali pia ziwe na inspector, akifika pale kwenye hospitali aone wafanyi kazi, wakaguliwe kikazi chao vile vile wanaokaguliwa waalimu wa shule. Kwa nini waalimu wa shule wana inspectors, lakini hospitali hakuna inspectors? Kwa hivyo, utaona watu ambao wako chini ya hospitali wanafanya vile wapendavyo, kwa sababu hawana msimamizi kama vile msimamizi wa ma-inspectors. Lakini tulionao hawatoshelezi.

Na changia kwamba mshukiwa atakaposhikwa akipelekwa seli, asiteswe, ajitetee awezavyo. Wala kujitetea isionekane kwamba ni dhambi. Mshukiwa akipelekwa kortini, maneno yake yasikilizwe, si lazima eti mpaka wakili ndipo atasikilizwa. Lakini mimi mshukiwa nitaonekana kama takataka, lakini wakili akisema mimi nawakilisha bwana Mwamzani, hapo polisi watashtuka, jaji atashtuka, lakini mimi mwenyewe sisikilizwi, kwa hivyo maneno yangu pia yakubaliwe.

Kitu kingine ambacho tunachangia ni kwamba hizi settlement schemes tulizosikia asubuhi, mimi ningependelea, ikiwa zitakuweko, wale wa pale karibu wawe nidyo wengi. Kwa mfano, hapa Mswambweni pakiwa na settlement scheme, watu wa

hapa Msambweni wawe kama 75% na sehemu za nje, nje za Kwale District watiwe humu humu, bora tu wawe ni wenzetu.

Kitu kingine nasema katika Katiba hii, shamba zile ambazo zimelala kwa muda mrefu sana, tugawanyiwe sisi. Zisilale hivyo hivyo mpaka hapa tuna shamba za madifani zimelala zaidi ya miaka kumi na mitano sasa. Ikiwa ni miwa tugawanyiwe, ikiwa ni kuuza mahindi tugawanyiwe wale wananchi wa pale karibu, zisilale bure.

County Council nazo zipewe kujisimamia kisawa sawa, zisiwe hazina pesa, mpaka mtu ukipita na maembe hapo barabarani maembe tu watozwa kodi. Kukaanga samaki pia watozwa kodi, kuuza papa pia watozwa kodi, kipande cha papa. Kwa hivyo county council zingepewa pesa za kutosha kutoka hazina ya serikali.

Kitu kingine na changia kwamba kuna maternity leave katika idara nyingi hata za serikali, hata za binafsi. Kwa hivyo katika Katiba hii, natoa maoni yakubaliwe kwamba mwanamke aliyeofilisiliwa, mwanamke aliyeolewa kwa ndoa sahihi apawe “eda” ya kufiliwa isiopungua miezi miwili. Akae nyumbani, apange akili yake iwe barabara, ajue atapambana namna gani na maisha huko nje. Apewe leave ya kuchelewa ya “eda” isiopungua miezi miwili, mwanamke ambaye ameolewa kwa ndoa sahihi.

Malipo ya uzeeni – pension: Mfanyi kazi akistaafu pension yake ifuate msululu ule ule wa idara yake, ile idara yake ilipe pension yake kama vile iliyvokuwa ikilipa mshahara wake. Badala ya kwamba ulikuwa umelipa hapa, sasa kuna tajiri mwingine huko, huku nawe una matataizo kadha wa kadha. Lakini ikiwa ni mwalimu au ni nani zile documents zake zote ziko pale pale apate ile pension yake mara moja kuanzia mwezi huo aliostaafu na kuendelea mpaka umri wake. Kwa hivyo zile idara zivalipe malipo ya kustaafu wale watu wao. NSSF, malipo pia haya yalipwe mara moja mtu ikiwa ameacha kazi, naimsaidie kimaiisha kuliko kuambiwa mpaka miaka hamsini. Leo nimekuwa na kazi maalum, pengine nilikuwa nimeajiriwa, nimefutwa kazi sijui tena nitapata kazi wapi, watu ni wengi, employment hakuna. Sasa naambiwa mpaka nifike miaka hamsini na mimi nina miaka arobaini. Kwa hivyo, nasema NSSF ilipe mtu akifikia kuanzia miaka arobaini hata arobaini na tano. Ikiwa kuna maswali, kabla sijaondoka, asanteni sana.

**Com. Kavetsa:** Kitu kimoja umesema kwa maternity leave wapatiwe miezi miwili. Na juu ya University – quota system, sasa unaridhika na vile university zimetawanyishwa kwa nchi. Hiyo quota system vile zimepangwa wakati wa sasa. Kuna tano Nairobi, kuna mbili Central, kuna ingine wapi. Ndio nakuuliza unaridhika?

*Interjections: (Inaudible).*

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Kwa hivyo zipatikane kila province, yaani sisi wa Pwani pia tusikose.

**Com. Kavetsa:** Umesema serikali ndio ita, unajua kazi ya mwaakilishi wa bunge ni nini?

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Najua.

**Com. Kavetsa:** Sasa unasema asilaumiwe.

**Yusuf Bakari Mwamzani:** ..... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Unajua wengi hawasemi mambo ya kwao. Unajua wengine wako hivyo hawasemi mambo ya kwao.

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Huenda wakawa hivyo.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Salim:** Samahani bwana Yusuf, mwenzangu hapa ana swala kuhusu “eda”.

**Com. Ratanya:** Hii leave ya “eda” unajua wengine wangetaka kufahamu vizuri, ili wakati wa kutetea nitetee sawa sawa (Laughter).

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Kurani kitabu cha waislamu, mwanamke wa ndoa sahihi akifiliwa anajitenga kwa miezi minne na siku kumi. Vile siku zile ni kwamba kujulikane kwamba ikiwa amekuwa pregnant ama nini, niya nani? Tunataka wakati huu at least apatiwe miezi miwili ya kujituliza akili na kupanga maisha atapambana nayo namna gani. Ni miezi minne na siku kumi, lakini na suggest miezi miwili.

**Com. Ratanya:** Lakini kama Islamic law inasema miezi minne unataka Constitution iseme ipunguzwe iwe ni miezi miwili?

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Hapana, huko ataendelea nayo kule nyumbani. Si kwamba imekatika hapo ile leave, official leave.

**Com. Ratanya:** Official one. Kama ameajiriwa na serikali.

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Kama ameajiriwa na serikali. Kama vile maternity leave awe nyumbani miezi miwili kuangalia afya yake. Na huyu pia aangalie afya yake ya kule kufiliwa mpaka pengine miezi miwili atakuwa amepata fahamu namna hiyo.

**Com. Kavetsa:** Na leave ya miezi miwili ikiisha, atarudi kazini?

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Hapana, hatumkatazi kurudi kwa sababu leave imekwisha, atakuwa na “eda” vile vile.

**Com. Ratanya:** Na akijiuzulu atapata mshahara wake?

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Ndio apate mashahara wake.

**Com. Ratanya:** Nataka mshahara wake wote apewe wote wa miezi minne, itakuwa sawa sawa?

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Sawa kabisa.

**Interjections:** (*Inaudible*).

**Yusuf Bakari Mwamzani:** Nakubali na mawazo ya wenzangu. Full “eda”.

**Com. Kavetsa:** We don't have microphones. Then don't let us play with the .... (*inaudible*). Mzee wewe sasa unaweza kufafanulia wengine waislamu sisemi wengine hawawezi, lakini mambo kama haya ambayo iko kwa Koran. Na inafaa ipangwe wakati huu, pengine Supkem itafanya, lakini inafaa ipangwe mambo gani ambayo inafaa iingizwe kwa Katiba, ambayo inaweza kuingizwa, iingizwe, ili isigongane sana. Na vile naona inatolewa kama moja, kwa moja na inafaa iwe kama hiyo yote. Sasa kwanza ikiwa kama msichana wangu, atakuja afunge ndoa kwa mvulana wako, watoto hupendana wenyewe. Halafu yeye ni mkristo amefundishwa mambo fulani na wako ni muislamu, itagongana tukikosa kulete iwe karibu. Ipi inafanana na tofauti iko wapi? Sasa pengine ingechukuliwa muda sijui kama Supkem itafanya au nani, lakini inafaa kama hili jambo kuna wanawake wanaofaa muda huo wa kujituliza. Lakini haijasemwa mahali tumeenda kuna waislamu wengi, lakini hayo mambo hayajatajwa.

**Com. Salim:** That's very important.

**Com. Ratanya:** Kama affirmative action tunaisikia lakini hatujui what you wanted to mean, ulikuwa unataka kusema aje?

**Com. Salim:** Labda nikikusaidia lakini ningemueleza mwenzangu hapa. Hata ikiwa yule mama au yule mjane – widow si muislamu. Ikiwa ameolewa na muislamu lazima pia akae “eda” nafikiri, ili kwamba ikiwa ameshika mimba ijulikane kwamba yule mtoto niwa mume yule aliyefariki. Kwa ajili ya urasi.

**Com. Kavetsa:** Sasa likiwa jambo nzuri hilo kama kwa waislamu, linafaa lizungumziwe ili lionekane hawa wanawake hata kama si waislamu wanafaa kupata eda.

**Com. Salim:** Ikiwa mume ni muislamu.

**Com. Kavetsa:** No, but it can benefit everybody.

*Laughter:*

**Com. Salim:** Sawa, kufuatia dini la kiislamu.

**Com. Kavetsa:** Lakini pengine lingine likiwa kama mtoto wangu atafunga ndoa na mtoto wako, halafu yeye ameambiwa ndoa ni ya maisha, milele. Na sasa anaambiwa shika talaka na anakataa. Naona pia inaweza kuleta shida, kuna yale ambayo yanaweza kuwa mazuri na mengine yanafaa tufafanue zaidi ili tujue ni nini.

**Com. Ratanya:** Kusiwe na complain.

**Com. Salim:** Asante sana mzee Mwamzani kwa maoni yako muhimu sana. Tukiendelea mbele tutamuita Salim Chonga. Salim Chonga yuko?

**Salim Chonga:** Kwa jina naitwa Salim Chonga, mkaazi wa hapa Msambweni. Maoni yangu ningependelea kusema, katika hii Katiba mpya tutakayo, ningependelea kusema huyu Electoral Commissioner asichaguliwe na Rais wa chama kinachotawala, achaguliwe na vyama vyote vya upinzani, au apigiwe kura na wananchi.

**Com. Salim:** Unamaanisha yule mwenyekiti wa Electoral Commission?

**Salim Chonga:** Achaguliwe na vyama vyote vya upinzani, au apigiwe kura na wananchi.

**Com. Ratanya:** Unasema Chairman wa Commissioners? Kwa sababu wanaweza kuwa wengi.

**Salim Chonga:** Commissioner, yule wa nchi nzima.

**Com. Ratanya:** Labda anamaanisha yule mwenyekiti. Unasema wote ma Commissioners? Wote wawe upande wa upinzani?

**Salim Chonga:** Hapana, wachaguliwe na vyama vyote.

**Com. Ratanya:** Anaweza kuwa anasema vyama vya upinzani peke yake.

**Salim Chonga:** Vyama vyote vishirikiane.



**Com. Ratanya:** Na unajua vile ilivyo sasa? Hawa wajumbe 22, wale wako sasa wamechaguliwa kati yao. Na wajumbe wametoka DP, kuna wengine walikuwa wa ile ilikuwa ya Odinga ya zamani, kuna KANU, kuna SDP yaani, sasa unamaanisha nini kwa sababu kama sasa tulivyo wale wako 22 wametoka vyama vyote ama pengine hukujua?

**Salim Chonga:** Sikujua hapo.

**Com. Salim:** Endelea.

**Salim Chonga:** Jambo lingine ni kuhusu hizi police stations. Mtu akishikwa kama uko muda wa kwenda kortini, aende siku ile ile, sio awekwe pale kwa siku nyingi. Nikirudi hapo hapo kwa police, mtu akiwa cell awe na freedom. Madhali amewekwa cell awe yuko ndani ya cell, sio alale na fingo.

**Com. Kavetsa:** Hawa waalimu walikuwa wakienda round. Wanasema wamefundisha watu lakini ungejua hili la Electoral Commission. Yes.

**Com. Ratanya:** Unajua kuna Electoral Commission na hii tunayo sasa hii ya Constitution Review Commission. Ama unamaanisha hii yetu.

**Salim Chonga:** No, ni ya electoral, hiyo Electoral Commission.

**Com. Ratanya:** Kwa sababu wengine wana-confuse. (*Laughter*). Ile ya uchaguzi na ya kurekebisha Katiba.

**Com. Salim:** Inatayarisha uchaguzi na kila kitu. Asante sana. Sasa twamuita Anisa Hussein Kilalo. Ameondoka, ametoka? Still on lunch, okay. Omari S. Tsuma. Ni Tsumo au Tsuumo?

**Com. Kavetsa:** S. ni Salim au Sali.

**Omari S. Tsumo:** Salim.

**Com. Salim:** Wajua kuna list ile tunafuata na tukasema kwamba tutaifuata ile list, halafu watu wengine wakijiandikisha tufuate hiyo.

**Interjections:** (*Inaudible*).

**Com. Kavetsa:** Mnapata tu one full day ambayo kila mtu anapata.

**Omari S. Tsumo:** Jina langu ni Omari Salim Tsumo. Kwanza mimi hasa naunga mkono serikali ya majimbo. Na sababu ambazo zimenifanya nipendelee serikali ya majimbo, ni kwamba huenda tukiwa na jimbo letu, au kila watu wakiwa na jimbo lao, itapatikana nafasi ya watu kuangalia matatizo ya jimbo lao ni nini. Kwa mfano, kama sasa, jimbo letu hili tumepungukiwa na viwanda kadhaa na tukiwa tumejitenga au tuna serikali yetu ya majimbo, tutapata nafasi ya kutafuta matajiri nje ili kutuletea viwanda kwa yale mazao ambayo mpaka sasa yanaoza bila kufikiriwa ki vyovyote. Tuna maembe mengi, mananasi, machungwa, hayo hayana kiwanda chochote. Mpaka sasa hayana kufikiriwa, lakini tukiwa na jimbo letu nafikiri mambo kama haya, tunaweza kuyapunguza ili tuweze kutafuta wale wasajili ambao wanaweza kuleta viwanda kwa mambo kama hayo.

Jambo lingine nafikiria kwamba kuwe na serikali moja imebidi hazina yote ya nchi iwe iko headquarters. Na hii husababisha mutumishi wa serikali anangojea mapato yake baada ya mwezi umemalizika, anapishwa mpaka tarehe ishirini hajajua mshahara wake uko wapi. Lakini tukiwa na majimbo, nafikiri kila jimbo litakuwa na hazina yake karibu, mambo kama haya huenda yakapungua.

Kitu cha tatu nakichangia ni kwamba ni fedheha kubwa kwa mwanamke yeyote kwenda hospitalini akiwa mja mzito na mwanamke huyu awe anahudumiwa na wanaume ikiwa mid-wife ambao ni wakike wakio pale, lakini wanaume wanahudumia wanawake kama hawa waja wazito. Hii nafikiri katika Katiba isiwekwe, isipokuwa mahali ambapo hakuna mid-wife wa kuhudumia wakina mama kama wale waja wazito.

Kitu kingine nafikiria pensioners, kwa sasa tuseme mtu akiwa ame-retire ni pensionable, nafikiri baada ya kufariki kwake, kwa sasa kuna malipo ya miaka mitano baada ya huyu muhusika kufariki. Lakini ningependelea badala ya miaka mitano katika wakati huu tulionao, iwe miaka kumi badala ya miaka mitano.

**Com. Kavetsa:** Umemaliza?

**Omari S. Tsumo:** Nimemaliza.

**Com. Kavetsa:** Okay, Je, ya mwisho unamaanisha nini?

**Omari S. Tsumo:** Ya mwisho ninamaanisha kwamba mpaka sasa mtu ambaye ni pensioner akifariki anapata malipo, waarasi wake wanalipwa kwa miaka mitano mbeleni. Kwa hivyo, badala ya miaka mitano, iwe miaka kumi. Na watu wa pension wanasahauliwa sana kwa nyongeza za mishahara.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo unapendekeza nini?

**Omari S. Tsumo:** Napendekeza serikali iwe inawafikiria kila wale civil servants wakiongezwa na hawa wapate kufikiriwa kidogo.

**Com. Kavetsa:** Mzee naona nimesikia kuna Civic Education Providers hapa, lakini sioni dalili ya civic education hata moja. Hiyo inaitwa, hiyo yakuongezwa hivyo na pia inaambatana na inflation, vile bei ya maisha inaenda juu, pia pension inafaa iongezwe na umesema kitu muhimu sana. Asante. Lakini Civic Education Providers I would like to say sioni informed choices, pengine mtu mwingine anaona. Can you call another person?

**Com. Salim:** Suleiman Abdalla.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Kavetsa:** Sioni dalili ya Civic Education hapa. Kuna mambo mazito na kila mtu anayafanya nyepesi. Civic Education Providers walifaa wawaonyeshe uzito wa mambo, ili watu wakizungumza walete opinions zake ziko informed. Ukichagua serikali ya mseto unajua maana yake ni nini. Ukichagua serikali ya majimbo unajua maana yake ni nini. Ukisema hapa industry ilitokea unajua maana yake ni nini, ilitokea vipi. Ukisema hakuna Universities hapa unajua ni nini unasema, lakini sasa watu wanasema tu mambo na hiyo ni sawa, maoni yako vile unajisikia ni sawa. Lakini sioni ile dalili ya watu waliofundishwa.

*Interjections from audience:* Problem iliyoko watu wengi madam kuongea ukweli, watu wengi hawajali vile civic, wanaongea kama watu watano watu sita. Kwa hivyo swali hilo lenyewe watu wenyewe wana problem ya kwamba vile watu wanachukua civic education, nitasema sio serious watu wote, labda wangukuwa serious wangukuwa wanahudhuria civic education na ingekuwa vizuri sana. Lakini kwa hakika wengi wanatoa maoni lakini hata hawakuja kufundishwa civic education.

**Com. Kavetsa:** All you have to know is that your are will be affected. Wajue to hivyo, kwa sababu tunauliza uliza vitu vidogo ndiyo tukapata maana ambayo ni ya Katiba.

**Com. Salim:** Naam bwana Suleiman Abdalla. Tafadhalini maoni yatolewa.

*Interjections: Sema jina lako.*

**Suleiman Abdalla Machafu:** Jina langu ni Suleiman Abdalla Machafu, ni mkaazi wa hapa Msambweni. Mimi serikali ninayoiunga ni ya majimbo. Shida nyingi sana zimetokea hapa kwetu nchini Kenya kwa sababu ya kwamba watu wamewekwa mseto. Na mseto wakati mwingi huwa unaleta dhiki moja, ya kwamba wale ambao wanamanufaa zaidi ni wale walioko mbele. Na tatizo hili limefanya kwamba tamaduni zetu nyingi zimepotea. Mdigo alikuwa na asili ya kuwa shamba au ardhi hauzi. Hawa wote hawa walioko hapa, uhuru ulipopatikana waliweka mikataba kwamba ardhi zao zilindwe. Kwa sababu ya serikali

ya mseto ya unyang'anyaji wa ardhi, watu wamesahau haki zao. Leo hii mtu anakuja anasema kwamba ardhi igawanywe. Babu yake aliyezaa baba yake, aliyezaa yeye, na waliokuwako kutoka enzi za mrego, kutoka enzi za muarabu, kutoka enzi za muingereza, mpaka uhuru unapatikana waliweka mikataba ya kwamba ardhi zao zote ziko kamili. Leo hii wamekuja wamewekwa katika muongozo ule wa utumwa, na kutawala katika mlolongo ule wa ujinga, wakaambiwa kama wameelimika mpaka wanajikuza kibilahi. Nimefika form four, nimefika university, lakini wamepewa muongozo ule wa kutawalwa, ambao sio wa Mungu. Ni wa ulimwengu tu na kunyang'anywa, wanakubali ardhi ziuzwe. Kwa sababu gani, serikali ya mseto ilikuja pale, ikavunja mikataba walioweka Lacanster House, ikavunja mikataba ile waliochukulia Uhuru, wakasema hiyo wagawanyane vipande vipande vipande. Na walikuwa wamewekwa masikini wakujiwunia kwamba hao ni wenye mapato.

**Com. Ratanya:** Sasa unapendekeza nini?

**Suleiman Abdalla Machafu:** Mimi ninapendekeza kwamba serikali iwe ya majimbo. Kwa sababu yaani hizo ni moja wapo ya tamaduni ambazo tunazungumza.

**Com. Kavetsa:** Endelea.

**Com. Salim:** Pendekezo la pili?

**Suleiman Abdalla Machafu:** Pendekezo la pili ni kwamba ardhi zote ambazo wale walioziweka, wakasema zilindwe, zirudishwe kwa wenyewe kama tamaduni zao, wazee wa ma-Kaya. Wazee wa ma-Kaya warudishiwe ardhi zao, watagawanyia watoto wao vile watakavyo. Scheme ivunjiliwe kabisa, wala haina ardhi iliyonunuliwa hata moja. Serikali ya mseto haikununua ardhi kwa mtu. Kwa hivyo ninasema kwamba haramu zilizofanywa za kufanya ardhi kuwa settlement, hizo settlement hizo za ardhi zivunjwe kabisa, hawa wote wanajua kwamba wanahaki. Hakuna mmoja hapa ambaye hana share ya Maunda, wote wametoka Maunda. Lakini kwa sababu ya kwamba wamewekwa katika mfumo ule wa ng'ombe, leo ile ng'ombe wameifanya ya wakamba. Kama wana majimbo yao wangejua wale wakamba ni wakenya? Lakini kwa sababu ya kwamba wanatumwa ni wale wale wakamba na wakikuyu, na wajaluo, na wabaluha wanasema kwamba ardhi igawanyiwe kwa wananchi. Wewe kweli kitu chako unaweza kubali kigawanywe, na wamefanya kazi huko, kila sehemu wamefanya kazi. Hawana hata ardhi huko nje. Na hii ndio majimbo ndiyo kitu kimojawapo. Na mimi nikisema kama Zema Makanya, ninasema kwamba sisi tulioko hapa Pwani tunaweza kuendesha serikali yetu. Tusingeomba serikali itujengee University. Wakati kulipopatikana Uhuru ma-professor wote walikuwa ni watu wa Pwani, wajomba wetu Mazrui. Mazrui wajomba wetu hao, tulikuwa nao hapa, walikuwa ni ma-professor hapa. Kenya haikuwa na ma-professor. Walikuwa wakikuyu kidogo, wajaluo ndio wengi, ama wabaluha ndio wengi, lakini kwa sababu tamaduni zimevunjwa, mpaka eneo hili mtu akitajiwa jambo la Kaya anaenda kwenye kitabu cha Kurani na hicho kitabu cha Kurani haina hata kitu moja hapo anaweza aka kiandama. Anakwenda kwenye kitabu cha bibilia, mduruma na mdigo na mpokomo wanakataana kwa sababu ya ukoloni, ambao umewafanya maskini na mgiriama. Sasa ule umaskini uliofanywa nao kila moja anacheka mwenzake lakini wote wako tupu.

**Com. Kavetsa:** Pendekezo?

**Suleiman Abdalla Machafu:** Pendekezo ni majimbo.

*Interjections: (Noise from the crowd).*

**Com. Kavetsa:** Umemaliza?

**Suleiman Abdalla Machafu:** Sasa ninaomba kwamba, kulingana na tamaduni zile, yale mashamba yaliyochukuliwa ambayo ni haki yao ni land owner. Kama vile Iramisi. Kitaruni hapa imechukuliwa ni Gema kwa sababu ya ufalme uliyokuwako huku. Ni ardhi ya mdigo tu mwenyewe ni barua huko. Chairman huyu ambaye ni wa Msambweni commission aliingia hapo. Yeye ni mwenyewe, lakini anaona haya kwa sababu ya yeye hawezi kujitaja. Kwa sababu ya nini? Ya nguvu hana. Najua mimi nikisema hivi leo huenda hata yule aende huko.

**Com. Ratanya:** Nani?

**Suleiman Abdalla Machafu:** Mzee Barugu. Lakini najua yeye ndiye atakayetengeneza serikali.

**Com. Ratanya:** Huyu mzee wa Kaya?

**Suleiman Abdalla Machafu:** Huyo mzee wa Kaya. Huyo.

**Com. Ratanya:** Asante bwana Abdalla.

**Suleiman Abdalla Machafu:** Nina mengi lakini inshallah kwa sababu yangu unajua niya kimaumbile nina mengi. Kwa hivyo nawapendelea wenzangu waongee lakini nataka majimbo.

**Com. Salim:** Maoni yako yamenaswa kwenye tape. Asante. Sasa naona kina mama watatu wameingia yumo kati yao Anisa Hussein yuko? Amefika. Anisa, ngoja kidogo.

**Com. Kavetsa:** Civic Education Provider yuko wapi? Okay. Kwa nini unasumbua wengine, nimekuuliza civic education providers. Nitaauliza huyu. Mlipofundisha watu aina za serikali mliwafundisha majimbo ni nini? Mkawafundisha oppositte ya majimbo ni serikali gani? Kwa sababu mzee ametumia hapo, serikali ya mseto. I want to know here what terms to use, which is the opposite. You are passing the bus.

**Civic Educator:** Okay, umesema serikali ya majimbo, ni serikali ambayo.

**Com. Kavetsa:** I just want to know what is the opposite.

**Civic Educator:** Opposite ya majimbo .... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** Nataka kujua kwa Kiswahili mliwaambia nini na kwa kidigo. Mliwaambia serikali ya mseto is the opposite of majimbo.

**Civic Educator:** Tuliwaambia ni serikali ya umoja, or can you come again?

**Com. Kavetsa:** I can't come again. What is the opposite of majimbo in Kiswahili.

**Civic Educator:** You know what I mean.

**Com. Kavetsa:** I don't know what you mean. What did you teach them? Kwa Kiswahili uliwaambia unitary ni nini?

**Civic Educator:** Unitary ni ile ya mseto.

**Com. Kavetsa:** Please, just leave it.

**Com. Ratanya:** Central Government - mseto.

**Com. Kavetsa:** Mseto is coalition. Wacha tuwache hapo kwa sababu tutachanganyikiwa zaidi.

**Com. Ratanya:** Lakini Kenya sasa haina serikali ya mseto.

**Com. Kavetsa:** Don't say that word again.

**Com. Salim:** Basi bwana Hassan shukrani. Anisa Hussein Kilalo.

**Com. Kavetsa:** Excuse me, hili sio jina la mama? Anisa.

**Interjections:** *Mimi ni Anisa.*

**Anisa Hussein Kilalo:** Mimi jina langu ni Anisa Hussein Kilalo. Ama mimi yangu ni shukrani tu kulingamana na watu ambao walitueleza kukusanya hii Katiba, wale ambao mliwafundisha nao wakaja wakatufundisha. Kwa vile yale ambayo sisi tulikaa tuKayajadili, tukazungumza mpaka tukaona kwamba hapa tumefikia kulingamana na fikira zetu, na ziko katika kitabu chetu ambacho tushaandika, hapo mimi nashukuru na sitazidi kuzungumza lolote lile, kwa sababu hayo yaliyoko humu ni yetu sisi sote na mimi nikiwemo. Kwa hivyo kwa hayo machache asanteni.

**Com. Ratanya:** (Inaudible) upeane Memorandum tu.

**Anisa Hussein Kilalo:** Memorandum yetu iko hapa.

**Com. Salim:** Sasa twamuita bwana Asman H. Machafa.

**Asman H. Machafu:** Mimi nasikiza.

**Com. Salim:** Ulikuwa kusikiza. Sawa. Nafikiri Bakari Chemelwe pia alikuja kusikiza. Yuko? Umekuja kusikiza sio bwana. Asante karibu.

**Bakari Chemelwe:** Ndio.

**Com. Salim:** Jume Pengo, pia nafikiri amekuja kusikiliza na kwa hivyo nitamuendea bwana Hassan Ngenya. Ashaazungumza.

*Interjections: Ashaazungumza. You didn't tick his name.*

**Com. Ratanya:** Tulikuwa na list ingine sasa tunarekebisha.

**Com. Salim:** Nafikiri hata bwana Hussein Rindano ashatoa maoni yake. Yusuf Ndreje.

**Yusuf Ndreje:** Mimi ni Yusuf Ndreje kutoka hapa Msambweni location. Kitu ambacho nimekuja hapa kutoa maoni yangu, mpaka sasa kuna msemu katika Katiba ya zamani, kwamba kuna uhuru wa kuabudu. Hili neno linaimbwa tu, uhuru wa kuabudu, lakini utakuta linaimbwa kinyimbo lakini haijapatikana. Kwa sababu ifuatayo. Utakuta Muislamu amepewa uhuru wa kuabudu wa bandia. Kwa mfano, mwanamke, mtoto wa kike kisheria ya kiislamu ni kwamba aingie awe amevaa vazi la sitara. Lakini akishafika darasani vazi la ijabu lavuliwa huwa anasoma bila ijabu. Vile vile mwanamke wa kiislamu katika kazi. Nyumbani atakuwa amevaa buibui, lakini akishafika ofisini, ofisa wake anataka lazima buibui livuliwe. Kwa hivyo, sasa utakuta hiyo ni kwamba uhuru wa kuabudu hakuna. Kama vile tunataka ambavyo, mfano nikitoa mfano wa makalasinga. Kalasinga

mmoja katika kilemba ni moja katika sheria yake ya dini yake, halafu utakuta kalasinga anaruhusiwa kuvaa kilemba, halafu unakuta mwanamke wa kiislamu, akifika mahali fulani anaambiwa avue buibui. Kwa hivyo uhuru huu tunataka ukamilike. Ikiwa ni mwanamke wa kiislamu inampasa ijabu yake aiingie nayo shuleni na aiingie nayo mpaka kazini kwake bila kunyanyaswa, bila kusumbuliwa.

Sehemu nyingine ambayo nataka kuchangia ni kwamba, katika hospitalini zetu, wote tulipokuwa tumetawaliwa, utakuta wakina mama wanazalishwa na wakina mama wenzao, na ambapo wakati huu utakuta watumishi ni kidogo, halafu utakuta kulikuwa na heshima. Kwa sababu heshima hii iko katika mila, lakini leo heshima hii imeondoka, utakuta ya kwamba mwanamke leo anazalishwa na mwanamume, ambapo hii si mila ya dini wala si mila za kiafrika.

Tukiridi katika upande wa elimu, schools – ni kwamba watoto wa kiislamu huwa hawapati mafundisho yao ya kiislamu katika shule. Kwa hivyo, ni kwamba tunataka Katiba hii, mtoto wa kiislamu akiingia shuleni lazima hakikishiwe shule hiyo vile vile kuna mwalimu wa kiislamu, iwe anafundisha mafundisho ya dini ya kiislamu. Sehemu nyingine ambayo nataka kuzungumzia hapa katika Katiba, schools kila watu huwa na skuli zao, kuna missionary schools na school za waislamu. Leo utakuta shule za waislamu ni kwamba huwa anaruhusiwa mtoto ambaye si wa kiislamu, lakini utakuta katika missionary schools hairuhusiwi muislamu. Kwa hivyo vile vile, Katiba hii vile vile ni moja katika kitu ambacho si kizuri. Kwa hivyo utakuta shule ya muislamu aingie muislamu na wa missionary aingie u-missionary wake. Lakini isichanganywe shule ya waislamu kwamba lazima asome mtoto wa kikristo kwa sababu unaambiwa kuwa hii ni Kenya moja. Hili si kweli.

**Com. Salim:** Yaani watoto wa kiislamu wasome peke yao?

**Yusuf Ndreje:** Watoto wa kiislamu ni kwamba shule kama ni ya waislamu, watoto waislamu wasome peke yao, waislamu. Lakini sio ule wa kiislamu anachanganywa na mtoto ambaye sio muislamu.

**Com. Salim:** Haya ni maoni yako, lakini tunataka ufafanue kidogo.

**Yusuf Ndreje:** Kama vipi?

**Com. Kavetsa:** Umesema eti shule ya waislamu iwe ya waislamu, ya wakristo iwe ya wakristo, ya wakalasinga iwe ya wakalasinga. Haya, sasa hiyo ndiyo kitu nasema ndio muhimu kwa sababu haitakuwa kutatizika kwa watoto wa kiislamu wa kike kutovaa nguo za kiislamu. Kwa sababu atakuwa kwa shule ya waislamu, sivyo?

**Yusuf Ndreje:** Hilo kwangu ni sawa.

**Com. Kavetsa:** Hawataambiwa watoe nguo za kiislamu, kwa sababu watakuwa kwa shule ya waislamu. Sivyo? Okay, sasa



unasema separate schools, schools tofauti kwa dini, okay sasa nani anachanganya? Si serikali?

**Yusuf Ndreje:** Sasa unakuta kwa sababu ni mtoto wa mkubwa pale wakikristo, lakini anafanywa lazima aende shule ambayo niya waislamu.

**Com. Ratanya:** Hiyo unasema kutoka primary mpaka hata university? Mbali mbali.

**Yusufu Ndreje:** Mbali mbali aje?

**Interjections:** *(Inaudible).*

**Com. Salim:** Kwa kila dini lijenge shule tofauti na gharama ya kujenga shule hizo za wakristo na waislamu na wabaniani ....  
(interjection).

**Yusuf Ndreje:** Zinaweza kuwa za machanganyiko lakini muislamu aruhusiwe kuvaa mavazi yake.

**Com. Kavetsa:** Lakini umesema ziwe tofauti. Kitu muhimu umesema si mambo ya mavaazi, ni mambo ya shule ziwe tofauti.

**Com. Salim:** Yaani zijengwe shule tofauti, waislamu zao peke yao. Na je, kama hakuna uwezekano?

**Yusuf Ndreje:** Mchanganyiko uweko, lakini waislamu wasinyanyaswe juu ya haki zao.

**Com. Salim:** Lakini kama mwenzangu alivyosema, hakuna mtu anayemlazimisha mtu kubadilisha mila yake au kumlazimisha kwa mfano msichana muislamu avue ijabu.

**Yusuf Ndreje:** Kwingine wanalazimishwa.

**Com. Ratanya:** Lakini hakuna sheria hiyo ya kulazimisha.

**Yusuf Ndreje:** ..... *(Inaudible).*

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo kwenye Katiba wataka tuseme nini? Mtoto wa kiislamu asilazimishwe kuvua nguo yake. Na katika maofisi unapendekeza vile vile, kuwe na maofisi ya hao waislamu peke yao au namna gani?

**Yusuf Ndreje:** Muislamu awe ofisini yoyote ile, lakini haki zake zisidhulumiwe, avae mavazi yake kama inatakanavyo.

**Com. Kavetsa:** Nataka kuuliza na wanaume waislamu, kwa sababu mimi naona wanawake waislamu wanajitahidi sana, wanaweka kitambaa kidogo hivi kama huyu msichana amekaa hapa mrembo mzuri huyu. Lakini wanaume waislamu wao pia wana mavazi wanafaa wavae kwa kazi?

**Com. Ratanya:** Wana mavazi special?

**Com. Salim:** Anyway, hayo ni mambo muhimu na kwa hivyo sisi tunataka kujua hasa tunaambiwa tufanye kitu gani. Kwa hivyo utatosheka pengine vile kukawa na kifungu katika Katiba mpya kusema kwamba msichana wa kiislamu au bibi wa kiislamu aruhusiwe kuendelea kuvaa hijabu au buibui kazini na shuleni. Hapo tu.

**Yusuf Ndreje:** Sawa.

**Com. Salim:** Tatizo lako litaondoka tukifanya hivyo sio? Bibi wa kiislamu au msichana wa kiislamu ana haki ya kuvaa ijabu au buibui kazini na shuleni , asilazimishwe kuvua. Asante.

**Com. Ratanya:** Na hiyo kazi ni mbali mbali, kuna polisi, kuna nurses, kuna clerks. Sasa kuna tofauti hapo. Kwa sababu polisi wana uniform.

**Yusuf Ndreje:** Kwa mfano, polisi huyo havai buibui.

**Com. Salim:** Lakini Commissioner akiuliza ikiwa msichana wa kiislamu anataka kufanya kazi polisi, au army .... (interjection).

**Com. Kavetsa:** Tunauliza maoni tuelewe maoni yako, hii si debate. Tafadhali, there is no point of order, this is not a court. We are listening to him. Tunasikiliza mambo yake ukiwa na yako ugonjee wakati wako.

**Com. Ratanya:** Tukimaliza pengine utamuuliza clarification kwa sababu yeye ndiye ana present. So, we have to finish our clarification na wewe.

**Com. Salim:** Bwana Yusuf kwenye jeshi au polisi, ikiwa msichana wa kiislamu atakayeingia polisi au kwenye jeshi kufanya kazi, akuambie mwenzangu hapa, si lazima atavaa uniform. Na buibui si uniform. Kwa hivyo tufanye nini katika hali kama hiyo?

**Yusuf Ndreje:** Hapo ni kivyake akitaka kuvaa uniform sawa, akitaka kuvaa buibui sawa.

**Com. Salim:** Muhimu ni kwamba asilazimishwe kuvua buibui ikiwa ataka kuvaa?

**Com. Ratanya:** Kuna mmoja alikuwa na clarification hapa?

**Com. Kavetsa:** It's useless.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Salim:** No, what we are trying to do is seek clarification. They may not have the ability to say exactly what they want. So we are trying to ask them questions to know so that we understand exactly what they are saying. That's all we are going and we have that duty to seek clarification so that we understand exactly what is being said. Maanake ni muhimu kwetu kufahamu mapendekezo na maoni, ikiwa hatukufahamu. Kwa hivyo, mambo haya ya ijabu tuseme au buibui wasema kwamba wasilazimishwe, sasa twamuuliza katika hali kama hii ni vipi. Kisha ni kwamba mshakubaliana kwamba madam yeye mwenyewe hana wasiwasi, ataka kuvaa uniform ya polisi, muache basi. Lakini asilazimishwe kuvua buibui akiwa ataka kulivaa buibui. All our questions were leading towards getting to know exactly what he wants and to make it easy for us.

**Com. Ratanya:** Tunatafuta constitutional issues, kunayo mambo yanahusu kuingia kwa constitution na kuna malalamiko hivi hivi. Kwa hivyo tunataka nyinyi mfafanue.

**Com. Salim:** Na bila shaka bwana Yusuf afahamu sababu ya kuulizwa haya maswala.

**Yusuf Ndreje:** Ninafahamu.

**Com. Salim:** Ya kuwa twajadiliana majadiliano hapa si kubisha, twataka kufahamu hata madhumuni ya mapendekezo yako. Asante. Ushamaliza? Bwana Bashir M. Kilalo. Twaendelea kufuata hii list, jina lako liko wapi kwa hakika lakini? Nafikiri huyu pia amekuja kusikiza.

**Bashir M. Kilalo:** Anatoa maoni kidogo, yuko hapa tayari.

**Com. Salim:** Ulijiandikisha kutoa maoni au?

**Bashir M. Kilalo:** Niliazimia kutoa maoni.

**Com. Salim:** Ni oral, ni written Memorandum.

**Bashir M. Kilalo:** Nimesema ni verbal, nimeandika form nyingine. Kwa halifu nyingine nilikuwa nimeandika verbal, oral.

**Com. Salim:** Sawa endelea.

**Bashir M. Kilalo:** Mimi ni Bashir Mohamed Kilalo ni mwalimu, mwalimu mkuu wa shule hii tuliyoko saa hizi. Katika Katiba ya Kenya, nitakuwa na mawili ya kuchangia.

La kwanza ni basic human needs, lakini nitaziita basic Kenyan needs: Katika basic Kenyan needs tutaingiza vitu vifuatavyo. Maji safi kwa kila mwanakenya. Kila mwanakenya apewe fursa au apate fursa ya kunywa maji masafi, popote pale anapoishi katika Kenya hii. Kuna sehemu nyingi sasa hivi ambazo maji ni ya taabu sana. Wananchi wajivunia uhuru wao, lakini matunda ya uhuru bado hawajayapata moja wapo ikiwa ni hiyo maji.

Pili ni mawasiliano: Tunaambiwa tujivunie uhuru, lakini kuna sehemu za Kenya ambazo sasa hivi kukiwa na shida mtu akifika hata makao makuu ya wilaya ama ya mkoa, atakuwa amemaliza siku nyingi sana, kwa kuwa hakuna usafiri wala hakuna njia ingine yoyote ya mawasiliano, hakuna simu. Napendekeza hivi.

**Com. Salim:** Bwana Kilalo, ukieleza kila jambo na pendekezo lake utaumaliza wakati wako.

**Bashir M. Kilalo:** Sawa. La tatu katika basic Kenyan needs iwe ni umeme au moto. Kila sehemu ya Kenya hii ingefikishiwa umeme au huduma za umeme na ufanywe malipo ya hafifu ambao kila mwanakenya anaweza kupata matumizi yake. Iwe ni katika basic Kenyan needs.

**Com. Kavetsa:** Unasema Kenyan needs kwa nini, sio human needs?

**Bashir M. Kilalo:** Nimesema Kenyans kwa maana nataka serekali yetu tukufu itakayochaguliwa ama itakayopendekezwa, ifanyie wakenya wake.

La pili ni elimu: Katika elimu napendekeza kwamba serikali itakayochaguliwa ama kupendekezwa na wananchi wa Kenya, ione kwamba kila mkoa utakuwa angalao na national schools tatu, moja wapo ikiwa ni ya ufundi. Shule hizi zisimamiwe na serikali katika upande wa vifaa na kila kitu, ili kusiwe na sehemu nyingine inapata vifaa vingi zaidi kuliko nyingine, kwa sababu national schools ndiyo catchment ya universities. We are sure kwamba mtoto akienda katika national schools tayari ataenda university. Lakini sehemu nyingi hazina ambayo inakuwa ni shida kwa wengine kwenda university. Katika upande huo wa elimu.

**Com. Kavetsa:** .....(inaudible) because the catchment areas kuna watu wengine wanasema iwachwe wazi .... (inaudible) ndiyo itachagua. Hapo ungependa aje hapo?

**Bashir M. Kilalo:** Hapo ningepeda quota system hii bado inaendelea.

**Com. Kavetsa:** Ndio nasema ukisema jambo uliseme kabisa tulielewe.

**Bashir M. Kilalo:** Upande huo huo wa elimu lakini sasa kwa upande wa waislamu. Vile ambavyo serikali yetu saa hizi imetupatia nafasi ya kuwa na Kadhi, napendekeza pia vile vile serikali ipate kujenga vyuo au shule za upande wa waislamu. Ikiwa muislamu atakuwa ametoka kwa post secondary school na angependa kusoma dini yake zaidi, iwe kuna pahali atakapokwenda kujifunza pale zaidi. Sijui kama nimeeleweka.

*Interjections: (Inaudible).*

**Bashir M. Kilalo:** Kwenye secondary schools, kuna colleges na university.

**Com. Kavetsa:** From primary au from secondary, do we have post secondary?

**Bashir M. Kilalo:** Post primary. Nimefikia mwisho.

**Com. Kavetsa:** Wacha nikuulize zaidi hapo, kwa sababu mzee alisema inafaa watoto wafundishwe elimu ya Islam kwa shule, wanafundishwa? Nakuuliza kuna subject Islamic Religious Education?

**Bashir M. Kilalo:** Ndio.

**Com. Kavetsa:** Mpaka class gani?

**Bashir M. Kilalo:** Mpaka secondary.

**Com. Kavetsa:** Sasa ile unasema ni post-secondary not post-primary.

**Bashir M. Kilalo:** Ni post-primary kwa sababu hii ....(inaudible) kwa primary na ataonelea kwamba atamuingiza kwa .... (inaudible) ile iliyoko katika secondary ... (inaudible) kwa mfano ikiwa tunasema tupate Kadhi wa kiislamu huyu lazima awe amesoma kwa hali ya juu sana, sio ile tu iliyoko sasa hivi.

**Com. Salim:** Kenya ni nchi ya dini tofauti tofauti, syllabus zilizoko shuleni pia ni national syllabus na tunavyojua ya kwamba syllabuses zimejaa subjects. Kwa hivyo tukianza kuingiza pia Islamic Religious Education in the syllabus in a more concentrated

manner won't that cause problems, you are an educationist?

**Bashir M. Kilalo:** Nafikiri yangu ni .... (inaudible) halafu anaonelea awe ....(inaudible) peke ya .... (inaudible).

**Com. Salim:** Ya serikali?

**Com. Kavetsa:** Hilo ni jukumu la Islam, hilo ni jukumu la Islam, kujenga kama vile pia wakikristo wakitaka kuendelea kwa u-pastor wanaendelea.

**Com. Ratanya:** Kama ma-seminary hivi.

**Bashir M. Kilalo:** Kwa maoni yangu ilikuwa serikali.

**Com. Salim:** Ni oni lako.

**Com. Kavetsa:** Ni maoni yako.

**Com. Ratanya:** Nina swali?

**Com. Salim:** Swali lingine ngojea.

**Com. Ratanya:** Nina swali lingine hapa mwalimu. Ulisema basic rights kama water – maji safi, katika serikali ambayo tunayo sasa, hata Constitution yenyewe ina mambo ya maji. Sasa hapa hukutuambia unataka improvement gani ifanywe namna gani, kwa Constitution mpya, kwa sababu maji iko, mambo ya maji yako, lakini makosa ni wapi ambao tungerekebisha kwa Katiba hii mpya. Na tena kwa barabara vile vile, kwa stima uliguzia hivi tu ukasema iwe provided, lakini mimi najua hiyo iko, lakini pengine kuna makosa. Na hukusema makosa ni makosa gani. Kwa education umejaribu kuonyesha kwamba kuwe na national schools na hiyo ni improvement kwa sababu pengine Coast hakuna. Hilo ni pendekezo nzuri, kuwe na university na quota system. Lakini hata hiyo ungepanua zaidi yale ambayo hayako. Pengine hakuna free education sasa pengine ungeongeza free education, hiyo ni maoni yako lakini sitaki kuongeza yangu, hiyo nikukuongoza kidogo. Na tena kwa hii pengine imemalizika hii ya post-primary schools za Islamic, hapo umeambiwa hata wa Catholic wana seminary na wengine. Kwa hivyo ninajua hata Islamic wana shule zao, hata Teachers Training College. Mimi, unajua Kamonja College nilikuwa nafundisha waalimu. Kwa hivyo najua kuna Teacher Training Colleges ambazo niza Islamic na kuna zingine za Catholic na dini zingine. Kitu kingine nilikuwa nataka kukuuliza kama kinaendelea kwa sababu niliacha kikiwa huku, ni kwa the joint syllabus. Lakini sasa imekuwa separate, imekuwa separate, imekuwa Islamic syllabus na pengine umesoma hiyo katika Teachers College na kuna Islamic na kuna Christian. Na tena kuna kitu tunaita pastoral program na pastoral care, hiyo umeiona huko kwa college? Kwa hivyo,

sasa inaendelea namna gani, hakuna pastoral programme kwa Islamic ama pastoral care? Kuna syllabus, lakini lazima kuwe na pastoral care na pastoral programme na hiyo ni Islam wenyewe wanatengeneza sio serikali, hiyo sio ya Constitution.

**Com. Kavetsa:** Huyu ni mwalimu, wazazi wakiwa hapa na wanafunzi wakiwa hapa kuna jambo ambalo unafikiri linafaa liwe kwa shule, ndani ya shule, vile wazazi wanaendelea na wanafunzi wanaendelea. Are there any issues which you think are important for these parents and these children?

**Com. Ratanya:** Ambao tumeona haliko kwa Katiba ni kitu ambacho hakiko sasa. Au ndio ungetuambia?

**Com. Kavetsa:** In your position as a professional, tell us.

**Com. Ratanya:** Na maji, unataka maji yawe namna gani kama ni maji ya pipe ile kubwa zaidi au ndogo.

**Bashir M. Kilalo:** Wacha nianze na ile ya maji kwa sababu nilikuwa nimeanza kuiguzia sasa. Umetuambia kwamba kwenye Katiba ya sasa hivi kuna mambo ya maji, lakini utekelezaji haujafanyika. Kwa sababu bado kuna sehemu zingine hazina maji safi, nyingi sana katika Kenya hii. Kwa hivyo, ikiwa Katiba inatuambia tupate maji sote kama basic rights yetu, basi haijatekelezwa na vile vile upande wa mawasiliano haijatekelezwa kama iko. Na marekebisho iwe hapo, maji kama ni yako sasa hivi, mwananchi wa kawaida mwingine hawezi kuyatumia vizuri, kwa sababu ulipaji wa malipo ni mkubwa. Halafu stima ni hivyo hivyo pia, leo ukitaka stima iingie nyumba ile kama ni kupitia hapa, kufika pale ni kivumbi, akina yahe pia hatuwezi kutumia stima ingawaje iko. Kwa hivyo tunaomba serikali iteremshe vile viwango vya malipo yawe chini, angalau mwananchi wa kawaida pia apate kutumia vitu kama hivyo. Nimemaliza.

**Com. Salim:** Bwana Ali K. Mkungu.

**Ali Kassim Mkungu:** Mimi naitwa bwana Ali Kassim Mkungu na kwetu ni hapa Msambweni. Kwanza nitazungumzia elimu, kwenye elimu mapendekezo yangu nasema mfumo wa elimu ubadilishwe ili turudi katika ule mfumo ule wa zamani wa 7-4-2. Kwa sababu inaonekana kuwa mfumo huu tulionao sasa mara nyingi hutoa watu ambao ukomavu wao huwa haujakamilika kikamilifu. Ukifananisha jinzi wanavyofanya shughuli zao, ukiwafaninisha na wale waliotoka na mfumo ule wa zamani, utapata asili mia kubwa ya wale waliotoka na mfumo wa zamani ni watu ambao wajidikaji wao wa shughuli za kila siku ni nzuri kuliko hawa wa 8-4-4. Kwa hivyo, mfumo ule wa 8-4-4 tubadilishe turudi katika mfumo ule wa 7-4-2-3. Kitu chengine ni katika elimu.

**Com. Kavetsa:** You are saying as if it is nothing.

**Ali Kassim Mkungu:** Surely, it's 7-4-2-3.

**Com. Kavetsa:** But you are just saying it as if it doesn't affect your life.

**Com. Salim:** You said 7-4-2-4, what does 4, the last 4 stand for?

**Ali Kassim Mkungu:** No, it's 3.

**Com. Kavetsa:** Secondly, the reason why it was changed to 8-4-4 was so that children can finish standard eight and finish primary school at an older age. Now, you are saying it is not so that someone who will finish standard seven will be more experienced and more mature than someone who finished standard eight?

**Ali Kassim Mkungu:** Yes. Kitu kingine ambacho ningetaka kueleza juu ya elimu ni kwamba, katika mfumo wetu wa elimu, syllabus na course books katika shule huwa zinabadilishwa kila baada ya muda. Hakuna muda maalum ambao tutaweza tuuweke, halafu tujue kuwa tunaweza kubadilisha syllabus yetu hii. Kwa hivyo ninasema, kuwe na muda kama vile wa miaka ishirini, ili tuweze kuangalia ile syllabus na tuweze kubadilisha zile course books, kwa sababu course books ama syllabus huwa inabadilishwa baada ya muda mfupi peke yake.

Kitu cha tatu katika elimu, elimu iwe ya bure na ya lazima, kwa sababu iwapo kutakuwa na mzazi ambaye hakupeleka mtoto shule, kuwe na taratibu ambazo mzazi yule anaweza kupata mashtaka. Kwa sababu mpaka sasa hivi elimu imeambiwa ni ya lazima, lakini ni kama si lazima kwa sababu kuna watoto wengi huwa wanakosa elimu kwa kutoajibika kwa wazazi. Napendekeza kwamba elimu iwe ni ya lazima, ya bure na lazima na iwapo kuna mtoto atakosa elimu, mzazi aweze kuchukulilwa hatua.

**Com. Salim:** Sasa bure kutoka wapi mpaka wapi?

**Ali Kassim Mkungu:** Bure kutoka elimu ya msingi kama ilivyokuwa. Kitu kingine ni kwamba elimu ya dini kama ... (inaudible) kuwa fully ni syllabus ya dini, kwa sababu huwa ni vitu vichache vichache, dini chache ambayo inafundishwa pale. Hivyo basi, kwa sababu tunataka mtoto apate msingi mzuri na awe na moral maturity ya kutosha, tunataka ile elimu ya dini, ile syllabus fully iletwe katika mashule ili mtoto asome dini yake kamalifu shule na asome dunia yake kamalifu shule.

**Com. Kavetsa:** Elimu ya dini kutoka wapi mpaka wapi?

**Ali Kassim Mkungu:** Shule ya msingi hadi ya secondary.

**Com. Ratanya:** Na hii unasema school syllabus ni nini?



**Ali Kassim Mkungu:** Kuna syllabus ya dini ambapo ikiwa kuna waalimu wa chuoni, kule chuoni, huwa kunafundishwa history, kunafundishwa geography, kunafundishwa lugha, kunafundishwa hesabu, kunafundishwa Kurani. Sasa basi syllabus ile ambayo iko kule madrasa ili watoto wapatiwe nafasi ya kuisoma ile kikamilifu, iweze kuletwa katika shule, wakianza kusoma mwanzo, wakitoka wawe ni kama wamesoma madrasa, kuliko ilivyo hivi leo.

**Com. Kavetsa:** Watoto wanasoma madrasa wakati huu. Madrasa, does that syllabus exist in the primary and secondary school?

**Ali Kassim Mkungu:** Ndio.

**Com. Kavetsa:** But they have already gone through it in school?

**Ali Kassim Mkungu:** Not yet, because wanaenda madrasa wakifika umri wa miaka saba, wanatoka madrasa wanakuja wanaletwa shule. Kule madrasa sasa wamekuwa wamekatisha hawaendi, na ikiwa wanakwenda, wanakwenda siku ya jumamosi ama jumapili. Hivi sasa kuna hii remedial teaching ya jumamosi. Kwa hivyo, watoto wanakosa nafasi ya kupata ile full syllabus ya kule madrasa. Sasa ndio wanasoma hii kidogo, kidogo, wanatoka hali ya kuwa wamesoma kweli ile syllabus ya dini, lakini hawakuipata kikamilifu. Lakini ikiletwa katika mashule, wakiwa na umri wa miaka saba, labda kule madrasa alienda mpaka darasa la pili ama la tatu, saa akianza pale kadiri ya anavyokwenda na syllabus hii na hii anaenda nayo vile vile, so that wakati anapomaliza course of study ya standard eight awe na yeye amemaliza ile ya madrasa yuko kimamilifu. Sasa anaendelea nayo katika darasa la nane.

**Com. Kavetsa:** Nijuavyo hii elimu ya dini ni ya maisha, sasa sielewi vipi hiyo school syllabus kwa sababu pia we have ya Christians, ya dini sio school syllabus. Shule hata za geography na historia na vitu vya sayansi unaonja hapa, unaonja hapa, halafu ukienda secondary unajilisha, halafu ukienda university ndio inakuwa full meal. Do you want them to have kids in standard eight?

**Ali Kassim Mkungu:** No.

**Com. Ratanya:** Kitu kingine unajua katika shule kuna curriculum, wewe ni mwalimu?

**Ali Kassim Mkungu:** Nilikuwa mwalimu.

**Com. Ratanya:** Ni ule mfano. Na inafanywa ili watoto wapatiwe msaada. Kwa hivyo, katika shule inafaa kuwe academic na ndio unaona wamegawanya masaa, kuna masaa ya history, kuna masaa ya kiswahili, kuna masaa ya craft, kwa hivyo yale

masaa yametolewa ni academic ni ya kupita mtihani wa National Examination Council. Lakini upande wa dini, tunajua vizuri sana, dini mtoto anaanza huko nyumbani na hiyo tunaita pastoral care, anafunzwa dini yake nyumbani na wazazi na pengine na wazee. Na huko madrasa kama Islamic, hiyo ni separate, out of school, wanafundishwa. Huku kwingine watoto wa Islamic wanafundishwa, lakini wakati wa shule inatajikana wafundishwe ile ya mtihani. Kwa sababu hii in public school sasa ukitaka hiyo yote iwe sasa wale watoto wachache wa Christian utawapatia ile na wahindi, kwa sababu a school like this one is public. Kwa hivyo lazima syllabus itunzwe vizuri na ninasema hivyo kwa sababu nilijihusisha na development ya Kenyan syllabus kwa Government ya Kenya. Hiyo iko namna hiyo, sasa taabu yako iishe, kwa sababu ongea mambo ya academic act ipatikane kwa sasa. Na halafu huko nyumbani wakati wa madrasa wawe free na wasizuiliwe kufunzwa hiyo ndio freedom.

**Ali Kassim Mkungu:** Kamati ya usalama, wananchi washirikishwe kupitia waakilishi wao katika KATA. Kamati zile zinazoangalia usalama wa wananchi. Usalama kwa wananchi, wananchi waruhusiwe kuwe na wale vijana wa mitaani, ambao hushirikiana na watu wa usalama ili kudumisha usalama katika mitaa. Sehemu nyingi kama hizi za kwetu, tuna vijana tunawaita “sungu sungu” kwa jina. Hawa hushirikiana na kuangalia usalama wa wananchi. Vijana kama hawa waweze kupata mafunzo ili waweze kutilia nguvu usalama wa sehemu zile za chini hapa nchini kote.

**Com. Ratanya:** Hao vijana unataka kufanya kama wenzetu Tanzania, wana jeshi la mgambo.

**Ali Kassim Mkungu:** Yes, kama wale ambao huwa wanaangalia usalama vijijini.

**Com. Ratanya:** Jeshi la mgambo katika location. Si ungesema vizuri namna hiyo.

**Ali Kassim Mkungu:** Tunawaita “sungu sungu” huku. Haya huduma – hospitali:” Huduma za afya mimi napendekeza zisiwe ni sehemu chache, lakini zote ziwe bure, kwa sababu hii ni haki ya kimsingi na watu sio wote kuwa wanajiweza kifedha kwa hivyo hudumu hizi ziwe bure na badala yake zile pesa za NHIF, ambazo huwa zinafaidisha wachache wale ambao wana uwezo wa kuenda mahospitali makubwa makubwa, ziweze kutumiwa ili kama hospital maintenance, lakini wananchi huku wapate huduma za bure. Inshallah namaliza ya mwisho. Vile vile kuwe na kamati za mahospitali za wenyeji, wanaoenda kwenye hospitali hizo kusimamia hali ya kazi pale hospitali, kuchunguza kama hospitali zinafanya kazi vizuri. Kwa sababu wakati huu kamati zipo lakini utaangalia utaona mtu aliyechaguliwa ni mtu ambaye hata haendi pale kwa huduma zake, kwa hivyo wachaguliwe watu wale ambao ni wenyeji kabisa na wanaenda katika hospitali zile kwa huduma ili waone yale matatizo yaliyoko pale na wajaribu kutatua. Kwa hayo machache nasema asante.

**Com. Kavetsa:** Hapa tumekuwa na jambo la wenyeji, hapa kuliko mahali pengine tumeenda. Wenyeji, wenyeji, mzaliwa, mzaliwa hasili ni nani huyo?

**Ali Kassim Mkungu:** Mzaliwa hasili ni yule mtu ambaye asilia yake inatoka katika sehemu ile kwa kuzaliwa. Kwa mfano,

ikiwa tutamtafuta nyuma tupate babu wa babu yake awe anatoka sehemu ile, sasa yule ndio tunamuita ni mtu asili wa sehemu ile.

**Com. Kavetsa:** Sasa sema babu au babu wa babu yake.

**Ali Kassim Mkungu:** Babu ni karibu sana itakuwa babu wa babu yake awe ni mtu wa sehemu hiyo.

**Com. Kavetsa:** Sio inauwezekano, watu wengine wanasema sahihi, kazi yetu nikuambia Tume watu walisema hivi, walisema vile. Sisi ni karani tu hatufai kusema chochote.

**Ali Kassim Mkungu:** Tunataka babu wa babu.

**Com. Ratanya:** Kuna kitu kingine hapa. Unajua kuna kamati ambayo inaitwa Hospital's Board, sasa hizo kamati zina taabu gani, unaona taabu gani ambayo iko hapo, ambayo ni lazima turekebishe kwa hii Katiba?

**Ali Kassim Mkungu:** Ndio, taabu zilizoko kwenye kamati hizi, ni kama vile nilivyotaja kwa ufupi hapa. Atachaguliwa mtu ambaye mtu yule kwa kusema kweli yeye mwenyewe haendi pale hospitali ile kuona matatizo yanaotokea pale, yeye hata akiumwa licha yeye mwenyewe, hata mtu wake haendi pale. Lakini kwa mfano mtu amechaguliwa ni mfanyi kazi anakaa Mombasa .... (inaudible).

**Com. Ratanya:** Unapendekeza nini?

**Ali Kassim Mkungu:** Mapendekezo yetu ni kwamba kuchaguliwe kamati ya watu ambao ni wa nyumbani na wanaenda katika hospitali ile, wanajua shida za pale hospitalini.

**Com. Salim:** Na nani atawachagua?

**Ali Kassim Mkungu:** Ni wananchi wa sehemu ile.

**Com. Ratanya:** Wazee wa nyumbani au nani? Chief awachague ama nani?

**Ali Kassim Mkungu:** Wachaguliwe na wazee kwa sababu wazee wanajua tabia ya huyu bwana. Bwana Ali.

**Com. Salim:** Unasemea eneo hili au?

**Ali Kassim Mkungu:** Nasemea nchi nzima, hii ni Katiba.

**Com. Salim:** Hapa Mombasa kuna kamiti kama hii, kama ni ukambani kuna kamiti kama hii, kwa hivyo unawakilisha wapi au eneo gani?

**Ali Kassim Mkungu:** Kwa sababu tunatengeneza Katiba, ambayo ni Katiba mpya inawezekana ikiwa hivyo, kwa sababu wale watu wa Mombasa ile hospitali ndiyo ambayo shida zao kwanza ndio zitaangaliwa. So, ni wale watu wa Mombasa kuchagua.

**Com. Salim:** Watu wa Mombasa watachagua kamiti ya kuchunguza hali ya hospitali.

**Ali Kassim Mkungu:** Tukisema wote wa Mombasa, si kuwa kila mmoja atakwenda achague bwana Commissioner. Kuna wazee, tuseme kamati ya wazee wa mji ama wazee wa ile sehemu, kwa mfano hii location yetu, tuna wazee wachache wachache.

**Com. Kavetsa:** ..... (inaudible).

**Com. Ratanya:** ..... (inaudible) kama upande wa Kenyatta National Hospital na hata .... (inaudible).

**Ali Kassim Mkungu:** Ndio bwana Commissioner, yapo ile mahali kama Nairobi City na kuna watu wengi. Lakini kunako watu ambao wanaishi pale Nairobi kabisa, licha wale wa kwenda kufanya kazi kurudi makwao. Tunao wanafanya kazi kule wanarudi makwao, tunao watu ambao wanajulikana sasa hivi kuwa hawa ni watu wanakaa hapa Nairobi kabisa kabisa.

**Interjections:** (Inaudible).

**Com. Ratanya:** Nairobi hata wahindi wako, wazungu, kila mtu na wote wanakaa na hata wameru kama mimi wako huko. (Laughter).

**Ali Kassim Mkungu:** Anyway, sasa tuchague kamiti ambazo zitachagua watu ambao wanaangalia hii hospitali.

**Com. Salim:** .... (inaudible). Kamiti ichaguliwe.

**Ali Kassim Mkungu:** Hilo lilikuja ni wazo langu, hivi sasa tulitafutie njia ambayo tutaweza kuli-frame katika hali ambayo tutapata kamiti hizo ambazo zitasimamia zile hospitali, watu ambao ni watu wanaenda kwa hiyo hospitali wanaona yale matatizo.

*Interjections: (Inaudible).*

**Ali Kassim Mkungu:** Bwana Idha tunazungumzia hospitali za umma, za serikali kwa sababu hapa kwanza tumesema tupate free hospital services, halafu huduma zile ziangaliwe.

**Com. Salim:** Pendekezo lingine ambalo limetolewa hapo awali ni la inspectors, kama private schools tuwe na inspectors, hospitali pia ziwe na inspectors. Hapo mtu ataweza kuchaguliwa kwa uzuri wake, bora utoe pendekezo kama hili. Nafikiri umuhimu wa kuwa na tamaa ni kuhakikisha kwamba hospitali kwendelea vizuri.

**Com. Ratanya:** Hebu hapo nijaribu kueleza hapo kidogo, kwa sababu hata wewe pengine ulipendekeza majimbo, pengine kama hii itapatikana katika commission kama ya Coast, hiyo board ama hiyo committee itachaguliwa na regional government kama hiyo kamiti ya hospitali itakuwa nzuri?

**Ali Kassim Mkungu:** Hapo kwanza nitasema serikali tunayohitaji ni ya majimbo, na ikiwa hiyo ikichaguliwa itakuwa ni sawa sawa tumeridhika.

**Com. Ratanya:** Na tena twende kwa national level. Kama Central Government ile itakuwa na President, Vice President na wengine nao wakichagua kamiti ya Kenyatta National Hospital unaona kama itakuwa ni sawa sawa, badala ya wazee wakae ... (inaudible) Kenyatta National Hospital.

**Ali Kassim Mkungu:** Itakuwa ni sawa sawa, lakini for consideration ama criteria they should use ni kwamba waangalie mtu ambaye ana fursa ama ana nafasi ya kuukua matumizi yake katika hospitali ile.

**Com. Ratanya:** Wataangalia watu kama watakuja hapa katika hii village. Wazee wenu hapa wa kienyeji, Kaya wakichagua board wateuliwe watoto wao hapa wale wanaweza kufanya kazi, sijui kama unanielewa. Nao wakichagua kamiti ya hospitali hapa hiyo itakuwa ni sawa sawa. Hospitali yenu hapa, wazee wawachague.

**Com. Kavetsa:** Unaweza kuandika Memorandum zaidi. Fikiria halafu uandike Memorandum zaidi vile inaweza kuwa kwa kila kiwango.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Ratanya:** Na ikiwezekana hiyo mambo yako yawe hapa kusaidia watu wa hapa.

**Com. Kavetsa:** Sijui unasema kamati ya wazee, sijui hao wazee kina mama wako hapo ndani, na kina mama ndio

wanashughulika na hospitali.

**Ali Kassim Mkungu:** Ndio kina mama wawe ndani.

**Com. Ratanya:** Kina mama wawe katika ile group ya wazee inaitwa “Kaya”.

**Ali Kassim Mkungu:** Ile group ya wazee inaitwa “Kaya” mara nyingi kina mama hawako.

**Com. Ratanya:** Lakini kuna mara ambao wakina mama wako?

**Ali Kassim Mkungu:** Ikibidi huwa wanashirikishwa, ikibidi.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo hawakataliwi kabisa. Kuna Memorandum?

**Com. Kavetsa:** Hiyo ni maoni mazuri uandike pale.

**Com. Salim:** Bwana Salim Kitwana.

**Salim Kitwana:** Jina langu ni Salim Kitwana na nina mapendekezo yafuatayo kuchangia katika Katiba. Upande wa serikali napendekeza tuwe na serikali ya majimbo, na kuwe na Rais ambaye ni ceremonial na Rais yule awe si mbunge na awe amechaguliwa na kura za wananchi. Na kuwe na waziri mkuu vile vile ambaye atakuwa amechaguliwa na chama chenye kutawala. Na vile vile kuwe na vice president ambaye atakuwa amechaguliwa na wabunge. Na majimbo yale, ningependekeza yawe yamepewa uhuru wa kujisimamia sana kimaswala ya kiuchumi. Fedha zote ambazo zitakuwa zimepatikana katika jimbo, ziwe ni zenye kunufaisha lile jimbo, labda kuwe na asili mia kumi tu peke yake, iende katika serikali kuu.

**Com. Kavetsa:** Wengine hata wanakuja na meli, wamekatakata nchi hii yote kwa majimbo, pengine si provinces. Kile kinachonishangaza ni kwa sababu wale watu ambao mnataka wamevamia sehemu yenu ya nchi, wanataka wandelee hivyo hivyo na nyinyi wenyewe mnaimba tu ni majimbo. Wengine wanasema hii majimbo inafaa ikae au serikali ya KANU ikiweko inafaa ikae na watu wamekatakata, Coast Province iko pamoja na North Eastern. Hii si mambo ya kusema siasa nini, na hiyo ndiyo itaangaliwa nani alisema hiyo, nani alisema majimbo. Kuna waalimu hapa wa economics watu ambao nawajua. Tafadhali majimbo ni mambo ambayo yatabadilisha Kenya, lakini mkiyachukua kidogo ni mambo ya siasa. Mambo ya Constitution majimbo itakuwa provinces. Na vile mko pamoja na North Eastern.

**Salim Kitwana:** Tumeyapata vizuri sana. Basi si mapendeleo yangu mimi, nasema kila province iweze kuwa jimbo la kivyake.

**Com. Salim:** Utawala wake uwe namna gani? Hilo jimbo litaitwa aje na mwenye kuongoza jimbo hilo ataitwa nani?

**Salim Kitwana:** Ataitwa Governor mkuu wa jimbo.

**Com. Kavetsa:** Na atakuwa na mamlaka gani ukilinganisha na Rais?

**Salim Kitwana:** Atachaguliwa na wananchi kwa njia ya kura.

**Com. Ratanya:** Atakuwa anafanya kazi yake ama atakuwa tu Nairobi?

**Salim Kitwana:** Kutakuwa na serikali ya chini pia, kutakuwa na chamber mbili, chamber moja ni ya serikali kuu kule, na chamber nyingine ni ya serikali ya jimbo. Tutaliita jimbo.

**Com. Salim:** Mtaliita aje?

**Salim Kitwana:** Tutaliita jimbo.

**Com. Salim:** .... (inaudible).

**Salim Kitwana:** Tutaliita Regional Parliament.

*Interjections: (Inaudible).*

**Salim Kitwana:** Ama jina nzuri tuliite Regional Assembly.

**Com. Salim:** Jimbo hilo litaendeshwa aje?

**Salim Kitwana:** Kwa hivyo tunasema katika kila jimbo, kila wilaya iweze kuwa na waakilishi watano wenye kukalia katika kikao cha jimbo lile.

**Com. Kavetsa:** .... (inaudible).

**Salim Kitwana:** Kila wilaya katika jimbo liweze kuchangia waakilishi watano, wakalie ile bunge ya pale kwenye lile jimbo.

*Interjections: (Inaudible).*

**Salim Kitwana:** Hapana ya parliament watakuwa wamechaguliwa kando na wale walio katika serikali ya lile jimbo.

**Interjections:** *(Inaudible)*.

**Salim Kitwana:** Katika jimbo la Region.

Elimu, napendekeza kuwe na at least university moja katika kila jimbo, kwa uchache. Na elimu ile iwe ni bure na ya lazima, ili kila mwananchi aweze kupata ile elimu, kwa sababu sasa hivi watoto wengi ni ma street boys, kwa sababu wazazi wao hawawezi ku-afford cost ya education. Kwa hivyo iwe bure kuanzia class ya kwanza mpaka form two, na kuanzia form three kuendelea, iwe mtu analipa, na ambaye mtu hawezi kulipa serikali imsimamie. Na akifanya vizuri katika mtihani, serikali impe kazi ili iweze kum-charge zile pesa ambazo ilimsomesha.

Kitu kingine ni maswala ya uchaguzi.

**Com. Kavetsa:** Umetwambia shule ziwe free na iwe kwa kila jimbo.

**Salim Kitwana:** Ndio.

**Com. Kavetsa:** Nani atasimamia university ambayo itakuwa kwa jimbo?

**Salim Kitwana:** Jimbo lenyewe.

**Com. Kavetsa:** .... (inaudible). Nauliza swali, I am not challenging you, I am just asking you.

**Salim Kitwana:** Lazima iwekwe university ya national kwa sababu ni nchi moja yote, ingawaje ni majimbo lakini ni nchi moja. Kwa hivyo kuna universities ambazo ni lazima kwa kila jimbo, halafu kuna university ambazo ni za nchi.

**Com. Ratanya:** Hii ya jimbo in National University, lakini lina watoto kutoka kila pahali?

**Salim Kitwana:** Hapana ina watoto wa kutoka lile jimbo, ile ya national ndiyo itakuwa inachangia watoto kutoka sehemu tofauti tofauti. Ili watoto wa kila jimbo wapate nafasi ya kuingia university, kwa sababu sasa hivi majimbo mengine kielimu, hawapati nafasi ya kuingia university.

**Com. Ratanya:** Lakini university ya hapa ya regional hamtaki wengine waiingie kwa hiyo. Also kama Coast university.



**Salim Kitwana:** Waingie watu wa lile jimbo, ile ya nchi ndiyo wataingia mchanganyiko.

**Com. Kavetsa:** Okay wach tuendelee sasa, unaweza kupitisha kwa maandishi baadaye.

**Salim Kitwana:** Sawa, ni hali ya kodi iondolewe kwa vyakula, ili viwe rahisi kila mwananchi aweze kupata chakula kwa bei ambayo anaiweza. Kwa maana sasa hivi si watu wote wanaweza kumiliki kununua chakula mara tatu kwa siku. Kuhusu upande wa kura, kura zihesabiwe kwenye vituo, na madaba yale ya kura yawe yako transparent. Kitu chengine, Katiba wakati labda kuna pendekezo linataka kutolewa liwe linarudishwa kwa raia wenyewe, lisiwe kama saa hivi ambayo linabadilishwa na kura za wabunge asili mia tisini na tano, wanajipandishia mishahara kule.

**Com. Kavetsa:** Umesema mambo ya Katiba, halafu umesema mambo ya mishahara ya wabunge. Ungefaa ujue haya mambo ya Katiba, Katiba ikiwa ibadilishwe lazima ibadilishwe na nani?

**Salim Kitwana:** Na wananchi wenyewe. Nimetoa mfano.

**Com. Salim:** Una maneno unayo kuhusu bunge?

**Salim Kitwana:** Nimetoa mfano nikasema sasa hivi Katiba tuliyonayo wanasema ikipitishwa asili mia tisini na tano kule, wanaweza kubadilisha vifungu fulani. Sasa kwa sababu ni wao ndio wanaopitisha kule, wanapitisha maswala ya mishahara yao.

**Com. Ratanya:** Sasa ungependekeza nini?

**Salim Kitwana:** Napendekeza tukitaka kufanya mabadiliko ya Katiba iletwe kwa wananchi wenyewe.

**Com. Ratanya:** Kwa njia gani?

**Salim Kitwana:** Kwa njia ile ambayo watakuwa wamesema kule bungeni wanasema tu, lakini hawapitishi. Inakuja huku, inakaliwa na wananchi wenyewe.

**Com. Salim:** Kama kikao kama hiki.

**Salim Kitwana:** Ndio.

**Com. Salim:** Kitachukua muda wa kila wakati ama?

**Salim Kitwana:** Hapana mabadiliko, kama wanataka kufanya mabadiliko.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Ratanya:** Maoni ya wananchi ni referendum, kwa mambo ya National Conference ama tuweke round.

**Salim Kitwana:** Ifanyiwe referendum.

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Ratanya:** Kuweka ndani hapo.

**Salim Kitwana:** Ndio, si mbaya kunikumbusha.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo National Referendum.

**Salim Kitwana:** Ndio. Na Katibu iweze kulindwa, kuwe na ofisi au wizara ya Katiba. Kitu kingine – Civic Education, iendelee katika mashule, ili kila mwananchi aishi akijua haki zake ni nini katika hii nchi. Swala lingine ni swala la ardhi.

**Com. Kavetsa/Com. Salim:** Sasa maliza.

**Salim Kitwana:** Oh, namaliza basi. Kumalizia nasema kwa kuwa tumepata uhuru miaka mingi iliyopita, mambo ya kuwa kila siku wanapiga firimbi wakishukisha bendera, watu wote wanasimama, ile inaonyesha ukoloni ndani yake. Kwa hivyo iwe bendera haisimamiwi kila siku.

**Com. Ratanya:** Umesema ya mwisho ni juu ya mashamba.

**Salim Kitwana:** Mumeniambia nimalize. Hiyo ya ardhi kama mnaitaka pia nitaita.

**Com. Kavetsa:** Excuse me kuna nchi zingine ambazo hazina ukoloni na wana uhuru, wanashukisha bendera yao kwa .... (inaudible). Sasa tufanye aje .... (inaudible).

**Com. Ratanya:** Kwa ardhi umesema kitu?

**Salim Kitwana:** Ardhi iwe ya indigenous people wawe ndio wenye haki ya kumiliki ardhi. Isiwe kama sasa hivi inagawanywa kama zawadi huko maofisini.

**Com. Kavetsa:** Ni wakina nani?

**Salim Kitwana:** Wale wenyeji wale ambao wameambiwa babu zao wamezaliwa katika hilo eneo.

**Com. Ratanya:** Babu au babu?

**Salim Kitwana:** Babu ya babu ndio.

**Com. Ratanya:** Asante sana.

**Com. Salim:** Mwanatumu, Mwanatumu, Mwanatumu yuko? Haya, karibu.

**Speaker from audience:** Namsema mwenzangu.

**Com. Salim:** Atakayesema yeye ni nani?

**Com. Salim:** Aitwaje?

**Speaker from audience:** Chandama.

**Com. Salim:** Amejandikisha yeye hapa.

**Speaker:** Ndio amejandikisha.

**Com. Salim:** Aitwa?

**Interjections:** *Chandama.*

**Com. Salim:** Mbona simuoni hapa. Unahakika amejandikisha?

**Interjections:** *Ndio.*

**Com. Kavetsa:** Call someone else and check while they are presenting.

**Com. Salim:** But you know we haven't had a .... (inaudible). Basi tuwache tutaendelea mbele. Kassim A. Machonne, yuko?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Miaka ishirini na nne Commissioners bado tulipokuwa shule exam ikikaribia tulikuwa twa study, mpaka nikajua nasoma kiliolio yote na .... (inaudible). Sasa point zetu zitaonekana kama niza kurudia lakini hali ni kwamba lengo ni moja na tunapigania kwa jambo moja. Kwa majina mimi naitwa Kassim Abdalla Juma, lakini umaarufu wangu ni Kassim Machonne. Natoka kisiwa cha Wasini huko ambao ndio mwisho wa Republic ya Kenya. Pale ndiyo mwisho kabisa wa Republic ya Kenya. Kwa hivyo kwanza katika kwenda haraka haraka, sababu Tume imechaguliwa mimi pendekezo langu nasema, muongezwa muda kwa vile mushajitolea kwa jambo la ukarabati wa hii sheria, basi musitupeleke katika kura kabla hamjakarabati ile sheria, kama si yote lakini hususani na ile inahusu na mambo ya uchaguzi.

Pendekezo langu lingine ni kuhusu mambo ya majimbo. Hata mimi naungana na wote wale walioanza kusema kwamba tungependa serikali ya majimbo, na serikali hii ya majimbo tulikuwa tunasema itakuwa na assembly mbili, Regional Assembly na National Assembly. Kule kwa Regional Assembly tungependekeza labda kutoke wajumbe wa tatu na kwa National achaguliwe mjumbe mmoja ambaye atakwenda Nairobi, akiwa anapata ushauri kwa hawa Regional Assembly or representatives wa kimsaidia na mawazo ya kwenda kupendekeza kule kwa taifa. Serikali hii iliyoko imetupatia uhuru wa kuabudu, lakini tunapendekeza serikali ijao kuwe na uhuru wa dini. Tofauti hiyo ni kwamba, uhuru wa dini yale mengi yaliyokuwa napiganiwa na hawa wasemaji wengine wamesema kama vile mambo ya "eda", mambo ya "ijabu" tukiwa na uhuru wa dini, tutaweza kufuata Islamic sheria. Tukiwa tumepata Islamic sheria hayo mambo yote haitahitajiwa kutajwa moja kwa moja yamo ndani humo yameelewa vilivyo kwa karne kumi na nne sasa. Kwa hivyo upande wa elimu, tunasema au mimi nashauri Tume mapendekezo ya watu wengine kwamba iwe quota system. Lakini hapa kwenye quota system kuna ujanja au ujanja fulani, kuna watu wanatoka kule shule ambazo labda wanasoma vizuri, wakati hii ni kesi nimeona sishtaki headmaster hapa, lakini wakaja kujiandikisha katika ule mtihani wa kidato cha nane katika mashule yetu haya ambayo yana udhaifu fulani wa masomo. Kwa hivyo unapata hata mtoto wa darasa la saba anaweza akashindana na hawa watoto wetu wa darasa la nane na akawashinda. Kwa hivyo ikija kuchaguliwa ameiba ile nafasi ya mtu wa Pwani au Msambweni ili hali yeye ametoka Nairobi and I have a test case here. Mtoto aliyetolewa State House School akaja aka-register huku kwetu mashambani, akashinda wale watoto wa standard eight by far, 200 marks. Kwa hivyo, unaona kama nafasi yetu hapo iliibiwa. Kwa hivyo, ujanja kama huo unafanyika hata kwa zile nafasi za University, ijapo tunasema tunataka B-, lakini B- ile inachukuliwa na Onyango au Njuguna. Kwa hiyo, tunapendekeza waalimu wakuu, wawe ni wazalendo ni wapenda Regional zao. Wasikubali kufanya mambo kama haya na ikiwa ni mtu yule amekuja kutuibia nafasi yetu, asiruhusiwe. Na kama vile kiti kitakuwa na mchango zaidi, mtu kama huyo hawezi kumshtaki mwalimu ambaye anatabia kama hiyo.

**Com. Ratanya:** Katiba itasaidia namna gani ama unataka msaidiwe namna gani, juu ya hawa waalimu?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Hiyo ni hatia kwa hivyo, Katiba izuie kusiwe na mtu kutoka shule nyingine, lazima iwe systematical uonyeshe umeanza standard one mpaka kufikia class ya nane. Ama ikiwa ni nafasi zile za kwenda University, umeanza form one hapa mpaka form four. Si uje uanzie form four halafu uchukuliwe wewe kama ile quota ya eneo lile. Kwa hivyo Katiba iseme iwe systematically.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim A. Juma (Machonne):** Mimi naweza kusema hizo ni exceptional cases labda zitakuwa moja mpaka tatu, lakini vile hali ilivyo sasa ni nyingi sana. Watu wamejua kwamba shule zetu huku zina udhaifu wa masomo, standard yake iko chini. Kwa hivyo, ni wengi lakini katika exceptional case kama hiyo inaeleweka. Lakini pia katika hiyo serikali ya majimbo, jambo kama hilo halitokea kwa sababu tunasema ajira ya makampuni ya binafsi, ama ajira ya utawala yaani Government, iwe localised iwe ni ya watu hapa. Kwa hivyo mambo ya transfer hayo pia yataenda yapotee. Sasa swali kama hilo halitokea, katika mapendekezo yangu ya ajira nilikuwa nimesema kwamba, iwe ya utawala ama iwe ya watu kibinafsi, iwe ya wenyewe wenyeji, watu wa hapa hapa. Kwa hivyo mambo ya transfer yatakuwa raisi na pia itakuwa gharama chache kwa serikali, kwa sababu ya zile allowances watu wanaopata katika transfer. Unless na mpaka iwe, mtu yule ambaye ataandikwa kutoka sehemu nyingine awe na special talent, ambayo talent hiyo imekosekana katika eneo ambalo yule anaandikwa kazi, iwe ni labda engineer ana ana ujuzi fulani pengine sijui wa computer ndio imuruhusu, otherwise isiwezekane. Wakati tuko kwenye mambo ya elimu, tunasema hii Civic Education, elimu ya uraia iwe ni compulsory ki-maskuli na vile vyombo vya dola, yaani kama hizi ma-redio na television vitenge katika wiki siku moja au mbili, air-time ambayo itatumika kwa civic education. Kwa wale, kama sisi ambao tumemaliza nafasi ya kusoma, lakini tupate nafasi ya kujifunza haki zetu za uraia. Iwe hiyo, na hiyo air-time itakuwa ikilipiwa na serikali. Tukija katika upande wa elimu, iwe ni ya lazima na ya bure kuanzia shule za vidudu mpaka form four.

**Com. Ratanya:** Shule za vidudu ni gani?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Vidudu ni kindergarten mpaka form four. Hili Swahili sanifu nafikiri wamewaita vidudu.

**Com. Kavetsa:** Watoto wanakubali, kwa sababu wanahaki zao?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Na hapo hapo pia kuna sheria mpya ambayo ilianza mwezi wa April mwaka jana, kwamba ni haki mtoto asomeshe, lakini sijaipitia sana lakini nadhani sheria hiyo haitambui elimu ya dini. Kwa hivyo napendekeza kwamba katika haki hiyo ya mtoto kuweza kushtaki mzazi wake kwa kutomsomesha, iwe ni kwa elimu yoyote. Akiwa anasomesha dini pia, hiyo pia ni masomo, awe hana ile haki ya kuweza kumshtaki, kwa sababu hakumpeleka shule. Iwe hata elimu ya dini pia imetosheleza haki hiyo.

**Com. Ratanya:** Umesema mpaka secondary ama University?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Secondary, yaani form four – “O” levels zamani tunaiita. Hapo ni compulsory serikali lazima iangalie. University si wote watafika.

Electoral Commission: Wale ma-Commissioners ihusishe wote wale waohusika, yaani vyama vyote isiwe kuwa wanachaguliwa tu na chama tawala, wale watu wao wapenda ama watakao wapendekeza.

**Com. Kavetsa:** Lakini hiyo iko kwa IPPG.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Iko kimaandishi lakini haitendeki.

**Com. Kavetsa:** Kuna watu wa Ford Kenya, kuna watu wa DP, kuna watu wa KANU, kuna watu wa SDP.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Kama imetendeka ni sawa, lakini mimi natilia mikakati kwamba iwe hivyo. Na uandikishaji wa kura uwe a continuous process, sio wakati wa kura tu peke yake. Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba sasa hivi waandikishaji wa kura baada mtu tu kupata kitambulisho naye pia apate kura yake, hata kama ni baada tu ya kura. Na kura zihesabiwe vituoni, pale pale zinazopigwa. Wale ma-agents wa wagombea uchaguzi wapewe karatasi peke yake sasa yule madebe yakija yakiletwa kwa ndege ama kwa landrover lakini kuenda pale center ambapo kura zote zitakusanyika, iwe kila mgombea agent wake ameshajua ni kura ngapi alipata kutoka hapo. Mimi mapendekezo yangu ni kwamba Rais asiwe na constituency, ili asifanye mapendeleo, awe atagombea na akikosa akae nje. Ningependekeza kuwa pesa ya nchi isitengenezwe kwa sura ya Rais yeyote, isipokuwa labda wale ma-Rais waliopita kwa sababu ya kuwa ibaki kama ni kumbu kumbu. Lakini inapotengenezwa kwa sura ya Rais aliyepo, ikija kwa kura anakuwa na hiyo advantage.

Na kura aina yeyote itakayoendelea iwe ni kura ya siri. Napendekeza iwe ni kura ya siri hatupendekezi kura ya waziwazi kama mlolongo, kwa sababu chuki zake zinabakia siku nyingi. Na kuwe pia na Tume ambayo itapendekeza kuwa hii ni Tume ya kienyeji, ya wazee ambayo itapendekeza wagombea kura hasa wa councilor na wabunge. Kwa sababu huenda wakora wakajitokeza na kwa sababu ya uwezo, wakadanganya watu na wakachaguliwa. Lakini Tume kama hii litachagua watu wenye nidhamu.

**Com. Salim:** Tume hii itakuwa ya nchi, location au vipi?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Kila constituency, na kila location. Tume kama ya watu kumi na mbili katika location ambayo ndiyo itapendekeza wale wagombea kura wote, ma-councillor wakae mbele yao, wajieleza sera zao, halafu waondoke, Tume ile itasema tumepitia zile sera na uchaguzi wetu umedanganya. Kwa hivyo, hata kama nyote muwaovu lakini

yule kidogo ana afadhali, yule peke yake ndio aruhusiwe kupigania u-councillor wa sehemu hiyo na kwa mbunge hivyo hivyo.

**Com. Ratanya:** ..... (inaudible).

**Kassim A. Juma (Machonne):** Nasema wawaakilishi kama kumi na mbili kwa location na waakilishi watatu kutoka kila location, ambao watakuwa wanakaa kwa tarafa ili kumchagua mbunge. Kila location itoe watu watatu ambao watakuwa katika Tume ya kuchagua au kuchunguza sera ya mbunge, kabla hatujachagua wakora.

**Com. Salim:** Na hawa waakilishi watachaguliwa na nani?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Waakilishi hawa watakuwa ni katika wale kumi na mbili.

**Com. Salim:** Na watachaguliwa na nani hawa?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Watachaguliwa na wazee wa kijiji.

**Com. Kavetsa:** Akina mama wakiwa ndani?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Tuko gender sensitive.

*Laughter:*

**Com. Ratanya:** Hawa wazee pengine ndio “Kaya”.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Hapana, kwa maana ya ndani “Kaya” ni kitu kingine na vijiji ni kingine. Kaya ni sehemu kidogo tofauti na vijiji. Vile vijiji vikubwa za kila location, at least zitoe mtu mmoja wa kila location wawe kumi na mbili katika tarafa.

**Interjections:** (Inaudible).

**Kassim A. Juma (Machonne):** Ndio wako tayari wazee wa kijiji na kuna wazee wengine wa heshima, ijapo hawajateuana, ni maoni ya wale kumi na mbili pia wanaweza kuwapendekeza kama opinion leaders, wakawasaidia katika mchango huo.

Katika uchaguzi wa Rais, tunasema makamu wa Rais awe niwakitoka, sasa tuko multi-party, kile chama chenye viti vingi zaidi, ndiyo achaguliwe makamu wa Rais. Pia tukiwa katika majambo ya kura, napendekeza kwamba ..... (interjection).

**Com. Salim:** Makamu wa Rais atachaguliwa kutoka chama gani?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Atachaguliwa katika kile chama ambacho kina viti vingi zaidi bungeni. Na pia, napendekeza kwamba punde tu bunge linapovunjwa mawaziri wote wawe hawana kazi, kwa sababu katika tugombania kura kipindi kinachofuatia, wakiwa bado ni mawaziri wana zile ‘undue’ advantages. Kwa hivyo vyeo vyao au ofisi zao zimalizike tu baada ya kuchaguliwa na wale ma Permanent Secretaries, ndio washikilie zile nafasi zao kama kuna maswali yoyote ma-Permanent Secretaries katika wizara hizo ndio waweze kujibu maswala hayo, lakini wao wawe hawako kazini kama mwingine yeyote.

**Com. Ratanya:** Na President na Vice President?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Wote hali ile ile, kwa sababu hao hata ndio wako na undue advantages zaidi hata kushinda hawa mawaziri. Kwa hivyo, pale ofisi zote zinabaki, AG na Auditor-General, Permanent Secretaries, hawa ndio wataendelea ile serikali ya muda kabla ya uchaguzi na Bunge lingine kuchaguliwa.

Katika hali ya uchumi, napendekeza serikali ijao ihifadhi uchumi kwa raia peke yake, kwa sababu sasa hivi kuna utatanishi hapo. Unaweza ukasema sheria iko hivi, lakini sivyo. Nitatoa mfano, kule kwetu Shimoni, tuko mpakani, ni wasembo wanaingia, wanaleta karafuu, wanaleta mambo ingine, wanauza wenyewe, wanakwenda Mombasa wanabadilisha sijui pesa za kigeni, wananunua mali mitambo-ini wenyewe, wanakuja pale Shimoni hawahitaji clearing au forwarding agents, wanasafirisha wenyewe, kutumia njia za ufisadi, labda ikiwa sheria ipo haitiliwi mkazo sana, kwa hivyo tunapendekeza sheria kama hiyo itiliwe mkazo sana, kwamba biashara au uchumi lazima ufanywe na wenyeji wenyewe na basi ikizidi mgeni afanye atajiandikisha na lazima afanye na mwenyeji fulani hapo, kuwe na hii co-operation of partnership na mwenyeji. Na kama kuna mgeni ambaye ana utajiri fulani mpaka amekubaliwa kwamba aweke mtambo, basi mtambo ule lazima uwe na asili mia arobaini ya share zake zipewe kwa wananchi. Labda kwa tofauti ya dini, kama ameweka mtambo wa bia, na pale kuna waislamu, hatutaki. Kwa hivyo, katika mitambo yote itakayoruhusiwa na serikali kuwekwa hapa na ni foreign investment, sio lazima mitambo hata kama ni service industry, kama vile ma-hoteli, air transport, lazima kuwe na asili mia arobaini share, wananchi waruhusiwe kununua share katika ile. Pia, masoko yaani marketing, serikali iwe na sijui utaita Tume, lakini iwe na mfuko maalum ya kusimamia, iwe na jukumu la kusimamia Tume ya kusimamia uuzaji. Itoe pesa na itoe technical know-how ya kuweza kutafuta soko la kila mazao, kwa sababu mbeleni tumeona serikali ilipotoa nguvu hizo ikachukua zote peke yake, kumekuwa na matatizo kama vile mipango ya majani na chai. Lakini mimi napendekeza itoe mfuko, yaani funds na itoe technical know-how pengine manpower, lakini wenye kutafutiwa halafu uuzaji urudi kwao wenyewe. Maanake ikirudi serikali tena kutakuwa na ukandamizaji, na matatizo kama yale yametokea katika sekta ya kahawa na nini yasirudiwe na hatutaki kuyaona tena.

Upande wa ardhi, ninavyofahamu mimi kuna ardhi ya aina tatu katika Kenya. Moja ni private, kuna crown au state land na kuna trust land. Ile ya private sina la kusema imefungwa, kila moja anajua taratibu zake, lakini uonevu mkubwa unakuja hapa



katika crown – state land au trust land. Commissioner asiruhusiwe tena kusimamia ardhi hizi, najua hivyo katika Katiba wanasema baraza lisimamiwe, lakini hiyo inabaki katika maandishi. Baraza halina hiari yoyote, bado linategemea Commissioner. Commissioner anaweza kumpa zawadi yule anayepiga kofi nyingi sana za Nyayo, na atakayefanya jambo lolote lile ambao anaona linampendeza, mambo kama haya yasitokee. Kwa hivyo, ardhi isimamiwe na baraza kupitia wenyeji. Nasikia nitaulizwa swali la wenyeji, wenyeji ni watu ambao wamekuwa hapo kutoka 1898, hii ni u-karne moja kutoka elfu moja elfu moja na mbili, kwa vile tunaenda Katiba mpya. Tunataka karne, hawa ndio wenyeji. Wenyeji ni wale walikuwa pale 1898, one century from today.

**Com. Ratanya:** Wako na kamati yao?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Kamati yao la kupitia baraza. Baraza, lile serikali la mitaa – county council. Sasa ile serikali ya mitaa, waakilishi wake na hili baraza la wenyeji ndio litakotoa, sio Commissioner wala sio President. Hatutaki tena mambo hayo.

Na mali ya asili inapotokea bahati, sehemu fulani ikawa na mali ya asili, au mara ingine sio mali lakini environment kama vile pango, ama fall, kama vile unasikia Ripon Falls kule kwetu tunahii marine park ambayo iko Kisiti marine, inapo sehemu fulani kupata bahata kama hiyo. Lazima ukusanyaji ama ile faida inayopatikana kutokana na bahati hiyo, asili mia hamsini itumike kwa faida ama kwa maendeleo, kwa mipangilio ya wenyeji wa sehemu hiyo. Kama mfano tumesema marine park kule Shimoni, Tiu mines hapa Nguluku na Maumba, hotels na jambo lolote ambalo unaweza kusema ni bahati ya Mwenyezi Mungu au sijui maumbile fulani limewakumba ama limetokelea kwa watu fulani, basi wapate asili mia hamsini ya faida hiyo, kwa maadili yao.

**Com. Salim:** Sasa maliza haraka.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Haya naenda haraka haraka ndio nimesema ime evaporate kwa sababu mambo ni mengi, mengine tunaacha, mengine tunaruka. Juzi juzi kulikuwa na seminar ya amani, katika agenda moja ya hiyo amani, ilikuwa ni tuwe na amani na vyumbe vingine. Lakini amani hii nafikiri wale vyumbe wengine wamefikiriwa zaidi kuliko vyumbe wanadamu. Mfano ni kwamba kule Shimoni kuna sehemu ambayo ndugu zetu wa kibara walikuja wakalima na tukawa tumefaidika sana anaitwa Mwazaro. Lakini manyani sijui nikwa vile ilikuwa yanaenda njaa sasa kukapatikana chakula, yalizaana mpaka ukulima sehemu hiyo wameshinda. Tayari tomato, kitunguu, maembe ilikuwa ni raisi sana lakini manyani yalivyokuja yaliharibu. Na hapo ni karibu na ofisi kuu ya headquarters ya KWS. Sasa ukiliua tu nyani, habari kwa njia ya kienyeji au nyingine zinafika kule na unakuja kutafutwa. Sasa wananchi waka surrender kwa manyani. Nafikiria hapa kuna ukandamizaji, lazima sheria iwepo, ya ajabu kweli tuna hiyo msawa unayoendelea wa amani, kuna vyumba vingine lakini sheria iwepo, ya kwamba mwanadamu awe na nafasi kubwa zaidi kuliko wa vyumbe vingine. Nafikiri nitakomea hapo kwa vile nikijilazimisha nita kosa.

**Com. Kavetsa:** Swali moja.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Ndio madam.

**Com. Kavetsa:** Upande wa Rais atachaguliwa vipi?

**Kassim A. Juma (Machonne):** Rais atachaguliwa kwa kura nchi nzima, kama vile ambavyo anachaguliwa hivi sasa. Lakini awe ni mgombea wa kiti cha urais peke yake.

**Com. Kavetsa:** Okay. Wengine wanasema iwe ni asili mia ya 25% itolewe kwa kila province, iwe 51%.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Ndio na mimi pia katika huo msemu wangu niko hapa, halafu anasema atachaguliwa nchi nzima. Yule atakayeshinda kwa wingi wa kura ndiye awe Rais na yule anayemfuatilia ndiye awe makamu wake.

**Com. Kavetsa:** Serikali ya mseto yaani coalition government.

**Kassim A. Juma (Machonne):** Ndio iwe ya mseto.

**Com. Salim:** Ndolo kata Ndolo.

*Interjections: Ashatoa? Sawa.*

**Com. Salim:** Ali Mwanzani. Hayuko. Amadi R. Kisero, hayuko. Stella Mumbi, hayuko. Alfan Kemo, hayuko. Omari Mwacharo, hayuko. Mohamed Jumadari, yuko. Sasa tuambie Mohamed Jumadari yuko? Huyu ni Omari Mwacharo, ameondoka. Sasa tutamuita huyu aliye hapa Omari Mwacharo, yuko au hayuko, hayuko? Mohamed Jumadari.

**Com. Kavetsa:** Highlight just the main points.

**Mohamed Salim Jumadari:** Kwa jina naitwa Mohamed Salim Jumadari ni mkaazi wa Msambweni. Kulingana na kazi iliyoko mbele yetu saa hizi, kwa ufupi ningependelea kwanza kurudi nyuma ki historia kwa kuangalia Katiba ile ya zamani kidogo kwa mukhtasari na ufupi. Nafikiri wengi mtakubaliana na mimi kwamba.

**Com. Kavetsa:** Unazungumza kwa Tume, sio kwa raia. Address the Commission.

**Mohamed Salim Jumadari:** Nafikiri tunakubaliana sote kwamba wakati wa nyuma tulikuwa na vita vya ukombozi na malengo yake yako kwa Katiba ile iliyopita na sote tuna amini kwamba vitu vingi hivi tunavyoongea hapa viko kule. Kama

mfano tulikuwa tunapigania haki ya kurudisha heshima ya wakenya, na heshima kuirudisha ni kujenga uchumi, ili kupinguza umaskini, afya bora, elimu bora na ardhi. Hayo malengo yapo. Kwa hivyo tatizo lile ambalo twaliona na lirekebishwe katika marekebisho haya, ni kwamba ile haki tuliyoambiwa tutarudishiwa wakati ma-rais wapya baada ya serikali ya muarabu, sultani wa Zanzibar na ya wakoloni waigereza, ambao ndio walihusika sana kutupokonya ardhi hizi. Mfano ukiangalia Msambweni kama uko juu ya hewa, ni mahali padogo sana kuliko pale palipoachiwa wakoloni wale wa zamani ambao wameridhisha matajiri kama Ram Singh wa Amalgamated Sugar Company ambapo ardhi hizi ..... (interjection).

**Com. Salim:** Samahani bwana Mohamed sasa watupa historia lakini sisi sote tunajua pia unayo Memorandum bado tutaisoma. Kwa hivyo fupisha maneno yako tafadhali kwani muda unayoyoma na tunao watu wengi bado.

**Mohamed Salim Jumadari:** Kwa hivyo kwa ufupi maoni yangu, kama mwanakenya ningependelea ardhi hizo ambazo kwa sasa hazina matumizi bora kwa wananchi wa Kenya, isipokuwa zinazotumiwa kwa utafiti wa kilimo ama mambo mengine ya maisha kama vile Mtwapa, cha Kari na vile vingine. Tungependelea zigawanyiwe wananchi na kupitia wizara mbali mbali kama ya elimu. Shule ziwe zinaletewa elimu ya technical, kama ni agriculture watoto wawe wanafundishwa, kama ni forestry watoto wawe wanafundishwa na kuwe na Treasury Colleges za kuweza kufundisha watoto kama uvuvi, ama ukulima, kulingana na eneo la Kenya vile ilivyo na natural Endowments ziko tofauti. Nafikiri upande wa elimu nimemaliza.

Kwa upande wa akina mama na watoto, tungependelea Katiba mpya ijayo iwe na vipengele ambavyo vinalinda haki za akina mama na watoto. Kwa sababu hivi sasa ukiangalia, kuna watoto tukiambiwa Katiba ya zamani inatambia haki ya msingi moja wapo ya binadamu ni elimu, hivi sasa ukiangalia huko makwetu ama area nyingi za nchi, utakuta nafikiri hatujachukua statistics, lakini zikichukuliwa huenda watoto ambao hawapati elimu ni wengi zaidi ya wale walio mashule. Kwa hivyo basi, tungependelea kwamba watoto hasa wa kike, wa kiume, na kina mama wapatiwe haki ya kikatiba ya elimu.

Point ingine, tungependelea pia katika Katiba yetu ambayo itarekebishwa kwa upya, kuwe na kipengele ambacho kitatupatia maendeleo ya kisiasa, ambayo tusikubali wana siasa waendeleo kundaganya wananchi kila mara. Na ikiwa itatokea, mwana siasa aseme uongo eti kwa sababu ya cheo ama nini, wananchi wapate njia ya kuweza kurekebisha matatizo hayo kikatiba, ili ikiwa ni malalamiko, yapelekwe vipi kwamba mtu huyu amedanganya. Maanake ikiendelea hivyo itakuwa kila siku tunaongea mambo ya siasa hivi, hivi na ukiangalia kulingana na mwanzo wake, wakosa sana ni wale wana siasa. Kwa hivyo mapendekezo kuanzia Rais wa bunge, tushasikia wabunge wengi wanapigana kule wanatukanana, hayo yote ni mambo ambayo kitaifa hayaleti picha nzuri. Kwa hivyo tungependelea mambo kama hayo katika Katiba mpya yawe yataangaliwa sana na yasimamishwe. Na ikiwa mtu ataendelea na mambo kama haya tupate njia ya kuweza kumrekebisha. Asante.

**Com. Salim:** Shukrani bwana Mohamed kwa maoni yako. Sasa twamuita Mohamed Mwakizayo, hayuko? Hamisi Mwakumaha, hayuko? Ruta Salim Ruta, hayuko? Ali Mwangore, hayuko? Kingi Ali, ametoka? Mohamed Mwarafayo. Hamisi Isiwa, ameenda? Juma Kibwebwe, hayuko? Joseph Odhiambo.

**Joseph Odhiambo:** Mimi naitwa Joseph Odhiambo, maoni yangu ni kama yafuatavyo. Ofisi ya Attorney General, Chief Justice, Police Commissioner wachaguliwe na Bunge, based on merit. Parliamentary candidates au wale wanagombea kiti cha Bunge, wawe na umri kati ya miaka ishirini na tano hadi sabini. Na wawe wana certificate ya form four kwenda mbele. Presidential candidates wawe na umri wa kati ya miaka thelathini na tano hadi sitini na awe ana degree ya kwanza ya chuo kikuu, ama zaidi. Hao wote parliamentary candidates na presidential candidates wasiwe wanauhusiano wowote na corruption cases, ama jambo lolote kuhusu corruption. Mayors na councillors wawe pia wana certificate ya form four na wachaguliwe directly na wananchi. MP's wawe na ma ofisi ambayo yanayojulikana katika constituencies zao. Parliamentary proceedings ziwe covered live na vyombo vya habari, kama television na radio. Ningependekeza tuwe na coalition government ambapo ministers wanachaguliwa kutoka vyama ambazo ziko kwenye Bunge na wale ministers wawe na relevant education kulingana na ile ministry anapewa. Permanent Secretaries, Chairman wa parastatals, wachaguliwe na serikali, serikali ichague employment bill ambayo itawachagua. Kwa mfano, Pricewater House ama Manpower Development na kadhalika, wasichaguliwe na rais. President apate kura zaidi ya 51% wakati wa uchaguzi.

Mambo ya nominated MP's na nominated councillors itupiliwe mbali. Watu wasiruhusiwe kupewa kazi za umma zaidi ya moja, kwa mfano mtu mmoja asiwe Chairman wa more than one institution or parastatal. Awe anafanya kazi moja. Turuhusu political parties ziwe registered nyingi iwezekanavyo, lakini zile manifesto zao ziwe tofauti. Chama kikitaka kuwe registered lazima ile manifesto yake iwe tofauti na ingine. Vyama pia vitafute njia ya kutafuta pesa kivyao, zisipewe pesa na serikali. Kubadilisha Katiba ama sehemu yoyote ya Katiba ambayo itakuwa mpya, ifanywe na National Referendum, isifanywe na wabunge peke yao. Halafu upande wa mambo ya agriculture, ningependekeza tufunge mambo ya ku-import mahindi na sukari wakati ambapo nchi yetu iko na mahindi na sukari ya kututosha. Halafu ningependekeza mambo kama ya agro-chemical, bei ipunguzwe kwa kupunguza ushuru ambao hizi vitu zinatozwa. Asanteni.

**Com. Kavetsa:** Nataka kuuliza kidogo, unajua mambo ya 51% ni majoritarians, yaani wale wengi halafu tuseme kabila ndogo hazitapata nafasi ya kuwa Rais, kwa sababu tunaona vile mambo yamepangwa sasa ni ya ukabila, au wale majority watapata always kuliko minority. Ni sawa kwako?

**Com. Kavetsa:** Kama huna jibu sasa hivi ni sawa lakini fikiria.

**Com. Salim:** Ningependa kujua ni wangapi ambao hawajatoa maoni ili tugawe wakati uliobaki kati yao wote. Ikiwa ni dakika moja mtu atosheke na hiyo dakika moja. Sawa, nitataja majina kisha nitatia alama kwenye majina, nitajua hawa ndio waliobakia. Sawa? Kufuatia nani aliyojiandikisha kwanza. Michael Wangai, okay. Isaac Mulei? Koko Mulwa? Tuanze na Michael Wangai kwa sababu yeye ndiye wa kwanza. Haya.

**Michael Wangai:** Kwa majina naitwa Michael Wangai na haya ndio maoni yangu. Ningependelea kwanza Katiba ya Kenya

uwe na utangulizi ambao utatambua ni Katiba ya akina nani, yaani wakenya, na inamtanguliza Mwenyezi Mungu? Ndio aweze kutuongoza katika nchi ambayo tutakuwa na amani. Na Katiba ningependelea kuwa, iweze kupatikana kwa uraisi, hiyo ina maana kuwa kwa ma-bookshop yote, hata kama vile njugu zinazouzwa Likoni Ferry, iwe pia nayo inaweza kupatikana kwa uraisi. Katiba hii isiweze kubadilishwa kiholela, iweze kubadilishwa katika utaratibu ambao utahusisha wakenya, inaweza kuwa ni professional body ama wabunge pamoja na wakenya wa kutoka tabaka mbali mbali. Katiba kama itaweza kubadilishwa kipengele chochote, iwe kutakuwa na National Referendum. Katiba hii isomeshwe shuleni, iwe katika curriculum ya shule kuanzia standard one kwenda juu. Halafu iweze kuwa na kipengele ambacho Katiba itaweza kutekelezwa, isiwe ni Katiba ambayo itafichwa na haitaweza kutekelezwa.

Elimu: Ningependelea elimu iwe ya bure, kuanzia nursery mpaka standard eight. Kuanzia form one kwendelea kuwe kuna bursary, serikali itoe bursary ambayo itawezesha mzazi ambaye hana uwezo wa kuendelea kusomesha watoto wake, asiwe mtoto hata mmoja ambaye anaweza kuwa na elimu ya secondary na hata university na colleges, asiwe hataweza kupata ile elimu, serikali ichukue jukumu lile.

Kwa waalimu iwe kuwa waalimu wote, kuanzia nursery mpaka waalimu wa vyuo vikuu, masomo yao yawe na muongozo moja.

Hiyo ina maana ya kuwa, vyuo vyote vikuu vinavyofundisha waalimu, viwe vita take-over, vyuo vyote vinavyofundisha waalimu wa primary. Ili mwalimu wa primary akitaka kupata degree yake, iwe ni kwa uraisi kuwe kuna mikakati ya raisi. Nawe vice-chancellor wa universities zote, awe atachaguliwa kutoka kwa ma-professor wale wanaofundisha universities zile. Awe pia atachaguliwa na ma-professor wale ambao watakuwa kwa kile chuo ambaye atakuwa yeye ndiye vice-chancellor. Vice chancellorship iwe ni rotational, isiwe mtu mmoja akawe akau pale tu, kama chancellor kwa muda wa miaka mitano.

Kazi: Vijana wapewe kazi, hiyo ni maana serikali iwe itachukua jukumu la kupatia vijana wote kazi, kijana akimaliza miaka kumi na nane na kuendelea na awe hayuko katika chuo chochote, awe ataweza kupata pesa serikali itampa pesa za kimaisha, awe anaweza kununua chakula, awe anaweza kulipa nyumba na maisha yake ya kila siku atayatekeleza ili uhalifu uweze kupungua. Serikali viwanda vyote katika kila sehemu ambapo vile viwanda vinaweza kuendelea.

Mahakama: Serikali iweze kuleta mahakama chini kwa wananchi. Mwananchi akiwa ana jambo lolote ambalo labda amepokonywa shamba lake, asiwe akipitia kwa lawyer, lawyer aseme kufungua file ni pesa kubwa inakuwa yule mnyonge anazidi kugandamizwa. Yule mtu akifanyiwa makosa anaenda direct kwa mahakama na anapeleka kesi yake na inasikizwa. Asante.

**Com. Salim:** Koki Mulwa, hayuko? Munyi Aman Akida? Uko? Karibu, msikizaji tu! Ali Mwanzabi, ameondoka? Asha Makai, ameondoka? Haraka dakika tatu tu ikiwa nikusoma.

**Siti Hussein:** Kwa majina naitwa Siti Hussein nawakilisha Msambweni Women Group. Mimi ningependa kuzungumza

machache kuhusu mambo ya haki za watoto. Baba na mama wakiachana ki-ndoa watoto wabaki na mama mpaka watimu umri wa miaka kumi na nane. Wakitimu umri wa miaka kumi na nane, awashugulikie kimasomo na kimalezi.

Jambo lingine ni kuhusu “Eda” kwa sisi wanawake wa kiislamu. “Eda” kwa wanawake wafanyao kazi wapatiwe likizo ya miezi minne na siku kumi nyumbani, mpaka wamalize “eda” hiyo. Isiwe ni kama vile huko ndani anavaa nguo za ki “eda” lakini anaenda kazini. Tupitisha kuwa wanawake wawe na likizo hio.

Biashara ndogo ndogo zisiwe na leseni, kwa sisi akina mama ambao tumeachwa wajane, hii inatusaidia sana kimaendeleo. Mama awe na haki ya kutunzwa na wanawe hata kama ameolewa na wanaume ishirini. Wizara ya huduma za watoto ikubali kumkata baba mshahara kwa kila huyu baba mtoto na uwe ni utunzaji wa mambo yote, kulingana na mshahara na hata kama bwana hana kazi, kutafutwe jinsi ya vile mtoto yule ataangaliwa. Mali iliyochumwa na baba na mama igawanye kati ya mama na watoto kwa usawa. Ni hayo tu, kina mama wapewa nafasi kila mahali.

**Com. Ratanya:** Mali gani?

**Siti Hussein:** Mali ile iliyochumwa na baba na mama igawe na mama na watoto sawa.

**Com. Ratanya:** Wakati wa kufa.

**Siti Hussein:** Wakati wa kufa.

**Com. Kavetsa:** Haya mambo ya “eda” wanaume huwa hawaendi “eda”?

**Siti Hussein:** Mara kina mama ndio wenye kukaa “eda”.

**Com. Kavetsa:** Nauliza swali, huenda kukawa na kitu fulani ambacho ni kizuri kwa kabila fulani, na ..... (inaudible). Na ikiwa kwa Kurani inasema ni wanawake lakini kimaisha iwe wanaume pia huenda eda.

**Siti Hussein:** Imewekwa kwa wanawake kwa sababu, na sababu fulani hapa. Na sasa hizo sababu ndio tulikuwa tunasema.

**Com. Salim:** Kwa sababu ya nini?

**Siti Hussein:** Na ndio kwa sababu ya mimba na mambo mengine ya kidini, kulingana na Koran.

**Com. Kavetsa:** Ni kwa waislamu pekee au ni kwa watu wote.

**Siti Hussein:** Kwa waislamu pekee, sijui wakina mama wengine lakini ningependekeza iwe hivyo kwa wote.

**Com. Ratanya:** Na maternity leave?

**Siti Hussein:** Maternity leave, hiyo miezi mitatu ni kidogo sana.

**Com. Ratanya:** Iko hapo?

**Siti Hussein:** Iko mambo. Eda ni miezi minne na siku kumi ile ile ya kawaida. Kwa sababu hatuwezi kufuta imeandikwa kwa maandiko. Na maternity leave ni kitu ambacho kiko katika mambo ya serikali.

**Interjections:** *(Inaudible).*

**Siti Hussein:** Iko, tunayo ile forty days. Sasa si kuna hizi zingine kama kwa wafanyi kazi, wakina mama wanaofanya kazi.

**Interjections:** *(Inaudible).*

**Com. Ratanya:** Wale ambao hawafanyi kazi hawana hiyo kwa sababu wako nyumbani?

**Siti Hussein:** Iko pia kwa saabu kuna forty days, hiyo ni kama maternity leave.

**Com. Ratanya:** Umesema niya forty days?

**Com. Salim:** Asante sana.

**Tinka Ali (14 yrs):** Jina langu ni Tinka Ali kutoka shule ya msingi ya Jomo Kenyatta, niko katika darasa la nane. Nina oni moja, ningependa wanafunzi wapewe msaada wa viatu na soksi, kwa sababu kuna wazazi wengine ambao huwa hawajiwezi katika kuwanunulia watoto wao viatu.

**Com. Ratanya:** Watoto wa kike au wa kiume?

**Tinka Ali:** Wote.

**Com. Ratanya:** Endelea.

**Tinka Ali:** Na sasa watoto hawa kama hawana viatu wakiwa waenda haja wakikanyaga kile kinyesi wanaweza kushikwa na ugonjwa mbaya, ama wakakatwa na vigai na misumari ambayo inaweza kuambukiza ugonjwa wa tetanus. Sasa zingine pia wanafunzi hao ambao hawana viatu wanaweza wakashikwa na funza. Na ambao wanafunzi hao wakienda darasani huwa hawezi kusoma kwa vile funza wanasumbua kwa kule kuwashawasha, hawezi ku-concentrate na mambo ya masomo. Kwa hivyo ningependa tupewe misaada ya viatu na soksi. Ni hayo tu.

**Janet Nyambariga (15 yrs):** Kwa majina naitwa Janet Nyambariga niko katika darasa la nane. Mimi ningependekeza wanafunzi kupatiwa gari la shule, maanake mara nyingi kama darasani huwa tunafundishwa kwa mfano GHC, huwa tunafundishwa mahali fulani ambapo pana vitu. Na huwa hivyo vitu ukiviona mtu anaweza ku-understand vizuri, sasa tukiwa na hiyo gari ya shule, tunaweza kusafiri na kuenda kuangalia vile vitu. Maoni yangu ni hayo tu.

**Com. Kavetsa:** Ungependa nani awapatie?

**Janet Nyambariga:** Ningependa serikali itupatie.

**Asha Mwatsuluka (16 yrs):** Kwa majina naitwa Asha Mohamed Mwatsuluka nasoma darasa la nane.

**Com. Ratanya:** Uko na miaka ngapi?

**Asha Mwatsuluka:** Miaka kumi na sita. Ningependa kuiomba serikali ituletee tractor ya kusafishia compound yetu, kwani sisi tukifanya kazi kama ya kukata nyasi wakati wa masomo tunapoteza wakati muda mwingi. Afadhali kuwe na tractor ya kukata nyasi, na sisi tunaendelea na masomo. Yangi ni hayo.

**Michael Kuria:** Kwa majina naitwa Michael Kuria kutoka shule ya msingi ya Jomo Kenyatta. Niko katika darasa la nane. Mapendekezo yangu ningependa kuiomba serikali iweze kusaidia mashule yaweze kununua vitu vya extra-curricular activities kama mipira hivi ili wanafunzi wawe wakivitumia na hata wanafunzi wengine, they discover their talents while they do that. Ingekuwa vizuri kama serikali ingewanunulia vifaa hivyo, hata unakuta wengine wana-discover their talents, halafu wanakuwa exposed to other things. Na pia, ningeiomba serikali kuhusu majina ya wale wanafunzi wanaomaliza colleges yaweze kuchapishwa kwenye magazeti ili wananchi waweze kuelewa kama kuna mapendekezo katika mambo yale, kwa sababu inawezekana kuwa wanapendelea mahali kama, pengine wanapendelea huko bara sana kuliko huku Coast, sasa unapata watu wa kule bara wanaenda colleges lakini wa huku Coast wengi wanawachwa. Asante.

**Com. Salim:** Ni wangapi ambao wamebakia? Jina lako.



**Com. Kavetsa:** Watoto mnajua mambo ya Children's Act? Mwalimu wanajua Children's Act? Kwa nini hawajui? Hiyo ni haki yao kwa sababu hawa wote wanazungumza juu ya shule yao wala sio haki zao kama watoto.

**Com. Salim:** Inaonekana hiyo civic education haijawafikia watoto kuhusu haki zao. Wapi district co-ordinator?

**Com. Ratanya:** Inafaa mwalimu nijue kwamba hii Katiba niya hawa watoto wala si yetu, kwa hivyo ningekuuliza uone kuwa hawa watoto wanapata elimu ya children's act kama wenzao otherwise si vizuri watoto kutojua haki zao.

**Mesaidi Sole Mwabana:** Kwa majina naitwa Mesaidi Sole Mwabana, deputy wa hapa, hii shule ambayo hii exercise inaendelea, mengi yamesemwa kuhusu wanawake, ningependekeza kuchangia katika haki za wanawake, kuhusu mambo kama ya kuchaguliwa katika idara nyingi ama mambo ya kazi fulani, kama kwenye Commission. Wanawake wawe wanahusishwa sana, sio kama vile tunaona katika Commission nyingi mwanamke anakuwa mmoja wengi wanakuwa wanaume. Hiyo huwa haitiliwi maanani, mambo ya gender. Kwa hivyo ningependekeza katika Katiba ambayo itakuwako wanawake wawe wanahusishwa sana katika mambo hayo.

Pili, mambo ya eda yashasemwa, yalikuwa kwenye haya maoni yangu.

Lingine ni mambo ya majimbo, mimi pia ningependelea serikali ya majimbo, lakini sasa walikuwa wakisema tu members wawe kama mfano hii Regional Assembly iwe na five members ambao wanatoka katika each District. Lakini katika hao five members ningependekeza hiyo serikali kama itaangalia wanawake pia wawe wanahusishwa sana katika mambo kama hayo. Na katika hiyo .... (inaudible).

**Com. Kavetsa:** ..... (inaudible).

**Mesaidi Sole Mwabana:** Haya basi mimi nawaambia.

**Com. Kavetsa:** ..... (inaudible).

**Mesaidi Sole Mwabana:** Basi mimi napendekeza wanawake wahusishwe katika hawo watu watano, mmoja awe mwanamke na hao wengine watakuwa wanaume.

**Interjections:** (Inaudible).

**Mesaidi Sole Mwabana:** Wale watatu, kuna watatu. Watatu, wanaume wawili na mwanamke.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo hutaki wanawake wengi?

**Mesaidi Sole Mwabana:** Wako, lakini sasa waingize pia.

**Com. Kavetsa:** What percentage?

**Mesaidi Sole Mwabana:** Percentage, the female should be included and should be more.

**Com. Salim:** More than men?

**Mesaidi Sole Mwabana:** More than men, yes.

**Com. Salim:** Wabadilisha sasa.

**Mesaidi Sole Mwabana:** Sijabadilisha nilikuwa nimesahau.

**Com. Kavetsa:** It may be twenty and we want to know, why don't you give us a percentage just like other people are giving us percentages. 100%, 2%, 3% whatever you want to give.

**Mesaidi Sole Mwabana:** The percentage is 40% men and then 60% iwe to women. Maanake kila mahali wanawake huwa hawaangaliwi sana. Sasa hiyo Katiba mpya na pia katika hiyo National Assembly, huwa kuna three members ambao watatoka katika ile Regional ambao watakuwa kwa National Assembly and among those three members, one female should be included among the three members.

**Com. Kavetsa:** ..... (inaudible).

**Com. Ratanya:** Is it the other way round?

**Mesaidi Sole Mwabana:** 60% men and 40% women. The other way round. Sasa nawaonea huruma sasa, huko si ni juu huko, wataenda kama kutakuwa na kura huko sasa pengine tutaungana na wengine kutoka Region nyingine, halafu mwisho pengine nisichukue wakati mwingi.

Elimu: Ningependekeza elimu ya bure, kutoka primary education darasa la kwanza mpaka la nane, halafu serikali iwe itaangalia pre-primary education, kwa maana wakati huu pre-primary education inakuwa based on shule au parents. Serikali huwa haishughuliki sana, kwa hiyo hiyo Katiba ingine ningeonlea maoni yangu kuwa pre-primary education pia iwe serikali

inaanagalia sana, kwa sababu ndiyo mwanzo wa elimu pale. Kwa hivyo, serikali iwe ikiangalia halafu elimu yenyewe iwe niya bure lakini ikifika secondary education iwe watalipa kama vile hufanyika katika university, unaenda halafu unapatiwa msaada. Syllabus iwe haibadilishwi kila mara, kuwe kuna wakati fulani wa kubadilisha syllabus, kwa maana huwa inatupa shida sana, mara kwa mara syllabus inabadilishwa bila mpango maalum. Kwa hivyo, ningeonelea syllabus iwe inabadilishwa baada ya muda fulani, baada ya miaka ishirini na tano ndio syllabus inabadilishwa, ili tuangalie ile nyingine ilifanya nini na hii ndio tunaibadilisha. Yale masomo ambayo yatakuwa kwenye ile syllabus, tuwe tunafundisha yale masomo ambayo yatakuwa yanatainiwa, sio masomo ambayo hayatainiwi. Masomo kama yale huwa ni mzigo kwa watoto na pia kwa wazazi, mtoto anafundishwa somo ambalo halitainiwi. Katika hiyo syllabus kuwe hakuna masomo ambayo hayawi examined. Kuwe tu tunafundisha yale masomo ambayo yatakuwa yanatainiwa, yasisupatie mzigo sana. Pengine kwa hayo machache, natoa shukrani.

**Com. Salim:** Sijui kama mwenzangu ana swali la kufafanua?

**Com. Kavetsa:** Lakini wekeni mikono juu. Munaongeza mikono.

**Com. Salim:** Tuko kwenye list ya mwisho. Bwana Tende sioni jina lako hapa.

**Tende Zengeza:** Langu liko nimekuja mwisho mwisho saa nane.

**Com. Salim:** Watu 15 kwa hivyo huu jamaa Tende .. Z. Tende ..... (inaudible) haya endelea.

**Tende Zengeza Tende:** Naitwa Tende Zengeza Tende kutoka Lunga Lunga location. Mimi sina maoni mengi mawili, matatu kidogo na sitayafafanua kwa urefu sana, kwa sababu ya kuchelea muda.

Kwanza naanza kule juu, ningependelea hiki cheo cha urais kipunguzwe mamlaka. Kisiwe na mamlaka zaidi ya kufanya mpaka zile sehemu zingine haziwezi kuamua isipokuwa afikiwe yeye. Nikija kwa ubunge, nasema wapelekwe watu wenye elimu kuanzia form four na kwenda juu.

Na kwenye ma-councillors, councillor awe ni mtu wa certificate kuanzia tunasema standard seven maanake tumesoma kitambo na kwendelea. Kwa ujumla aingie na certificate sio aende tu kwa sababu anajua kuzungumza.

Lingine ni kwamba katika Katiba hii, watu wa kule reserve, wawe wanahudumiwa sawa na wa town. Kwa mfano, ikiwa kumetokea kwamba sehemu ya Pwani inataka kuwekwa maji kila sehemu, ama nchi kavu ambayo haitumiki kikamilifu, basi ifikiwe kule nchi kavu kweli, sio iambiwe ni nchi kavu ifikie Msambweni na kuna barabara ya lami, mpaka Kinango iingiwe. Huko sijui itabidi ni mole kuingiwe, sijui ni Lunga Lunga ya wapi huko ndani, kuwe kunapata maji safi, moto ukifika kwa mfano

kama Lunga Lunga town kuwe kuna msaada wa serikali kuwasaidia wale ambao wako reserve nao wapate kitu kile.

**Com. Kavetsa:** Endelea.

**Com. Salim:** Uko karibu.

**Tende Zengeza Tende:** Ndio, ni karibu kumaliza mimi.

**Com. Salim:** Haya kilimo.

**Tende Zengeza Tende:** Kilimo nacho, nafikiri nchi zingine watu wanasaidiwa na matingatinga, yakija kwa district wawe watu wanaotoa maombi ni watu wa kutoka kule mashambani, si watu wa town.

**Com. Kavetsa:** Pendekezo.

**Tende Zengeza Tende:** Napendekeza ikiwa kumekuja mambo yoyote katika district, basi kuchukuliwa kutoka sub-location wafaidike.

**Com. Salim:** Wafaidike na nini?

**Tende Zengeza Tende:** Na mambo ya ukulima.

**Com. Ratanya:** Kwa mfano kama kuna tingatinga ya serikali hapo, sasa kama ni kulimia watu, sio ulimie ma councillor na wale wengine kama ma chief.

**Com. Ratanya:** Kuna zingine hulimia watu?

**Tende Zengeza Tende:** Kuna zingine ambazo huwa zinalimia watu kimsaada. Yule ambaye hajiwezi. Halafu kuna point moja ambayo nilikuwa nimesahau, lakini sasa hiyo ni muhimu sana, hata hapa jirani wetu wanafanya kitu kama hicho. Ni kwamba idara ya polisi ikiwa wanadhulimu mwananchi wa kawaida ambaye hana uwezo, kuwe na chombo ambacho hakitapitia katika station pale, yule mwananchi aseme shida yake ile amefanyiwa na kuwe na board ya kuchukulia hatua mara moja. Sio uende ukasema kwa station hivyo, ukitoka pale kidogo unaambiwa wewe umekuja kunisema kwa sababu nimekosea hivi na hivi, basi wewe unapotezwa. Umekosewa wewe na unarudi unapotezwa wewe kwa sababu huna haki. Halafu hivi vyombo vitatu viwe vinajitegemea sasa, vile vya juu kama mahakama, Bunge – na kitu gani tena kuna ingine nimesahau lakini anyway.

**Com. Salim:** Na serikali.

**Tende Zengeza Tende:** Na serikali, very good.

**Com. Salim:** Mamlaka.

**Tende Zengeza Tende:** Mamlaka. Pia watu wa reserve wapelekewe vyombo vya habari ili shida zao zifike huko juu. Maana hakuendi waandishi wa habari huko huko ma-reserved na watu wanaumia na shida. Kwa mfano kama kumeingia njaa, mtu anaumia na njaa na hana njia ya kujieleza kwamba huku tuliko sisi tuna njaa. Mpaka asafiri pengine mpaka ofisi ya chifu, na akiletewa ule msaada anaanza kufaidika na hiyo ofisi ya chifu, hata wewe mwenye nja utapata kilo moja. Ofisi ya chifu, councillor watajikusanyia chakula mpaka ingine wauze.

**Com. Ratanya:** Sasa unapendekeza nini?

**Tende Zengeza Tende:** Napendekeza kama ni msaada imufikie yule ambaye anaumia.

**Com. Ratanya:** That's through a direct power.

**Tende Zengeza Tende:** Sio direct, lakini waambiwe kazi yao nikutangaza tu kwamba siku fulani kuna msaada. Na ikija iwe yule mwananchi anajua kwamba siku fulani itakuja ama store fulani, ama ni katika hiyo ofisi mgawanyaji awe nani, huyo mwenyewe anaye umia ndio wasidhulumiane.

**Com. Kavetsa:** Kwa nini mnakubali hayo ifanyike?

**Tende Zengeza Tende:** Si kukubali.

**Com. Kavetsa:** Ni kukubali ..... (inaudible).

**Tende Zengeza Tende:** Mimi nasema hivi, wananchi siamini kwamba wamekubali, kwa sababu siku zilizopita sisi tulikuwa hatuchagui. Unayemchagua siye anayepita, kwanza hili jambo la kwanza. Sasa kama amepitishwa yule ambaye hukumchagua, si ni lazima atakulalia?

**Com. Kavetsa:** Lazima umuambie akuwakilishe.

**Tende Zengeza Tende:** Umuambie, hata ukimuambia na yeye anajua kule werevu uko wapi, wafikiri atakuakilisha, hakuna.

**Com. Salim:** Asante sana. Ushamaliza?

**Tende Zengeza Tende:** Nishamaliza asante.

**Com. Kavetsa:** Kama una mengi nitamuuliza huyu hapa akusaidie kuiandika halafu mtaituma kwa Tume. Sawa?

**Tende Zengeza Tende:** Sawa kabisa.

**Com. Salim:** Sahare Kisupi.

**Sahare Kisupi:** Tayari.

**Com. Salim:** Kwa ufupi kabisa bila kupoteza wakati .... (inaudible).

**Sahare Kisupi:** Na nitatoa kwa ufupi sana, ki-upepo sio kumaliza yote. Tumekuja hapa kwa naiba ya Commission kuja kuchangia Katiba mpya ya Kenya. Lakini kwangu ni ufupi nikisema ufupi, tunasema tunairudia Katiba kuifufua ya Kenya, hatuichangii. Katiba tunayo ifufua ni ile ambayo ilitoka Lacanster house. Katiba hii niya sitini na mbili, sitini na tatu, iliyokuwa inawakilishwa na partition zetu za Kenya. Moja ikiwa na majimbo au KADU ikiwakilishwa na Ronald Ngala, Masinde Muliro, Daniel arap Moi ambaye sasa ndio President wa nchi.

*Interjections: (Noise from the audience).*

**Com. Salim:** Hayo yote tunayajua. Leo wataka Katiba ibadilishwe vipi?

**Sahare Kisupi:** Kwa hiyo, nikusema ile Katiba ya mwaka huo ndio inayostahili maanake Kenya haikutumika, ilichujwa, watu wakatamia muelekeo wao wa ule mlio usikia tukiambiwa tuna serikali ya mseto. Hatuna serikali ya mseto, lakini walileta mchujo wakafanya mseto.

**Com. Kavetsa:** Wakati huu ungependa nini?

**Sahare Kisupi:** Ningependa Katiba ya majimbo.

**Com. Salim:** Na hiyo ni kama ilivyokuwa?

**Sahare Kisupi:** Kama ilivyokuwa.

**Com. Salim:** Bila mabadiliko.

**Sahare Kisupi:** Bila mabadiliko. Ikiwa mkoa umepata jimbo lake, utaunda sheria zake kufuatana na vile hali ilivyo. Nikisema mkoa ni kivipi, tuko na mikoa minane, groups, kwa mfano Gema – Kikuyu, Meru, Embu asili mia ishirini na tano na ishirini na nne. Kamukusu – Kalenjin, munisikize vizuri, Maasai, Turkana, Samburu wana asili mia kumi na tisa hamsini na mbili. Luhya wana asili mia kumi na mbili thelathini na nane. Luo, Suba wana asili mia kumi na asili mia tisini na tano. Kamba wana asili mia tisa zero five. Tunarudi kimkoa, Kisii, Kuria wana asili mia tano ishirini na nne.

**Com. Salim:** Kwa kiwango kigani hao?

**Sahare Kisupi:** Ni wakati wa ninety-seven. Tulieni kwamba nataka kumaliza hapo. Coastal groups ni asili mia tisa hamsini na mbili, lakini hawaeleweki ni kina nani. Mama Commissioner amesema je, North Eastern. North Eastern wana asili mia tano sabini na mbili. Marsabi and Isiolo asili mia mbili thelathini na nane. Lakini hawana groups. Kwa hio nikisema Katiba iwe ya majimbo nikusema kwamba ile asili mia tano ya uchaguzi wa President ilichukuliwa kwenye mikoa sita sehemu tatu ikachukuliwa mikoa hii miwili ikafanywa kuwa sehemu tano kwa asili mia tano kumptisha President, kwa maana groups hakuna, no, nil, hawana. Ni watu tu wakutangatanga kama wa kuokotwa kujaza ile nafasi ili President aweze kufanya lolote.

**Com. Kavetsa:** Uheshimu kila mkenya na maisha yake na vile anaishi na vile ana abudu. Hutadharau mtu mbele ya Tume, kutanganaga ni nini? Utaheshimu kila mkenya na maisha yake.

**Interjections:** *(Inaudible).*

**Sahare Kisupi:** Naomba Tume msamaha. Tunarudi sasa kwenye uchaguzi.

**Com. Salim:** Patia mwingine nafasi.

**Com. Ratanya:** Tupatie mapendekezo.

**Sahare Kisupi:** Kwa hivyo mapendekezo.

**Com. Salim:** Pendekezo lako la kwanza wataka majimbo kufuatia Katiba ya mbeleni.

**Sahare Kisupi:** Kwa sababu nitawaonyesha vitu.

**Com. Salim:** Yes or no? Tafadhali.

**Sahare Kisupi:** Hizi ni ardhi zimegawanwa.

**Com. Salim:** Tafadhali jibu swali

**Sahare Kisupi:** Kwa hayo machache ninashukuru. Kwa sababu hiyo yote nikuchoka, kazi ya Tume nikupokea na hakika mumepewa jukumu kubwa la kusikiliza wananchi. Utapata mwenda wazimu amekuja, utapata mwenye maswala ovyo ovyo nayo kazi yako ni kumsikiliza. Mimi ninasema hivi Katiba iwe ya majimbo.

**Com. Salim:** Pendekezo lingine?

**Sahare Kisupi:** Na pendekezo lingine ni kwamba ni ile moja, katika waislamu wamezungumza lakini mahakama ya kiislamu haini korti kuu ya rufani. Tukitoka kwa malalamiko ya Kadhi, hapa ametuoza tunakwenda kwa korti ya kiislamu. Tunakwenda kwa Chief Kadhi, ukitoka hapo unakwenda kwa korti ya kisheria, ambapo yule anayewakilisha korti ya kisheria sasa za nchi ni tofauti na zile taratibu zilizoko katika ratiba za kidini.

La kumaliza ni elections, baada ya jimbo, government na mawaziri wake watatoa nafasi kuweko na uchaguzi wa serikali kuu ya united state, yaani serikali kuu ya kuwakilisha majimbo, ambayo waakilishi wake watatoka kwenye sehemu za majimbo.

Raisi asiwe juu ya sheria. Yote yaliyoko Kenya ni kwa sababu Rais amekalia sheria, hata mkuu wa sheria hawezi kumaliza lazima amuone Rais. Ardhi imetogawanywa kimahakama, ni sheria President anasema toa hiyo scheme, hapo sitarudia. Mahakama iwe juu kwa sababu ya sheria, Rais awe chini ya sheria. Anapofanya makosa kulingana na maongozi yake, awe ni mshtakiwa kufuatana na kazi yake, akiwakilisha raia katika nchi kama Rais.

**Com. Salim:** Ashtakiwe wapi?

**Sahare Kisupi:** Kortini?

**Com. Salim:** Asante sana.

**Sahare Kisupi:** Namalizia kwamba yule polisi anaposhika mtu unashangaa ukifika kortini utaambiwa kwamba polisi maneno yake ni ya hakika kuliko wewe ambaye umepelekwa kortini, ima umefanya ima hukufanya kitendo. Inachukuliwa moja kwa



moja fine, kesi kwamba wewe una hatia. Pendekezo langu, napendekeza polisi yule ambaye atakuweko kortini, aweze kueleza sababu za kufanya mpaka akushike. Ni sehemu chache sana jambo hili ambalo hutokea mahakamani.

**Com. Salim:** Polisi aulizwe nini?

**Sahare Kisupi:** Polisi, mimi nimeshitakiwa file iko kortini, ni polisi yule aje tupeane maswali directly mimi na yeye vile mwanzo wa kufanya ushikwaji wa mimi.

**Com. Kavetsa:** Kuna watu ambao wana .... (inaudible) ati polisi ndiye anakushika halafu ndiye anasimamia kwa sababu hauna mtu mwingine anakushika halafu wanaenda kwa korti wanasema wamekushika kwa nini na nini, na inakuwa kama vile unasema ndio ukweli wa mambo.

**Sahare Kisupi:** Prosecutor wa korti, yeye ndiye anazungumza maswala ya fine na kukuhoji wewe ambabpo ulishikwa na polisi. Polisi asiyekushika anaambiwa na adhumani jamaa amefanya hivi. Nashukuru kwa hayo machache sina mengi. Tume, Commissioner jina langu nimeweka hapo na itapata Memorandum zaidi kwa sababu kule ofisini Kencom najua mtaziona, mkiziona mtaambatanisha na haya kwa maana muda umeharibika na umetoweka. Nashukuru kwa haya machache.

**Com. Salim:** Asante bwana Sahare. Tuko tayari kupokea Memorandum yako. Sasa ni Peter.

**Interjections:** (Inaudible).

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Asante jina ni Kassim Nasoro Ndarusi Mwazi Mshenga.

**Com. Kavetsa:** Endelea.

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Ikiwa Katiba hii nashukuru sana kwamba Katiba imeanza sitini na tatu wadhifa wa nchi hii, hayati Mzee Jomo Kenyatta. Mpaka leo mimi nashukuru sana kwamba Katiba inaendelea vizuri vile vile, lakini sitini na tatu hayati Mzee Jomo Kenyatta, wadhifa wa nchi hii alisema mwananchi pale alipo, hata ikiwa ni chini ya mti aishi pale pale. Lakini maendeleo yalipoendelea ni mpaka akalimizika hayati huyu ameingia Rais Daniel arap Moi kwa haki, kwa sababu alisema anafuata Nyayo. Kwa hivyo nilifanya shukrani sana kwa hali ya Rais hayati Mzee Jomo Kenyatta wadhifa wa nchi hii, mpeperusho wa bendera ya nchi hii kwa kusema mwananchi pale alipo aishi pale pale, hata ikiwa ni chini ya mti, pale nilifurahi sana.

Lakini muda mfupi, mahali ninapoishi nilisikia panaitwa crown lands. Nilijaribu kuweka mkono kidogo, nafikiri nikaishi tena karne nikapata kama panaitwa “scheme”. Hapo niliuliza ni nini maana ya scheme, wanasema scheme itapatiwa yule ambaye ametangulia pale pahali, ndiye ataanza kupatiwa halafu mwingine. Lakini muda mfupi nilipata ngwangwa wanapasua tu,

walipofika kwangu nikawazulia wakasema hii ni amri ya serikali. Kwa hivyo nilikubali kupasuliwa kwa ardhi hiyo mpaka kumalizika, dakika nilipata namba bandia. Mapema, nikaambiwa namba hii ni yako tena ni ya hapo hapo unapoishi. Nikiangalia mwaka wa hamsini na mbili nikimuuliza babu anasema hii ni ardhi ya serikali mpaka ni ule wa nguzo zile za simu, sasa pia hatuzioni vya vyuma hivi. Kwa hivyo kifupi nimeshukuru uwezekano wa Katiba hii kuwasili mahali kama hapa ambapo tulikuwa hatuwezi kufika, kwa sababu mimi naugua kule niliko kwa muda mrefu. Shamba langu limepasuliwa, limemalizwa namba niliyopata sio ya pale, nililia. Nikajaribu kwenda kwa mguu ama kwa gari pole pole mpaka nikaauliza nikaambiwa shamba hili nila DC. Kwa hivyo nilifanya juhudi kutafuta DC huyu kwa kukopa tikiti, mpaka nikapata nikaambiwa kwamba huyu anaitwa Hassan Bonu. Nikaauliza yuko Kenya? Nikaambiwa yuko Kenya.

**Com. Ratanya:** Aitwa nani?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Hassan Bonu. Kwa hivyo nilikaa muda nikampa chifu wangu ananiambia unaitwa na nani? DC, ana nini:? Si unasema una shamba eti ni vizuri, pia hapo ningeshukuru. Tukaenda, mpaka nikafika Mombasa, tukapanda, tukafika. Nafikiri DC huyu aliniambia shambani mwako mumetoka namba ya mtu. Mtu mwenyewe amesema atakupatia laki kumi, kama mimi mkuu wa mkoa nilisema apata laki sabini na tano, akupatie nyumba akuchimbia kisima, akulimie na shamba, nikamwambia hayo mambo matatu yanatosha kabisa uhai wa binadamu. Kwa hivyo ikiwa wewe ni DC wa haki ulimeza kiapo kwa kutumikia umma, shambani mwangi mimi siondoki. Shambani mwangu siondoki wacha ya maji ya kisima hata visima vya petroli mimi siondoki, sababu hamsini na mbili na tumika mkoloni. Na lipa kodi kumi na mbili mpaka leo siwezi, kwa hivyo DC huyu nilimueleza shambani mwangi siondoki na wala sitaka maneno kutoka kinywani mwako kunirudishia. Kwa hivyo mimi nilirudi moja kwa moja mpaka kwangu, nikaangalia niaona kwamba ardhi yote hiyo, watu waliopata namba ni watu saba peke yake. Na nambari zile walizopata si zile za makaoni mwao, ni mbali mbali kurushwarushwa. Ardhi yote namba zimekwenda nje, wa kwanza nilisikia maenyakuwa yangu, mwingine siwezi kusema. Kwa hivyo mimi nasema ikiwa Tume hii ina haki, mimi ningependelea sana hasa nambari kama hii, Mungu akipenda iende moja kwa moja mpaka pahali popote ili nambari hii ya shamba hili langu niweze kupata, kama mtawala wa nchi hii.

**Com. Salim:** Ina namba?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Wanasema mia mbili tisaini na moja na nia mbili themanini na sita. Huyu amekalia shamba langu, hii nambari niya shamba langu. Mnifanyie msaada mkubwa ikiwa hili ni Tume la haki na watu ambao hawawezi kufika nchi hii.

**Com. Kavetsa:** Haya pendekezo mzee hi hiyo shida yako tumeisikia na ni hadithi ambayo ina watu wengine wengi. Sasa pendekezo ambalo linaweza kuisaidia wewe na wengine kama wewe, ni pendekezo lipi? Unapendekeza nini?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Ningependekeza kama Tume hii niya haki ifanye nguvu moja kwa moja, wananchi

warudishiwe zile haki zao ambazo zimenyakuliwa na wanyakuzi wengine wenye nguvu. Warudishiwe wenyewe wananchi.

**Com. Kavetsa:** Na haya mambo yalikutendekeza mwaka gani?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Sijui, sikusoma mimi. Mimi natumia bongu tu. 1991. Na barua nimemaliza si kupewa chochote, nimekwenda mapka nimemalizika.

**Com. Kavetsa:** I am trying to figure out ..... (inaudible). When did this sharing out of shambas start? Iianza mwaka gani?

*Interjections: (Inaudible).*

**Com. Salim:** Unajua sisi kazi yetu ni kufanya kazi ya kumjalua mtu kazi yake, lakini kumsikiza maanake ..... (inaudible).

**Com. Ratanya:** Mzee ulikuwa unaambiwa ulipe 10% ya hii, deposit ya 10%.

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Nililipa ya namba.

**Com. Ratanya:** 90 days .... (inaudible).

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Sema Kiswahili kwa sababu no English.

**Com. Kavetsa:** ..... (inaudible).

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Nililipa.

**Com. Kavetsa:** Wacha niulize, kuna Commission yoyote ishawai kufika huko?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Imepita.

**Com. Ratanya:** Baada ya hapo ulilipa pesa ingine baada ya hiyo 10%?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Sikulipa, nitalipa vipi na nilipa hiyo sasa nililopata hiyo sasa bado niko mbio mpaka leo.

**Com. Ratanya:** Ulilipa hiyo peke yake?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Nililipa hiyo peke yake.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Kuna watu ambao hawakupata namba na humo humo wametimiza haki humo humo, lakini namba hawana na shamba zimekwenda, makaburi yako humo humo, misikiti iko humo humo, pia vitu hivyo vyote vimechukuliwa kwa watu wengine. Sasa kama tutajiunga kwa wakili tutajiunga wangapi na wengine hatuna nafasi. Hapa mimi nimefanya kuombewa tikiti, haki ya Mungu.

**Com. Kavetsa:** Hii shida ni yake ama ni shida imetendeka kwa wengine.

**Public:** Imetendeka sana sana ... (inaudible).

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Mikoani yote si mahali pengine. Si mimi ndio peke yangu. Ni kote, umma mzima. Mimi niko hapa hapo tu nikingoja, na ngoja kwa hamu.

**Com. Ratanya:** Kwa hivyo hiyo hutakosa kama iko hapa hapo.

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Nitakosa.

**Com. Ratanya:** Hutakosa.

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Mimi niko hapo hapo ninaishi hapo. Tena hata ikiwa ni wewe unakuja mgeni ujitahadharishe kwa vile ilivyo hapa, haki tena.

**Com. Ratanya:** Haya basi vizuri sana. Tutakusaidia, lakini mambo kama haya huchukua muda.

*Interjections: (Inaudible).*

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Hatuna.

*Interjections:* Bwana Commissioner hakuhakikishia huyu bwana anapanga kila kitu, huyu namtii .... (inaudible), anapanga lake. Anakuambia ukiwa mgeni uje vizuri basi wampa pesa yule.

**Com. Salim:** Lazima uende huko useme haki yangu ulipata au hukuipata.

**Com. Ratanya:** Hii settlement scheme inaitwa aje?

**Kassim Nasoro Ndarusi Mshenga:** Yaitwa Ukingoni Settlement Scheme.

**Com. Kavesta:** You know when we taked to the people at Bura who settled there in the temporary scheme walisema sisi serikali ilituleta hapa na pia wale wengi wao wanasema sisi serikali wale walikuweco wanasema serikali ilichukua mashamba zetu. So inaonekana kama hata wale walikuja, hawakutarajiwa wakati huo sijui ni nini. Kuna kitu kilitendeka hapo, serikali inajua haya mambo. For the people who came say the government brought us here, the government took our shambas. Sasa pengine kwa hiyo ndio inafanya watu wazunge ili wasaidiwe.

**Com. Salim:** Okay, tumpate Peter Kenga.

**Peter Kenga:** Mimi ni majina naitwa Peter Kenga, na nafanya kazi na idara ya Kilimo.

**Com. Salim** Tafadhalini tutamiliza, wacheni atoe maoni yake.

**Peter Kenga:** Nitakuwa na machache sana ya kuzungumza kwa sababu mengi nimeandika katika Memorandum na nishaipeana. Katika idara zetu za kuimarisha kilimo, ningependekeza kwamba ama ninaomba maombi kwamba, ile importation ya farm inputs kama fertilizer iwe duty free, ndio bei ya vitu kama mbolea irudi chini ili wakulima waweze kutumia mbolea na kuimarisha kilimo chao. Utakuta kwamba bei ya vitu vya kulimia imekuwa juu sana kwa sababu ya ile importation duty ambayo imewekwa na wakulima wengi hawawezi wakaimudu. Na pia imefanya mpaka cost of production imekuwa very high, kwa hivyo farm inputs ziwe imported duty free.

La pili, katika hali ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu, utakuta kwamba kuna ma bilioni ya pesa ambayo yanapotea ambayo yangeingia katika serikali as in form of revenue. Kwa mfano, kuna wale wafanyi kazi wa serikali wa ngazi za juu, watu ambao wanauwezo wa kulipa hii custom duty wakati wanapoingiza vitu vyao, hao wamepewa nafasi au privilege ya ku-import vitu kama magari duty free kama lecturers wa university na wale wengine wengi, ambapo mtu mnyonge yule wa chini akijaribu kuingiza radio tu kutoka Tanzania nchi jirani kwa mfano ama baiskeli ili gharama ya kulipa custom duty itamshinda.

**Com. Salim:** Pendekezo.

**Peter Kenga:** Pendekezo ni kwamba sasa wale watu wasiwe na zile privileges ambazo zina deprive the government of billions of money in terms of revenue, zile privileges ziondolewe, ili kwamba wale pia nao walipe ushuru wanapoingiza mali yao nchini, ili ile pesa isaidie serikali kuimarisha uchumi wa Kenya.

**Com. Salim:** Hizi privileges ziondolewe.

**Peter Kenga:** Hizo privileges ziondolewe. Lingine, wakati serikali inapoangaliwa mishahara ya watumishi wa umma, inaangaliwa indiscriminatively. Kwa mfano, hizi lucrative salaries za Honourable Members of Parliament ziko juu kiasi ya kwamba hawawezi waka justify kwa nini wapate mishahara ya manake ya pesa, hali kwamba kuna mfanyi kazi mwingine mnyonge anayepata as low as Shs.3,000/= per month na mtu kule juu anapata more than Shs.300,000/= and something thousands per month. These salaries should be reviewed and ile gap between huo mishahara wa juu na ule wa chini, iwe harmonized, iwe reduced. Wapunguziwe mishahara iongezewe hawa wa chini nao wainuke ki maisha.

La tatu, ningependekeza tu serikali ya coalition government, ya muungano.

**Com. Kavetsa:** A coalition government ya mseto.

**Peter Kenga:** Ya mseto. Nafikiri kwa ufupi sababu ya wakati wacha nifikie hapo, kwa sababu mengine nimeshayaandika na nimeyapeana. Asante sana.

**Com. Salim:** Asante sana bwana Kenga yeye ndiye wa mwisho kutoa maoni yake na tumefurahi kwamba tumeweza kumaliza na kuwasikiliza na kila mtu akapata nafasi ya kutoa maoni yake. Kilio bakia ni kuwashukuru sana nyote, kwa sumra yenu jinsi ambavyo mumebakia hapa, mumekaa masaa mengi sana ili mpate nafasi ya kutoa maoni na wale wengine kati yenu ambao wameendelea kukaa, hata baada ya kutoa maoni yenu, mungependa pia kusikiza maoni ya wenzenu na hiyo ni ishara nzuri sana.

Kwamba mambo haya ya Katiba na kurekebisha Katiba ni muhimu kwenu. Nataka kuwahakikishia kwamba sisi pia ni muhimu kwetu na hii kazi yetu tutaifanya with very open hearts with impartiality na objectivity. Na maoni yenu yote tumeyanasa tumeyaandika na tutarudi Nairobi kuyachunguza, kuyasoma kwa makini zaidi kwa wale mliotupa Memorandum, na Mungu atusaidie na dua zenu pia ziwe nasi, ili tuandike Katiba ambayo itapendekezo wananchi, na ambayo itatusaidia kwendesha nchi yetu kwa njia iliyobora zaidi kuliko hapo awali.

**Com. Kavetsa:** Tafadhhalini msichukue kama huu ndio mwisho, au m-relax kusema mumetoa maoni. The people who are not here, please get them to write Memorandums, there are very few Memorandums from Coast in our library and we need to have very many there, get the teachers to write, get the students to write, get the wazees to write. Wazee wa “Kaya” kila mtu, hapa hii sehemu ya Digo, nafikiri sehemu hii ni ya Digo. Lazima mkae mfikirie ile nilisema ilitosha, kama ulisema mujulishe mwingine na mwingine ajulishe mwingine aandike, ndiyo tuwe na kumbu kumbu huko, kweli makaratasi ya kufanyia kazi sisi, lakini pia kumbu kumbu za watu ambao watakuja baadaye watoto wa watoto wetu, ili waione kilikuwa ni kitu kizuri watu wetu walishiriki. Na ile nataka kumwambia, watu wanatoa maoni na vile mliona kama kwa hili jambo la majimbo, wanatoa hata na sehemu zenyewe. Mzee mwingine alizungumza mambo ya utamaduni. Wacha yeye achore aonyeshe utamaduni wa Coast Province unakaa vipi. Wacha mwingine, hata yule alikuwa ametoa hiyo mambo ya wa Kalenjini ni wangapi, wadigo wa Coast ni wangapi? Hiyo pia inafaa iwe kwa Memorandum, hiyo ni details za Memorandum. Lakini ikikaa tu vile tuko hivi na tuna

